# Asa Di Vaar

**Safari ya kuelekea kiroho**

**Tafsiri yaKiswahili**

SikhBookClub.com

SGGSONLINE.COM

# INDEX

1. Asa Di Vaar ---------------------------------------------------------------------- 1
2. Ardas-Sala ---------------------------------------------------------------------------- 98
3. Njia ya Nafsi --------------------------------------------------------------------- 103
4. Falsafa ya Safari -------------------------------------------------------------- 105
5. Wajibu wa Wanawake ------------------------------------------------------- 107
6. Umuhimu wa Turban -------------------------------------------------------- 111
7. Unyenyekevu msingi katika Safari yako ------------------------------------ 113

🙏🙏🙏We are distributing Free Gutkas, Divine message of the Guru globally in all the major languages, To Continue this Monumental task, please donate at https://sggsonline.com/donation

This Sewa has been done by Sewadars & SikhBookClub.

This text is only a translation and only gives the essence of the Guru's Divine word. For a more complete understanding, please read the Gurumukhi Sri Guru Granth Sahib Ji. If any errors are noticed, please notify us immediately via email at walnut@gmail.com.

Publisher

© Sikhbookclub.com

Chino, Ca 91710

ੴ ਸਤਿ ਨਾਮੁ ਕਰਤਾ ਪੁਰਖੁ ਨਿਰਭਉ ਨਿਰਵੈਰੁ ਅਕਾਲ ਮੂਰਤਿ ਅਜੂਨੀ ਸੈਭੰ ਗੁਰ ਪ੍ਰਸਾਦਿ ॥

ik-o$^{N}$kaar satnaam kartaa purakh nirbha-o nirvair akaal moorat ajoonee saibha$^{N}$ gur parsaad.

Kuna Mungu mmoja tu. Jina Lake ni 'Milele'. Yeye tu ndiye Muumba wa vyote na anaenea kote. Yeye yu bila hofu, bila uadui. Uwepo Wake unazidi wakati. Yeye amezidi mzunguko wa kuzaliwa na kufa. Yeye anajiangaza mwenyewe na anagunduliwa tu kwa Neema ya Guru.

ਆਸਾ ਮਹਲਾ ੧ ॥

aasaa mehlaa 1.

Raag Aasaa, Guru wa Kwanza:

ਵਾਰ ਸਲੋਕਾ ਨਾਲਿ ਸਲੋਕ ਭੀ ਮਹਲੇ ਪਹਿਲੇ ਕੇ ਲਿਖੇ ਟੁੰਡੇ ਅਸ ਰਾਜੈ ਕੀ ਧੁਨੀ ॥

vaar salokaa naal salok bhee mahlay pahilay kay likhay tunday as raajai kee Dhunee.

Vaara na slokas, slokas pia zimeandikwa na Guru wa Kwanza, inafaa kuimbwa kwa tuni ya Tunda-As Raajaa;

ਸਲੋਕੁ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਬਲਿਹਾਰੀ ਗੁਰ ਆਪਣੇ ਦਿਉਹਾੜੀ ਸਦ ਵਾਰ ॥

balihaaree gur aapnay di-uhaarhee sad vaar.

Ninajisalimisha kwa upendo kwa Guru wangu milele;

ਜਿਨਿ ਮਾਣਸ ਤੇ ਦੇਵਤੇ ਕੀਏ ਕਰਤ ਨ ਲਾਗੀ ਵਾਰ ॥੧॥

jin maanas tay dayvtay kee-ay karat na laagee vaar. ||1||

Ambaye amekweza kiroho binadamu kuwa malaika na hakuchukua wakati wowote kufanya hivi.

ਮਹਲਾ ੨ ॥

mehlaa 2.

Salok, Guru wa Pili:

ਜੇ ਸਉ ਚੰਦਾ ਉਗਵਹਿ ਸੂਰਜ ਚੜਹਿ ਹਜਾਰ ॥

jay sa-o chandaa ugvahi sooraj charheh hajaar.

Iwapo miezi mia moja ingetokea na jua elfu moja kupambazuka,

ਏਤੇ ਚਾਨਣ ਹੋਦਿਆਂ ਗੁਰ ਬਿਨੁ ਘੋਰ ਅੰਧਾਰ ॥੨॥

aytay chaanan hidi-aa$^{N}$ gur bin ghor anDhaar. ||2||

Hata na mwanga mwingi hivyo, bado kungekuwa na giza totoro ya ujinga pasipo mafundisho ya Guru. (kumaanisha kwamba haijalishi kiasi kipi cha maarifa tunaweza kupata kutoka vyanzo vingine, pasipo Guru hatuwezi kupata mwangaza wa kweli au hekima takatifu).

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਨਾਨਕ ਗੁਰੂ ਨ ਚੇਤਨੀ ਮਨਿ ਆਪਣੈ ਸੁਚੇਤ ॥

naanak guroo na chaytnee man aapnai suchayt.

Ee Nanak, wale ambao hawamkumbuki Guru na wanaojifikiria kuwa wajanja sana.

ਛੁਟੇ ਤਿਲ ਬੂਆੜ ਜਿਉ ਸੁੰਞੇ ਅੰਦਰਿ ਖੇਤ ॥

chhutay til boo-aarh ji-o sunjay andar khayt.

Hawatakikani kama mimea bandia ya ufuta inayosalia imeachwa bure shambani.

ਖੇਤੈ ਅੰਦਰਿ ਛੁਟਿਆ ਕਹੁ ਨਾਨਕ ਸਉ ਨਾਹ ॥

khaytai andar chhuti-aa kaho naanak sa-o naah.

Ee Nanak, wakiachwa pweke, wanaonekana kutaabika kama ambao badala ya mmoja wana mamia ya mabwana (na hivyo basi hawana bwana wa kweli)

ਫਲੀਅਹਿ ਫੁਲੀਅਹਿ ਬਪੁੜੇ ਭੀ ਤਨ ਵਿਚਿ ਸੁਆਹ ॥੩॥

falee-ah fulee-ah bapurhay bhee tan vich su-aah. ||3||

Mimea bandia ya ufuta inaonekana kutoa maua na kunawiri lakini imejawa na majivu tu. Vivyo hivyo wale, wasiofuata mafundisho ya Guru, wamekufa kiroho licha ya kuwa wamefanikiwa.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਆਪੀਨੑੈ ਆਪੁ ਸਾਜਿਓ ਆਪੀਨੑੈ ਰਚਿਓ ਨਾਉ ॥

aapeen$^{H}$ai aap saaji-o aapeen$^{H}$ai rachi-o naa-o.

Mungu alijiumba Mwenyewe, na Yeye Mwenyewe aliumba utukufu Wake.

ਦੁਯੀ ਕੁਦਰਤਿ ਸਾਜੀਐ ਕਰਿ ਆਸਣੁ ਡਿਠੋ ਚਾਉ ॥

duyee kudrat saajee-ai kar aasan ditho chaa-o.

Pili, Yeye alitengeneza uumbaji; akienea katika uumbaji, Yeye anautazama kwa furaha.

ਦਾਤਾ ਕਰਤਾ ਆਪਿ ਤੂੰ ਤੁਸਿ ਦੇਵਹਿ ਕਰਹਿ ਪਸਾਉ ॥

daataa kartaa aap too$^{N}$ tus dayveh karahi pasaa-o.

Ee Mungu, Wewe Mwenyewe ndiye mfadhili na Muumba wa viumbe vyote, na kwa Raha Yako, Wewe unatawaza neema Yako kwao.

ਤੂੰ ਜਾਣੋਈ ਸਭਸੈ ਦੇ ਲੈਸਹਿ ਜਿੰਦੁ ਕਵਾਉ ॥

too$^{N}$ jaano-ee sabhsai day laisahi jind kavaa-o.

Wewe ndiwe ujuaye yote; Wewe unatoa uhai, na kuuchukua tena kwa neno Lako tu.

ਕਰਿ ਆਸਣੁ ਡਿਠੋ ਚਾਉ ॥੧॥

kar aasan ditho chaa-o. ||1||

Kwa kuenea katika uumbaji, Wewe unatazama mchezo (wa dunia) kwa shauku

ਸਲੋਕੁ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਸਚੇ ਤੇਰੇ ਖੰਡ ਸਚੇ ਬ੍ਰਹਮੰਡ ॥

sachay tayray khand sachay barahmand.

Ee Mungu Mwenyezi, mabara Yako ni ya Kweli (ya Milele), na wa Kweli ni Ulimwengu Wako.

ਸਚੇ ਤੇਰੇ ਲੋਅ ਸਚੇ ਆਕਾਰ ॥

sachay tayray lo-a sachay aakaar.

Ya Kweli (Milele) ni dunia Zako, na uumbaji Wako ni wa Kweli.

ਸਚੇ ਤੇਰੇ ਕਰਣੇ ਸਰਬ ਬੀਚਾਰ ॥

sachay tayray karnay sarab beechaar.

Ya Kweli ni matendo Yako na fikira Zako zote.

ਸਚਾ ਤੇਰਾ ਅਮਰੁ ਸਚਾ ਦੀਬਾਣੁ ॥

sachaa tayraa amar sachaa deebaan.

Ya Kweli ni Amri Yako na mahakama Yako ni ya Kweli.

ਸਚਾ ਤੇਰਾ ਹੁਕਮੁ ਸਚਾ ਫੁਰਮਾਣੁ ॥

sachaa tayraa hukam sachaa furmaan.

Kweli ni Amri ya mapenzi Yako, Kweli ni Utaratibu Wako,

ਸਚਾ ਤੇਰਾ ਕਰਮੁ ਸਚਾ ਨੀਸਾਣੁ ॥

sachaa tayraa karam sachaa neesaan.

Kweli ni Huruma Yako, Za Kweli ni thawabu Zako (ishara ya neema Yako).

ਸਚੇ ਤੁਧੁ ਆਖਹਿ ਲਖ ਕਰੋੜਿ ॥

sachay tuDh aakhahi lakh karorh.

Mamilioni ya watu wanaotafakari kukuhusu pia ni wa kweli.

ਸਚੈ ਸਭਿ ਤਾਣਿ ਸਚੈ ਸਭਿ ਜੋਰਿ ॥

sachai sabh taan sachai sabh jor.

Uumbaji wote unategemea nguvu na uweza Wako.

ਸਚੀ ਤੇਰੀ ਸਿਫਤਿ ਸਚੀ ਸਾਲਾਹ ॥

sachee tayree sifat sachee saalaah.

Ya Kweli ni Sifa Yako, Kweli ni Ibada Yako.

ਸਚੀ ਤੇਰੀ ਕੁਦਰਤਿ ਸਚੇ ਪਾਤਿਸਾਹ ॥

sachee tayree kudrat sachay paatisaah.

Ee Mfalme wa Kweli, uumbaji Wako unadumu milele.

ਨਾਨਕ ਸਚੁ ਧਿਆਇਨਿ ਸਚੁ ॥

naanak sach Dhi-aa-in sach.

Ee Nanak, wale wanaotafakari kuhusu Yule wa Kweli kwa kujitoa kwa upendo wanakuwa wa Kweli wenyewe (wanaungana na Mungu)

ਜੋ ਮਰਿ ਜੰਮੇ ਸੁ ਕਚੁ ਨਿਕਚੁ ॥੧॥

jo mar jammay so kach nikach. ||1||

Lakini wale wanaopitia mzunguko wa kuzaliwa na kufa wananaswa katika udanganyifu na hawawezi kuungana na Mungu.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਵਡੀ ਵਡਿਆਈ ਜਾ ਵਡਾ ਨਾਉ ॥

vadee vadi-aa-ee jaa vadaa naa-o.

Ukuu wake ni mkuu, ni mkuu kama Utukufu Wake.

ਵਡੀ ਵਡਿਆਈ ਜਾ ਸਚੁ ਨਿਆਉ ॥

vadee vadi-aa-ee jaa sach ni-aa-o.

Ukuu wake ni mkuu, ni wa kweli kama haki Yake.

ਵਡੀ ਵਡਿਆਈ ਜਾ ਨਿਹਚਲ ਥਾਉ ॥

vadee vadi-aa-ee jaa nihchal thaa-o.

Ukuu wake ni mkuu, unaodumu kama makao Yake.

ਵਡੀ ਵਡਿਆਈ ਜਾਣੈ ਆਲਾਉ ॥

vadee vadi-aa-ee jaanai aalaa-o.

Ukuu wake ni mkuu, kama Yeye anavyofahamu maombi yetu.

ਵਡੀ ਵਡਿਆਈ ਬੁਝੈ ਸਭਿ ਭਾਉ ॥

vadee vadi-aa-ee bujhai sabh bhaa-o.

Mkuu ni utukufu Wake, kama Yeye anavyoelewa hisia zetu zote.

ਵਡੀ ਵਡਿਆਈ ਜਾ ਪੁਛਿ ਨ ਦਾਤਿ ॥

vadee vadi-aa-ee jaa puchh na daat.

Mkuu ni ukuu Wake, kama Yeye anavyotoa bila kuulizwa.

ਵਡੀ ਵਡਿਆਈ ਜਾ ਆਪੇ ਆਪਿ ॥

vadee vadi-aa-ee jaa aapay aap.

Mkuu ni utukufu Wake, kama Yeye Mwenyewe alivyo vyote katika vyote.

ਨਾਨਕ ਕਾਰ ਨ ਕਥਨੀ ਜਾਇ ॥

naanak kaar na kathnee jaa-ay.

Ee Nanak, vitendo Vyake haviwezi kuelezwa.

ਕੀਤਾ ਕਰਣਾ ਸਰਬ ਰਜਾਇ ॥੨॥

keetaa karnaa sarab rajaa-ay. ||2||

Chochote alichokifanya, au atakachofanya, vyote ni kwa Mapenzi Yake Mwenyewe.

ਮਹਲਾ ੨ ॥

mehlaa 2.

Salok, Guru wa Pili:

ਇਹੁ ਜਗੁ ਸਚੈ ਕੀ ਹੈ ਕੋਠੜੀ ਸਚੇ ਕਾ ਵਿਚਿ ਵਾਸੁ ॥

ih jag sachai kee hai koth-rhee sachay kaa vich vaas.

Dunia hii ni makao ya Mungu wa Milele na Yeye anaishi ndani yake.

ਇਕਨ੍ਹਾ ਹੁਕਮਿ ਸਮਾਇ ਲਏ ਇਕਨ੍ਹਾ ਹੁਕਮੇ ਕਰੇ ਵਿਣਾਸੁ ॥

ikn$^{H}$aa hukam samaa-ay la-ay ikn$^{H}$aa hukmay karay vinaas.

Kwa Amri Yake, wengine wanaunganishwa na Yeye, na wengine, kwa Amri Yake, wanaangamizwa.

ਇਕਨ੍ਹਾ ਭਾਣੈ ਕਢਿ ਲਏ ਇਕਨ੍ਹਾ ਮਾਇਆ ਵਿਚਿ ਨਿਵਾਸੁ ॥

ikn$^{H}$aa bhaanai kadh la-ay ikn$^{H}$aa maa-i-aa vich nivaas.

Wengine, kwa Mapenzi Yake, wanaokolewa kutoka kwa viambatisho vya kidunia, wakati wengine wanafanywa wabaki wamezama katika hivyo.

ਏਵ ਭਿ ਆਖਿ ਨ ਜਾਪਈ ਜਿ ਕਿਸੈ ਆਣੇ ਰਾਸਿ ॥

ayv bhe aakh na jaap-ee je kisai aanay raas.

Hakuna mtu anayeweza kusema nani ataokolewa kutoka kwa viambatisho vya kidunia.

ਨਾਨਕ ਗੁਰਮੁਖਿ ਜਾਣੀਐ ਜਾ ਕਉ ਆਪਿ ਕਰੇ ਪਰਗਾਸੁ ॥੩॥

naanak gurmukh jaanee-ai jaa ka-o aap karay pargaas. ||3||

Ee Nanak, mfuasi huyo pekee wa Guru anakuja kujua kuhusu siri hii ambaye Yeye anamwangazia kwa maarifa maTakatifu.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਨਾਨਕ ਜੀਅ ਉਪਾਇ ਕੈ ਲਿਖਿ ਨਾਵੈ ਧਰਮੁ ਬਹਾਲਿਆ ॥

naanak jee-a upaa-ay kai likh naavai Dharam bahaali-aa.

Ee Nanak, aliyeumba roho, Mungu ameteua hakimu wa haki arekodi nakala za vitendo vyao.

ਓਥੈ ਸਚੇ ਹੀ ਸਚਿ ਨਿਬੜੈ ਚੁਣਿ ਵਖਿ ਕਢੇ ਜਜਮਾਲਿਆ ॥

othai sachay hee sach nibrhai chun vakh kadhay jajmaali-aa.

Hapo, Wanadamu wanahukumiwa tu kwa msingi wa ukweli na ukweli tu; waongo (waovu) wanatiwa alama na kutenganishwa na walio wa kweli.

ਥਾਉ ਨ ਪਾਇਨਿ ਕੂੜਿਆਰ ਮੁਹ ਕਾਲ੍ਹੈ ਦੋਜਕਿ ਚਾਲਿਆ ॥

thaa-o na paa-in koorhi-aar muh kaal[H]ai dojak chaali-aa.

Wale wasio wa kweli hawapati nafasi katika mahakama ya Mungu na wanaondoshwa ili wateseke katika fedheha kubwa.

ਤੇਰੈ ਨਾਇ ਰਤੇ ਸੇ ਜਿਣਿ ਗਏ ਹਾਰਿ ਗਏ ਸਿ ਠਗਣ ਵਾਲਿਆ ॥

tayrai naa-ay ratay say jin ga-ay haar ga-ay se thagan vaali-aa.

Wale ambao wamepenyezwa na upendo wa Jina Lako huibuka washindi, wakati waongo wanapoteza mchezo wa maisha.

ਲਿਖਿ ਨਾਵੈ ਧਰਮੁ ਬਹਾਲਿਆ ॥੨॥

likh naavai Dharam bahaali-aa. ||2||

Ee Mungu, Wewe umeteua Hakimu wa Haki kurekodi nakala za vitendo vya wanadamu.

ਸਲੋਕ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਵਿਸਮਾਦੁ ਨਾਦ ਵਿਸਮਾਦੁ ਵੇਦ ॥

vismaad naad vismaad vayd.

Inastaajabisha mikondo mingi ya sauti, yanastaajabisha maarifa ya Vedas.

ਵਿਸਮਾਦੁ ਜੀਅ ਵਿਸਮਾਦੁ ਭੇਦ ॥

vismaad jee-a vismaad bhayd.

Vizuri ni vuimbe, nzuri ni spishi.

ਵਿਸਮਾਦੁ ਰੂਪ ਵਿਸਮਾਦੁ ਰੰਗ ॥

vismaad roop vismaad rang.

Miundo ni mizuri, na rangi ni nzuri.

ਵਿਸਮਾਦੁ ਨਾਗੇ ਫਿਰਹਿ ਜੰਤ ॥

vismaad naagay fireh jant.

Kwa kutazama viumbe wengi mno wakizurura uchi, nimo katika hali ya kustaajabu.

ਵਿਸਮਾਦੁ ਪਉਣੁ ਵਿਸਮਾਦੁ ਪਾਣੀ ॥

vismaad pa-un vismaad paanee.

Ninastaajabu nikitazama kwamba mahali fulani upepo unavuma na kwingine maji yanatiririka,

ਵਿਸਮਾਦੁ ਅਗਨੀ ਖੇਡਹਿ ਵਿਡਾਣੀ ॥

vismaad agnee khaydeh vidaanee.

Inastaajabisha, jinsi moto unavyoonyesha mwonyesho wake mwenyewe wa ajabu.

ਵਿਸਮਾਦੁ ਧਰਤੀ ਵਿਸਮਾਦੁ ਖਾਣੀ ॥

vismaad Dhartee vismaad khaanee.

Ninastaajabu kwa furaha ninapotazama dunia hii ikitunza viumbe kutoka vyanzo vyote vya uhai.

ਵਿਸਮਾਦੁ ਸਾਦਿ ਲਗਹਿ ਪਰਾਣੀ ॥

vismaad saad lageh paraanee.

Inastaajabisha, jinsi wanadamu wanavyohusishwa katika kufurahia Baraka Zako.

ਵਿਸਮਾਦੁ ਸੰਜੋਗੁ ਵਿਸਮਾਦੁ ਵਿਜੋਗੁ ॥

vismaad sanjog vismaad vijog.

Inastaajabisha mchakato ambao kwa kuupitia watu wanaunganishwa na kutenganishwa

ਵਿਸਮਾਦੁ ਭੁਖ ਵਿਸਮਾਦੁ ਭੋਗੁ ॥

vismaad bhukh vismaad bhog.

Ee Mungu, ni vigumu kuamini kwamba mahali pengine kuna njaa nyingi mno na mahali pengine vitu vinafurahiwa kwa wingi.

ਵਿਸਮਾਦੁ ਸਿਫਤਿ ਵਿਸਮਾਦੁ ਸਾਲਾਹ ॥

vismaad sifat vismaad saalaah.

Mahali Fulani Muumba anasifiwa na kutukuzwa,

ਵਿਸਮਾਦੁ ਉਝੜ ਵਿਸਮਾਦੁ ਰਾਹ ॥

vismaad ujharh vismaad raah.

Kwingine kuna nyika ilhali kwingine kuna njia zilizotengenezwa vizuri. Inastaajabisha tu kuona mchezo huu Wako wa ajabu.

ਵਿਸਮਾਦੁ ਨੇੜੈ ਵਿਸਮਾਦੁ ਦੂਰਿ ॥

vismaad nayrhai vismaad door.

Inastaajabisha kwamba mtu anasema kwa Wewe yu karibu; mwingine anasema kwamba Wewe upo mbali mno,

ਵਿਸਮਾਦੁ ਦੇਖੈ ਹਾਜਰਾ ਹਜੂਰਿ ॥

vismaad daykhai haajraa hajoor.

Wakati wengine pia wanakuona Wewe kando yao (ukienea kote).

ਵੇਖਿ ਵਿਡਾਣੁ ਰਹਿਆ ਵਿਸਮਾਦੁ ॥

vaykh vidaan rahi-aa vismaad.

Nikitazama ajabu hizi, ninastaajabishwa.

ਨਾਨਕ ਬੁਝਣੁ ਪੂਰੈ ਭਾਗਿ ॥੧॥

naanak bujhan poorai bhaag. ||1||

Ee Nanak, wale wanaoelewa ajabu hizi Zako wamebarikiwa na hatima kamili.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, ya Guru wa Kwanza:

ਕੁਦਰਤਿ ਦਿਸੈ ਕੁਦਰਤਿ ਸੁਣੀਐ ਕੁਦਰਤਿ ਭਉ ਸੁਖ ਸਾਰੁ ॥

kudrat disai kudrat sunee-ai kudrat bha-o sukh saar.

Chochote kinachoonekana, au chochote kinachosikika kwenye mazingira ni ajabu ya nguvu Yako. Hofu kwa heshima Yako ambayo ndiyo kiini cha amani, yote ni mchezo Wako.

ਕੁਦਰਤਿ ਪਾਤਾਲੀ ਆਕਾਸੀ ਕੁਦਰਤਿ ਸਰਬ ਆਕਾਰੁ ॥

kudrat paataalee aakaasee kudrat sarab aakaar.

Ni nguvu Yako, ambayo inaonyeshwa katika maeneo ya chini ya dunia na angani, na katika miundo yote ya ulimwengu.

ਕੁਦਰਤਿ ਵੇਦ ਪੁਰਾਣ ਕਤੇਬਾ ਕੁਦਰਤਿ ਸਰਬ ਵੀਚਾਰੁ ॥

kudrat vayd puraan kataybaa kudrat sarab veechaar.

Vedas, puranas, vitabu vya kisemiti na mawazo yaliyoelezwa ndani yao, yamewezekana kwa nguvu Yako.

ਕੁਦਰਤਿ ਖਾਣਾ ਪੀਣਾ ਪੈਨ੍ਣੁ ਕੁਦਰਤਿ ਸਰਬ ਪਿਆਰੁ ॥

kudrat khaanaa peenaa pain[H]an kudrat sarab pi-aar.

Ni nguvu Yako iliyopo, ambayo inatenda kazi kuwezesha dhana ya kula, kunywa, kuvaa na kuhisi upendo katika viumbe vinavyoishi.

ਕੁਦਰਤਿ ਜਾਤੀ ਜਿਨਸੀ ਰੰਗੀ ਕੁਦਰਤਿ ਜੀਅ ਜਹਾਨ ॥

kudrat jaatee jinsee rangee kudrat jee-a jahaan.

Kwa Nguvu Yako kunatokea spishi za aina na rangi zote; kwa Nguvu Yako viumbe vinavyoishi vya dunia vinakuwepo.

ਕੁਦਰਤਿ ਨੇਕੀਆ ਕੁਦਰਤਿ ਬਦੀਆ ਕੁਦਰਤਿ ਮਾਨੁ ਅਭਿਮਾਨੁ ॥

kudrat naykee-aa kudrat badee-aa kudrat maan abhimaan.

Hata matendo yote mazuri, maovu, staha na fedheha zote zinatendeka kulingana na Nguvu na mapenzi Yako.

ਕੁਦਰਤਿ ਪਉਣੁ ਪਾਣੀ ਬੈਸੰਤਰੁ ਕੁਦਰਤਿ ਧਰਤੀ ਖਾਕੁ ॥

kudrat pa-un paanee baisantar kudrat Dhartee khaak.

Kwa Nguvu Yako upepo, maji na moto upo; kwa Nguvu Yako ardhi na vumbi ipo.

ਸਭ ਤੇਰੀ ਕੁਦਰਤਿ ਤੂੰ ਕਾਦਿਰੁ ਕਰਤਾ ਪਾਕੀ ਨਾਈ ਪਾਕੁ ॥

sabh tayree kudrat too$^N$ kaadir kartaa paakee naa-ee paak.

Ee Mungu, kila kitu kipo chini ya Nguvu Yako, Wewe ndiwe Muumba mwenye nguvu yote. Jina Lako ndilo Takatifu kabisa kwa yote.

ਨਾਨਕ ਹੁਕਮੈ ਅੰਦਰਿ ਵੇਖੈ ਵਰਤੈ ਤਾਕੋ ਤਾਕੁ ॥੨॥

naanak hukmai andar vaykhai vartai taako taak. ||2||

Ee Nanak, Yeye anathamini uumbaji kulingana na amri Yake, na anaenea kote Yeye Mwenyewe.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਆਪੀਨੈੑ ਭੋਗ ਭੋਗਿ ਕੈ ਹੋਇ ਭਸਮੜਿ ਭਉਰੁ ਸਿਧਾਇਆ ॥

aapeen$^H$ai bhog bhog kai ho-ay bhasmarh bha-ur siDhaa-i-aa.

Baada ya kuishi kupitia maumivu na raha za maisha, mwili wa binadamu unakuwa mrundo wa mchanga na roho inaondoka.

ਵਡਾ ਹੋਆ ਦੁਨੀਦਾਰੁ ਗਲਿ ਸੰਗਲੁ ਘਤਿ ਚਲਾਇਆ ॥

vadaa ho-aa duneedaar gal sangal ghat chalaa-i-aa.

Mtu aliyenaswa katika shughuli za kidunia anapofariki, yeye anaongozwa kwa mahakama ya Hakimu wa haki.

ਅਗੈ ਕਰਣੀ ਕੀਰਤਿ ਵਾਚੀਐ ਬਹਿ ਲੇਖਾ ਕਰਿ ਸਮਝਾਇਆ ॥

agai karnee keerat vaachee-ai bahi laykhaa kar samjhaa-i-aa.

Hapo, vitendo vyake vizuri na vibaya vinahesabiwa na kuelezwa kwake.

ਥਾਉ ਨ ਹੋਵੀ ਪਉਦੀਈ ਹੁਣਿ ਸੁਣੀਐ ਕਿਆ ਰੂਆਇਆ ॥

thaa-o na hovee pa-udee-ee hun sunee-ai ki-aa roo-aa-i-aa.

Iwapo vitendo vyake vibaya vinazidi vitendo vizuri, Yeye anapewa adhabu kali. Yeye hapati pahali pa kujificha na hakuna anayesikia vilio vyake vya uchungu.

ਮਨਿ ਅੰਧੈ ਜਨਮੁ ਗਵਾਇਆ ॥੩॥

man anDhai janam gavaa-i-aa. ||3||

Kutokana na ujinga yeye ameharibu maisha ya kibinadamu bure.

ਸਲੋਕ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਭੈ ਵਿਚਿ ਪਵਣੁ ਵਹੈ ਸਦਵਾਉ ॥

bhai vich pavan vahai sadvaa-o.

Katika hofu kwa heshima ya Mungu, upepo unaendelea kuvuma milele.

ਭੈ ਵਿਚਿ ਚਲਹਿ ਲਖ ਦਰੀਆਉ ॥

bhai vich chaleh lakh daree-aa-o.

Katika hofu kwa heshima (chini ya mapenzi) ya Mungu, maelfu ya mito yanatiririka.

ਭੈ ਵਿਚਿ ਅਗਨਿ ਕਢੈ ਵੇਗਾਰਿ ॥

bhai vich agan kadhai vaygaar.

Katika hofu kwa heshima ya Mungu, moto unatenda kazi ulioteuliwa kufanya.

ਭੈ ਵਿਚਿ ਧਰਤੀ ਦਬੀ ਭਾਰਿ ॥

bhai vich Dhartee dabee bhaar.

Katika hofu kwa heshima ya Mungu, dunia inahimili mzigo wa uumbaji.

ਭੈ ਵਿਚਿ ਇੰਦੁ ਫਿਰੈ ਸਿਰ ਭਾਰਿ ॥

bhai vich ind firai sir bhaar.

Katika hofu kwa heshima ya Mungu (chini ya amri Yake), mfalme Indra, mungu wa mvua katika muundo wa wingu ananing'inia kichwa chini, kana kwamba linatembea kwenye kichwa chake.

ਭੈ ਵਿਚਿ ਰਾਜਾ ਧਰਮ ਦੁਆਰੁ ॥

bhai vich raajaa Dharam du-aar.

Katika Hofu ya Mungu, Hakimu wa Haki wa Dharma anasimama mlangoni Pake.

ਭੈ ਵਿਚਿ ਸੂਰਜੁ ਭੈ ਵਿਚਿ ਚੰਦੁ ॥

bhai vich sooraj bhai vich chand.

Chini ya Amri Yake, jua linang'aa na mwezi unaakisi.

ਕੋਹ ਕਰੋੜੀ ਚਲਤ ਨ ਅੰਤੁ ॥

koh karorhee chalat na ant.

Wanasafiri mamilioni ya maili, bila mwisho.

ਭੈ ਵਿਚਿ ਸਿਧ ਬੁਧ ਸੁਰ ਨਾਥ ॥

bhai vich siDh buDh sur naath.

Katika hofu kwa heshima ya Mungu (chini ya amri Yake), wanaishi Wasiddha, Buddha. Miungu-nusu na Mayogi.

ਭੈ ਵਿਚਿ ਆਡਾਣੇ ਆਕਾਸ ॥

bhai vich aadaanay aakaas.

Ni katika hofu kwa heshima Yake ambapo anga imeenezwa juu ya dunia

ਭੈ ਵਿਚਿ ਜੋਧ ਮਹਾਬਲ ਸੂਰ ॥

bhai vich joDh mahaabal soor.

Katika mapenzi ya Mungu, kuna wapiganaji na mashujaa wenye nguvu mno.

ਭੈ ਵਿਚਿ ਆਵਹਿ ਜਾਵਹਿ ਪੂਰ ॥

bhai vich aavahi jaaveh poor.

Katika hofu kwa heshima Yake, halaiki za wanadamu na viumbe wanazaliwa na kufa.

ਸਗਲਿਆ ਭਉ ਲਿਖਿਆ ਸਿਰਿ ਲੇਖੁ ॥

sagli-aa bha-o likhi-aa sir laykh.

Uumbaji mzima unatenda kazi chini ya hofu kwa heshima (amri) Yake.

ਨਾਨਕ ਨਿਰਭਉ ਨਿਰੰਕਾਰੁ ਸਚੁ ਏਕੁ ॥੧॥

naanak nirbha-o nirankaar sach ayk. ||1||

Ee Nanak, ni Mungu wa milele asiye na muundo peke yake asiye na hofu yoyote.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਨਾਨਕ ਨਿਰਭਉ ਨਿਰੰਕਾਰੁ ਹੋਰਿ ਕੇਤੇ ਰਾਮ ਰਵਾਲ ॥

naanak nirbha-o nirankaar hor kaytay raam ravaal.

Ee Nanak, ni Mungu asiye na muundo peke yake, ambaye hana hofu; maelfu ya miungu wengine hawana maana mbele Yake.

ਕੇਤੀਆ ਕੰਨ੍ ਕਹਾਣੀਆ ਕੇਤੇ ਬੇਦ ਬੀਚਾਰ ॥

kaytee-aa kan$^{H}$ kahaanee-aa kaytay bayd beechaar.

Kuna hadithi nyingi mno kuhusu Krishna, wengi sana wanaotafakari juu ya Vedas.

ਕੇਤੇ ਨਚਹਿ ਮੰਗਤੇ ਗਿੜਿ ਮੁੜਿ ਪੂਰਹਿ ਤਾਲ ॥

kaytay nacheh mangtay girh murh pooreh taal.

Waombaji wengi sana wanachezacheza, wakizunguka kwa mpigo wa ngoma.

ਬਾਜਾਰੀ ਬਾਜਾਰ ਮਹਿ ਆਇ ਕਢਹਿ ਬਾਜਾਰ ॥

baajaaree baajaar meh aa-ay kadheh baajaar.

Wafanya mazingaombwe wanafanya mazingaombwe yao sokoni, wakitengeneza njozi ya uongo.

ਗਾਵਹਿ ਰਾਜੇ ਰਾਣੀਆ ਬੋਲਹਿ ਆਲ ਪਤਾਲ ॥

gaavahi raajay raanee-aa boleh aal pataal.

Wanaimba kuhusu wafalme na malkia, na kusimulia hadithi zisizo na maana.

ਲਖ ਟਕਿਆ ਕੇ ਮੁੰਦੜੇ ਲਖ ਟਕਿਆ ਕੇ ਹਾਰ ॥

lakh taki-aa kay mund-rhay lakh taki-aa kay haar.

Wanavaa vipuli na mikufu ya bei ghali.

ਜਿਤੁ ਤਨਿ ਪਾਈਅਹਿ ਨਾਨਕਾ ਸੇ ਤਨ ਹੋਵਹਿ ਛਾਰ ॥

jit tan paa-ee-ah naankaa say tan hoveh chhaar.

Ee Nanak, miili, ambayo inavalishwa vito, mwishowe inakuwa majivu.

ਗਿਆਨੁ ਨ ਗਲੀਈ ਢੂਢੀਐ ਕਥਨਾ ਕਰੜਾ ਸਾਰੁ ॥

gi-aan na galee-ee dhoodhee-ai kathnaa karrhaa saar.

Hekima takatifu haiwezi kupatwa kwa maneno matupu. Kueleza jinsi ya kupata maarifa matakatifu ni vigumu mno kama kutafuna chuma.

ਕਰਮਿ ਮਿਲੈ ਤਾ ਪਾਈਐ ਹੋਰ ਹਿਕਮਤਿ ਹੁਕਮੁ ਖੁਆਰੁ ॥੨॥

karam milai taa paa-ee-ai hor hikmat hukam khu-aar. ||2||

Ni wakati tu ambapo tumebarikiwa na Neema Yake, ambapo tunapata hekima takatifu; jitihada yote nyingine na amri hupelekea fadhaiko tu.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਨਦਰਿ ਕਰਹਿ ਜੇ ਆਪਣੀ ਤਾ ਨਦਰੀ ਸਤਿਗੁਰੁ ਪਾਇਆ ॥

nadar karahi jay aapnee taa nadree satgur paa-i-aa.

Ee Mungu, unapotupa Mtazamo Wako wa Neema, ndipo kwa Neema Yako mtu anakutana na Guru wa kweli.

ਏਹੁ ਜੀਉ ਬਹੁਤੇ ਜਨਮ ਭਰੰਮਿਆ ਤਾ ਸਤਿਗੁਰਿ ਸਬਦੁ ਸੁਣਾਇਆ ॥

ayhu jee-o bahutay janam bharammi-aa taa satgur sabad sunaa-i-aa.

Roho hii ilizurura kupitia kuzaliwa kwingi, hadi Guru wa Kweli alipoitamkia Neno Takatifu.

ਸਤਿਗੁਰ ਜੇਵਡੁ ਦਾਤਾ ਕੋ ਨਹੀ ਸਭਿ ਸੁਣਿਅਹੁ ਲੋਕ ਸਬਾਇਆ ॥

satgur jayvad daataa ko nahee sabh suni-ahu lok sabaa-i-aa.

Enyi watu wote sikilizeni kwa makini, hakuna mfadhili mwengine aliye mkuu kama Guru wa kweli.

ਸਤਿਗੁਰਿ ਮਿਲਿਐ ਸਚੁ ਪਾਇਆ ਜਿਨ੍ੀ ਵਿਚਹੁ ਆਪੁ ਗਵਾਇਆ ॥

satgur mili-ai sach paa-i-aa jin[H]ee vichahu aap gavaa-i-aa.

Wale ambao wameondoa majivuno kutoka ndani mwao, kwa kukutana na Guru wa kweli, wamemgundua Mungu.

ਜਿਨਿ ਸਚੋ ਸਚੁ ਬੁਝਾਇਆ ॥੪॥

jin sacho sach bujhaa-i-aa. ||4||

Guru wa kweli pekee ndiye hudhihirisha uelewa kuhusu Mungu wa Milele.

ਸਲੋਕ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਘੜੀਆ ਸਭੇ ਗੋਪੀਆ ਪਹਰ ਕੰਨ੍ ਗੋਪਾਲ ॥

gharhee-aa sabhay gopee-aa pahar kan[H] gopaal.

Dunia hii ni kama mchezo wa Mungu ambayo ndani mwake Gharian zote (muda wa dakika २४) ni kama Gopis au vijakazi wa maziwa na Pehari zote (muda wa saa tatu) ni kama Krishana.

ਗਹਣੇ ਪਉਣੁ ਪਾਣੀ ਬੈਸੰਤਰੁ ਚੰਦੁ ਸੂਰਜੁ ਅਵਤਾਰ ॥

gahnay pa-un paanee baisantar chand sooraj avtaar.

Katika mchezo huu wa kidunia, upepo, maji na moto ni kama mapambo yanayovaliwa na Wagopi. Jua na mwezi ni kama umwilisho mara mbili.

ਸਗਲੀ ਧਰਤੀ ਮਾਲੁ ਧਨੁ ਵਰਤਣਿ ਸਰਬ ਜੰਜਾਲ ॥

saglee Dhartee maal Dhan vartan sarab janjaal.

Dunia nzima inatoa rasilimali zinazohitajika, na misongamano ya kidunia ni bidhaa zinazohitajika katika kupanga mchezo huu.

ਨਾਨਕ ਮੁਸੈ ਗਿਆਨ ਵਿਹੂਣੀ ਖਾਇ ਗਇਆ ਜਮਕਾਲੁ ॥੧॥

naanak musai gi-aan vihoonee khaa-ay ga-i-aa jamkaal. ||1||

(katika mchezo huu wa njozi za kidunia) Ee Nanak, pasipo maarifa matakatifu, ubinadamu wote unadanganywa na kuangamizwa na pepo wa mauti.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਵਾਇਨਿ ਚੇਲੇ ਨਚਨਿ ਗੁਰ ॥

vaa-in chaylay nachan gur.

Wakati inapangwa mionyesho hii, wanafunzi wanacheza muziki, na maguru wanadensi.

ਪੈਰ ਹਲਾਇਨਿ ਫੇਰਨ੍ਹਿ ਸਿਰ ॥

pair halaa-in fayrni[H] sir.

Wakati wanadensi wanapiga piga miguu yao na kuzungusha vichwa vyao.

ਉਡਿ ਉਡਿ ਰਾਵਾ ਝਾਟੈ ਪਾਇ ॥

ud ud raavaa jhaatai paa-ay.

Mchanga unaruka na kuanguka vichwani pao.

ਵੇਖੈ ਲੋਕੁ ਹਸੈ ਘਰਿ ਜਾਇ ॥

vaykhai lok hasai ghar jaa-ay.

Wakiwatazama, watu wanacheka, na kasha wanaenda nyumbani.

ਰੋਟੀਆ ਕਾਰਣਿ ਪੂਰਹਿ ਤਾਲ ॥

rotee-aa kaaran pooreh taal.

Wanapiga ngoma kwa ajili ya mkate (ili kuchuma riziki).

ਆਪੁ ਪਛਾੜਹਿ ਧਰਤੀ ਨਾਲਿ ॥

aap pachhaarheh Dhartee naal.

Wanajirusha chini kwenye ardhi.

ਗਾਵਨਿ ਗੋਪੀਆ ਗਾਵਨਿ ਕਾਨ੍ ॥

gaavan gopee-aa gaavan kaan[H].

Wanaimba wakivaa kama vijakazi wa maziwa na Krishna.

ਗਾਵਨਿ ਸੀਤਾ ਰਾਜੇ ਰਾਮ ॥

gaavan seetaa raajay raam.

Wanaimba wakiwa wamevaa kama Sitas, Ramas na wafalme wengine.

ਨਿਰਭਉ ਨਿਰੰਕਾਰੁ ਸਚੁ ਨਾਮੁ ॥

nirbha-o nirankaar sach naam.

Mungu hana woga wala muundo; Jina Lake ni la Kweli.

ਜਾ ਕਾ ਕੀਆ ਸਗਲ ਜਹਾਨੁ ॥

jaa kaa kee-aa sagal jahaan.

Ulimwengu mzima ni Uumbaji Wake.

ਸੇਵਕ ਸੇਵਹਿ ਕਰਮਿ ਚੜਾਉ ॥

sayvak sayveh karam charhaa-o.

Watawa hao tu wanamkumbuka Yeye kwa ujitoaji wa upendo, ambao, kwa Neema Yake ni wachangamfu.

ਭਿੰਨੀ ਰੈਣਿ ਜਿਨ੍ਾ ਮਨਿ ਚਾਉ ॥

bhinnee rain jin[H]aa man chaa-o.

Wao, ambao akilini mwao kuna hamu kali ya kumpendeza Mungu; maisha yao yamepambwa kwa kiburudisho Takatifu.

ਸਿਖੀ ਸਿਖਿਆ ਗੁਰ ਵੀਚਾਰਿ ॥

sikhee sikhi-aa gur veechaar.

Kwa kutafakari Guru, wale ambao wamejifunza mafundisho haya;

ਨਦਰੀ ਕਰਮਿ ਲਘਾਏ ਪਾਰਿ ॥

nadree karam laghaa-ay paar.

Akiwajalia Neema Yake, Mungu anawasaidia kuvuka bahari ya kidunia ya maovu.

ਕੋਲੂ ਚਰਖਾ ਚਕੀ ਚਕੁ ॥

koloo charkhaa chakee chak.

Shinikizo la mafuta, dulabu, mawe ya kusaga, gurudumu la mfinyanzi,

ਥਲ ਵਾਰੋਲੇ ਬਹੁਤੁ ਅਨੰਤੁ ॥

thal vaarolay bahut anant.

Vimbunga vingi, visivyohesabika katika jangwa.

ਲਾਟੂ ਮਾਧਾਣੀਆ ਅਨਗਾਹ ॥

laatoo maaDhaanee-aa angaah.

vifuniko vinavyozunguka, vijiti vya kusukasuka, mashine za kupura,

ਪੰਖੀ ਭਉਦੀਆ ਲੈਨਿ ਨ ਸਾਹ ॥

pankhee bha-udee-aa lain na saah.

kuanguka bila hewa kwa ndege,

ਸੂਐ ਚਾੜਿ ਭਵਾਈਅਹਿ ਜੰਤ ॥

soo-ai chaarh bhavaa-ee-ah jant.

na viumbe wanaozunguka zunguka kwenye pia,

ਨਾਨਕ ਭਉਦਿਆ ਗਣਤ ਨ ਅੰਤ ॥

naanak bha-udi-aa ganat na ant.

Ee Nanak, hakuna kikomo kwa idadi ya vitu na viumbe, ambao wanazungushwa zungushwa.

ਬੰਧਨ ਬੰਧਿ ਭਵਾਏ ਸੋਇ ॥

banDhan banDh bhavaa-ay so-ay.

Akiwafunga viumbe katika Vifungo vya Maya, Mungu anawazungusha zungusha.

ਪਇਐ ਕਿਰਤਿ ਨਚੈ ਸਭੁ ਕੋਇ ॥

pa-i-ai kirat nachai sabh ko-ay.

Kila mtu anazurura kote kulingana na hatima ambayo msingi wake ni vitendo vyake vya awali.

ਨਚਿ ਨਚਿ ਹਸਹਿ ਚਲਹਿ ਸੇ ਰੋਇ ॥

nach nach haseh chaleh say ro-ay.

Wale wanaozurura maisha yao yote wataombolea katika kuondoka kwao mwishowe.

ਉਡਿ ਨ ਜਾਹੀ ਸਿਧ ਨ ਹੋਹਿ ॥

ud na jaahee siDh na hohi.

Hawatimizi hali ya juu zaidi ya kiroho, wala hawakuwi stadi katika shughuli za kidunia.

ਨਚਣੁ ਕੁਦਣੁ ਮਨ ਕਾ ਚਾਉ ॥

nachan kudan man kaa chaa-o.

Kudensi na kuruka kwao kwote ni kiburudisho cha akili tu.

ਨਾਨਕ ਜਿਨ੍ਹ ਮਨਿ ਭਉ ਤਿਨ੍ਹਾ ਮਨਿ ਭਾਉ ॥੨॥

naanak jinH man bha-o tinHaa man bhaa-o. ||2||

Ee Nanak, wao tu wana upendo wa Mungu akilini mwao, ambao wana hofu kwa heshima ya Mungu.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਨਾਉ ਤੇਰਾ ਨਿਰੰਕਾਰੁ ਹੈ ਨਾਇ ਲਇਐ ਨਰਕਿ ਨ ਜਾਈਐ ॥

naa-o tayraa nirankaar hai naa-ay la-i-ai narak na jaa-ee-ai.

Ee Mungu, Jina Lako ni Yule asiye na muundo, na iwapo tukukumbuke Wewe kwa ujitoaji wa upendo basi tunaepuka mateso yote.

ਜੀਉ ਪਿੰਡੁ ਸਭੁ ਤਿਸ ਦਾ ਦੇ ਖਾਜੈ ਆਖਿ ਗਵਾਈਐ ॥

jee-o pind sabh tis daa day khaajai aakh gavaa-ee-ai.

Roho na mwili yote ni Yake; kumuuliza Yeye atupe lishe ni bure.

ਜੇ ਲੋੜਹਿ ਚੰਗਾ ਆਪਣਾ ਕਰਿ ਪੁੰਨਹੁ ਨੀਚੁ ਸਦਾਈਐ ॥

jay lorheh changa aapnaa kar punnhu neech sadaa-ee-ai.

Iwapo unatamani maslahi yako, basi tenda vitendo vyema na ujihisi mnyenyekevu.

ਜੇ ਜਰਵਾਣਾ ਪਰਹਰੈ ਜਰੁ ਵੇਸ ਕਰੇਦੀ ਆਈਐ ॥

jay jarvaanaa parharai jar vays karaydee aa-ee-ai.

Hata iwapo mtu mwenye nguvu ajaribu kusukuma alama za uzee, bado uzee unakuja ukijificha kwa njia tofauti.

ਕੋ ਰਹੈ ਨ ਭਰੀਐ ਪਾਈਐ ॥੫॥

ko rahai na bharee-ai paa-ee-ai. ||5||

Hakuna anayeweza kusalia duniani humu wakati pumzi alizoagiziwa mapema zimekwisha.

ਸਲੋਕ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Shalok, na Guru wa Kwanza:

ਮੁਸਲਮਾਨਾ ਸਿਫਤਿ ਸਰੀਅਤਿ ਪੜਿ ਪੜਿ ਕਰਹਿ ਬੀਚਾਰੁ ॥

musalmaanaa sifat saree-at parh parh karahi beechaar.

Waislamu wanasifu sharia ya Kiislamu; wanasoma na kuitafakari.

ਬੰਦੇ ਸੇ ਜਿ ਪਵਹਿ ਵਿਚਿ ਬੰਦੀ ਵੇਖਣ ਕਉ ਦੀਦਾਰੁ ॥

banday say je paveh vich bandee vaykhan ka-o deedaar.

Kulingana nao, watumishi wa Mungu ni wale tu wanaofuata kwa makini sharia ya Kislamu ili kuona Mwono wa Mungu.

ਹਿੰਦੂ ਸਾਲਾਹੀ ਸਾਲਾਹਨਿ ਦਰਸਨਿ ਰੂਪਿ ਅਪਾਰੁ ॥

hindoo saalaahee saalaahan darsan roop apaar.

Wahindu wanamsifu Mungu anayestahili sifa, mzuri na asiye na kikomo kwa maandishi yao.

ਤੀਰਥਿ ਨਾਵਹਿ ਅਰਚਾ ਪੂਜਾ ਅਗਰ ਵਾਸੁ ਬਹਕਾਰੁ ॥

tirath naaveh archaa poojaa agar vaas behkaar.

Wanaoga katika ziara takatifu za hija, wakitoa matoleo ya maua, na kuchoma ubani mbele ya sanamu.

ਜੋਗੀ ਸੁੰਨਿ ਧਿਆਵਨ੍ਿ ਜੇਤੇ ਅਲਖ ਨਾਮੁ ਕਰਤਾਰੁ ॥

jogee sunn Dhi-aavni[H] jaytay alakh naam kartaar.

Mayogi wanatafakari kuhusu utupu wa kikosmiki na Jina la Muumba kama Alakh (asiyeweza kufahamika)

ਸੂਖਮ ਮੂਰਤਿ ਨਾਮੁ ਨਿਰੰਜਨ ਕਾਇਆ ਕਾ ਆਕਾਰੁ ॥

sookham moorat naam niranjan kaa-i-aa kaa aakaar.

Kulingana na Mayogi, Mungu hawezi kugusika, haathiriwi na utajiri na nguvu za kidunia na pia ulimwengu mzima ni kama muundo wa mwili Wake.

ਸਤੀਆ ਮਨਿ ਸੰਤੋਖੁ ਉਪਜੈ ਦੇਣੈ ਕੈ ਵੀਚਾਰਿ ॥

satee-aa man santokh upjai daynai kai veechaar.

Wazo la ukarimu huleta kuridhika akilini mwa watu wakarimu.

ਦੇ ਦੇ ਮੰਗਹਿ ਸਹਸਾ ਗੂਣਾ ਸੋਭ ਕਰੇ ਸੰਸਾਰੁ ॥

day day mangeh sahsaa goonaa sobh karay sansaar.

Wanatoa hisani kwa nia za kibinafsi, kwa sababu wanaulizia Mungu awape mara elfu ya kile wanachotoa, na wanatarajia dunia itukuze kutoa kwao.

ਚੋਰਾ ਜਾਰਾ ਤੈ ਕੂੜਿਆਰਾ ਖਾਰਾਬਾ ਵੇਕਾਰ ॥

choraa jaaraa tai koorhi-aaraa khaaraabaa vaykaar.

Kwa upande mwingine, wezi, washerati, waongo, waovu na wabaya,

ਇਕਿ ਹੋਦਾ ਖਾਇ ਚਲਹਿ ਐਥਾਊ ਤਿਨਾ ਭਿ ਕਾਈ ਕਾਰ ॥

ik hodaa khaa-ay chaleh aithaa-oo tinaa bhe kaa-ee kaar.

Wanaondoka duniani mikono mitupu baada ya kutumia sifa za vitendo vyao vya awali kujihusisha katika vitendo vya dhambi. Ni kazi bure kiasi gani wanayoifanya?

ਜਲਿ ਥਲਿ ਜੀਆ ਪੁਰੀਆ ਲੋਆ ਆਕਾਰਾ ਆਕਾਰ ॥

jal thal jee-aa puree-aa lo-aa aakaaraa aakaar.

Katika dunia na galaksi tofauti, kuna aina nyingi sana ya viumbe wanaoishi majini na kwenye ardhi.

ਓਇ ਜਿ ਆਖਹਿ ਸੁ ਤੂੰਹੈ ਜਾਣਹਿ ਤਿਨਾ ਭਿ ਤੇਰੀ ਸਾਰ ॥

o-ay je aakhahi so too$^{N}$hai jaaneh tinaa bhe tayree saar.

Ee Mungu, ni Wewe tu unayejua wanachoulizia viumbe hao. Wanakutegemea Wewe kwa riziki yao.

ਨਾਨਕ ਭਗਤਾ ਭੁਖ ਸਾਲਾਹਣੁ ਸਚੁ ਨਾਮੁ ਆਧਾਰੁ ॥

naanak bhagtaa bhukh saalaahan sach naam aaDhaar.

Ee Nanak, watawa daima wana hamu ya kumsifu Mungu na Jina la milele ndilo tegemeo yao ya pekee.

ਸਦਾ ਅਨੰਦਿ ਰਹਹਿ ਦਿਨੁ ਰਾਤੀ ਗੁਣਵੰਤਿਆ ਪਾ ਛਾਰੁ ॥੧॥

sadaa anand raheh din raatee gunvanti-aa paa chhaar. ||1||

Daima wanaishi katika raha ya milele, nao ni wanyenyekevu mno kwa watu wema.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਮਿਟੀ ਮੁਸਲਮਾਨ ਕੀ ਪੇੜੈ ਪਈ ਕੁਮ੍ਹਿਆਰ ॥

mitee musalmaan kee payrhai pa-ee kum$^{H}$i-aar.

Mabaki ya Mwislamu, mwishowe yanakuwa kama udongo kwenye gurudumu la mfinyanzi.

ਘੜਿ ਭਾਂਡੇ ਇਟਾ ਕੀਆ ਜਲਦੀ ਕਰੇ ਪੁਕਾਰ ॥

gharh bhaa[N]day itaa kee-aa jaldee karay pukaar.

Vyungu na matofali yanatengenezwa kutoka kwake, na hulia unapochomeka katika tanuri.

ਜਲਿ ਜਲਿ ਰੋਵੈ ਬਪੁੜੀ ਝੜਿ ਝੜਿ ਪਵਹਿ ਅੰਗਿਆਰ ॥

jal jal rovai bapurhee jharh jharh paveh angi-aar.

Unapoungua kwenye tanuri, udongo huu (mabaki ya mwislamu) hulia kana kwamba unachomeka jehanamuni.

ਨਾਨਕ ਜਿਨਿ ਕਰਤੈ ਕਾਰਣੁ ਕੀਆ ਸੋ ਜਾਣੈ ਕਰਤਾਰੁ ॥੨॥

naanak jin kartai kaaran kee-aa so jaanai kartaar. ||2||

Ee Nanak, Muumba aliyefanya uumbaji; peke yake ajua nani anayeenda mbinguni au jehanamu. (kuenda jehanamu au mbinguni hakutegemei mbinu ya kuondoa maiti).

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਬਿਨੁ ਸਤਿਗੁਰ ਕਿਨੈ ਨ ਪਾਇਓ ਬਿਨੁ ਸਤਿਗੁਰ ਕਿਨੈ ਨ ਪਾਇਆ ॥

bin satgur kinai na paa-i-o bin satgur kinai na paa-i-aa.

Pasipo kufuata mafundisho ya Guru wa Kweli, hakuna mtu aliyewahi kumgundua Mungu, ndio bila kufuata mafundisho ya Guru wa Kweli, hakuna mtu aliyewahi kumgundua Mungu.

ਸਤਿਗੁਰ ਵਿਚਿ ਆਪੁ ਰਖਿਓਨੁ ਕਰਿ ਪਰਗਟੁ ਆਖਿ ਸੁਣਾਇਆ ॥

satgur vich aap rakhi-on kar pargat aakh sunaa-i-aa.

Yeye amejithamini Mwenyewe katika Guru wa Kweli; akijidhihirisha Mwenyewe, Yeye hutangaza hili kwa uwazi.

ਸਤਿਗੁਰ ਮਿਲਿਐ ਸਦਾ ਮੁਕਤੁ ਹੈ ਜਿਨਿ ਵਿਚਹੁ ਮੋਹੁ ਚੁਕਾਇਆ ॥

satgur mili-ai sadaa mukat hai jin vichahu moh chukaa-i-aa.

Anapokutana na Guru wa Kweli, mtu, anayekana kiambatisho kwa utajiri na nguvu ya kidunia anakombolewa milele.

ਉਤਮੁ ਏਹੁ ਬੀਚਾਰੁ ਹੈ ਜਿਨਿ ਸਚੇ ਸਿਉ ਚਿਤੁ ਲਾਇਆ ॥ ਜਗਜੀਵਨੁ ਦਾਤਾ ਪਾਇਆ ॥੬॥

utam ayhu beechaar hai jin sachay sio chit laaiye. jagjeevan data paa-i-aa. ||6||

Tukufu zaidi ni wazo hilo, kwamba yule aliyepatanisha akili yake kwa Mungu, amemgundua Yeye, Mpaji wa uhai kwa dunia.

ਸਲੋਕ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਹਉ ਵਿਚਿ ਆਇਆ ਹਉ ਵਿਚਿ ਗਇਆ ॥

ha-o vich aa-i-aa ha-o vich ga-i-aa.

Katika ubinafsi (hali ambayo mtu anajifikiria kuwa ametengana na Mungu) mtu anakuja duniani, na katika ubinafsi yeye anaondoka duniani.

ਹਉ ਵਿਚਿ ਜੰਮਿਆ ਹਉ ਵਿਚਿ ਮੁਆ ॥

ha-o vich jammi-aa ha-o vich mu-aa.

Katika ubinafsi mtu huzaliwa, na katika ubinafsi hufariki.

ਹਉ ਵਿਚਿ ਦਿਤਾ ਹਉ ਵਿਚਿ ਲਇਆ ॥

ha-o vich ditaa ha-o vich la-i-aa.

Ili kudumisha ubinafsi (utambulisho tofauti), mtu anatoa na kukubali hisani.

ਹਉ ਵਿਚਿ ਖਟਿਆ ਹਉ ਵਿਚਿ ਗਇਆ ॥

ha-o vich khati-aa ha-o vich ga-i-aa.

Katika ubinafsi mtu hupata, na katika ubinafsi mtu hupoteza.

ਹਉ ਵਿਚਿ ਸਚਿਆਰੁ ਕੂੜਿਆਰੁ ॥

ha-o vich sachiaar koorhi-aar.

Katika ubinafsi mtu huwa wa kweli au wa uongo.

ਹਉ ਵਿਚਿ ਪਾਪ ਪੁੰਨ ਵੀਚਾਰੁ ॥

ha-o vich paap punn veechaar.

Katika ubinafsi mtu huwaza kwa makini kuhusu vitendo vya dhambi na vizuri.

ਹਉ ਵਿਚਿ ਨਰਕਿ ਸੁਰਗਿ ਅਵਤਾਰੁ ॥

ha-o vich narak surag avtaar.

Ni kwa ajili ya ubinafsi kwamba wakati mwingine mtu ana starehe zote na wakati mwingine anateseka kwa maumivu.

ਹਉ ਵਿਚਿ ਹਸੈ ਹਉ ਵਿਚਿ ਰੋਵੈ ॥

ha-o vich hasai ha-o vich rovai.

Katika ubinafsi mtu hufurahi, na katika ubinafsi mtu analia.

ਹਉ ਵਿਚਿ ਭਰੀਐ ਹਉ ਵਿਚਿ ਧੋਵੈ ॥

ha-o vich bharee-ai ha-o vich Dhovai.

Katika ubinafsi wakati mwingine akili ya mtu imejawa na uchafu wa maovu, na wakati mwingine mtu anafanya jitihada katika ubinafsi za kusafisha uchafu huu.

ਹਉ ਵਿਚਿ ਜਾਤੀ ਜਿਨਸੀ ਖੋਵੈ ॥

ha-o vich jaatee jinsee khovai.

Katika ubinafsi wakati mwingine mtu hupoteza hadhi na cheo cha kijamii.

ਹਉ ਵਿਚਿ ਮੂਰਖੁ ਹਉ ਵਿਚਿ ਸਿਆਣਾ ॥

ha-o vich moorakh ha-o vich si-aanaa.

Katika ubinafsi, wakati mwingine mtu anatenda kwa kiburi, na wakati mwingine anatenda kama mwenye busara.

ਮੋਖ ਮੁਕਤਿ ਕੀ ਸਾਰ ਨ ਜਾਣਾ ॥

mokh mukat kee saar na jaanaa.

Yeye hajui thamani ya wokovu au ukombozi.

ਹਉ ਵਿਚਿ ਮਾਇਆ ਹਉ ਵਿਚਿ ਛਾਇਆ ॥

ha-o vich maa-i-aa ha-o vich chhaa-i-aa.

Kwa kuwa katika ubinafsi mtu anajihusisha katika upendo wa utajiri na nguvu ya kidunia, au anasalia katika giza ya ujinga.

ਹਉਮੈ ਕਰਿ ਕਰਿ ਜੰਤ ਉਪਾਇਆ ॥

ha-umai kar kar jant upaa-i-aa.

Akiishi katika ubinafsi, binadamu anazaliwa tena na tena.

ਹਉਮੈ ਬੂਝੈ ਤਾ ਦਰੁ ਸੂਝੈ ॥

ha-umai boojhai taa dar soojhai.

Mtu anapoelewa ubinafsi, basi huijua njia inayoelekea kwa mahakama ya Mungu.

ਗਿਆਨ ਵਿਹੂਣਾ ਕਥਿ ਕਥਿ ਲੂਝੈ ॥

gi-aan vihoonaa kath kath loojhai.

Bila hekima ya kiroho, mtu huzidi kuteseka katika mazungumzo bure na mabishano.

ਨਾਨਕ ਹੁਕਮੀ ਲਿਖੀਐ ਲੇਖੁ ॥

naanak hukmee likee-ai laykh.

Ee Nanak, ni kwa Amri ya Mungu ambapo hatima ya mtu inaandikwa.

ਜੇਹਾ ਵੇਖਹਿ ਤੇਹਾ ਵੇਖੁ ॥੧॥

jayhaa vaykheh tayhaa vaykh. ||1||

Kama mtu anavyoona (kufikiria) wengine, baada ya muda mfupi mtu anasitawisha tabia kama yao.

ਮਹਲਾ ੨ ॥

mehlaa 2.

Salok, Guru wa Pili:

ਹਉਮੈ ਏਹਾ ਜਾਤਿ ਹੈ ਹਉਮੈ ਕਰਮ ਕਮਾਹਿ ॥

ha-umai ayhaa jaat hai ha-umai karam kamaahi.

Hii ndiyo hali ya ubinafsi, kwamba watu wanaendelea kutenda vitendo vyao kwa ubinafsi.

ਹਉਮੈ ਏਈ ਬੰਧਨਾ ਫਿਰਿ ਫਿਰਿ ਜੋਨੀ ਪਾਹਿ ॥

ha-umai ay-ee banDhnaa fir fir jonee paahi.

Huu ndio utumwa wa ubinafsi, kwamba wanazaliwa tena na tena.

ਹਉਮੈ ਕਿਥਹੁ ਊਪਜੈ ਕਿਤੁ ਸੰਜਮਿ ਇਹ ਜਾਇ ॥

ha-umai kithhu oopjai kit sanjam ih jaa-ay.

Ubinafsi hutoka wapi? Unawezajekuondolewa?

ਹਉਮੈ ਏਹੋ ਹੁਕਮੁ ਹੈ ਪਇਐ ਕਿਰਤਿ ਫਿਰਾਹਿ ॥

ha-umai ayho hukam hai pa-i-ai kirat firaahi.

Ubinafsi huu upo kwa Amri ya Mungu; watu wanazurura kulingana na vitendo vyao vya awali.

ਹਉਮੈ ਦੀਰਘ ਰੋਗੁ ਹੈ ਦਾਰੂ ਭੀ ਇਸੁ ਮਾਹਿ ॥

ha-umai deeragh rog hai daaroo bhee is maahi.

Ubinafsi ni ugonjwa sugu, lakini tiba yake pia imo ndani yake.

ਕਿਰਪਾ ਕਰੇ ਜੇ ਆਪਣੀ ਤਾ ਗੁਰ ਕਾ ਸਬਦੁ ਕਮਾਹਿ ॥

kirpaa karay jay aapnee taa gur kaa sabad kamaahi.

Mungu anapojalia Neema Yake, mtu anatenda kulingana na Mafundisho ya Guru.

ਨਾਨਕੁ ਕਹੈ ਸੁਣਹੁ ਜਨਹੁ ਇਤੁ ਸੰਜਮਿ ਦੁਖ ਜਾਹਿ ॥੨॥

naanak kahai sunhu janhu it sanjam dukh jaahi. ||2||

Nanak anasema, sikizeni, enyi watu; kwa njia hii (kwa kutafakari kuhusu Jina la Mungu), huzuni zinazotokana na ugonjwa wa ubinafsi zinaondoka.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਸੇਵ ਕੀਤੀ ਸੰਤੋਖੀਈ ਜਿਨ੍ਹੀ ਸਚੋ ਸਚੁ ਧਿਆਇਆ ॥

sayv keetee santokhee-ee$^N$ jin$^H$ee sacho sach Dhi-aa-i-aa.

Watu hao tu waliotosheka, wanaotafakari kuhusu (Mungu) wa Milele kwa upendo na ujitoaji, kwa kweli wanamtumikia Yeye.

ਓਨ੍ਹੀ ਮੰਦੈ ਪੈਰੁ ਨ ਰਖਿਓ ਕਰਿ ਸੁਕ੍ਰਿਤੁ ਧਰਮੁ ਕਮਾਇਆ ॥

on$^H$ee mandai pair na rakhi-o kar sukarit Dharam kamaa-i-aa.

Wao hawayakaribii maovu, lakini hu tenda mema na kuishi kwa uadilifu.

ਓਨ੍ਹੀ ਦੁਨੀਆ ਤੋੜੇ ਬੰਧਨਾ ਅੰਨੁ ਪਾਣੀ ਥੋੜਾ ਖਾਇਆ ॥

on$^H$ee dunee-aa torhay banDhnaa ann paanee thorhaa khaa-i-aa.

Wamejiweka huru kutoka kwa vifungo vya kidunia, na wanakula chakula na maji kwa kiasi (kinachotosha kuishi).

ਤੂੰ ਬਖਸੀਸੀ ਅਗਲਾ ਨਿਤ ਦੇਵਹਿ ਚੜਹਿ ਸਵਾਇਆ ॥

too$^{N}$ bakhseesee aglaa nit dayveh charheh savaa-i-aa.

Ee Mungu, Wewe ndiye mfadhili mkuu zaidi, Wewe hutoa kila mara, zaidi na zaidi.

ਵਡਿਆਈ ਵਡਾ ਪਾਇਆ ॥੭॥

vadi-aa-ee vadaa paa-i-aa. ||7||

Kwa kumtukuza Yeye, wanamgundua Mungu Mkuu.

ਸਲੋਕ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਪੁਰਖਾਂ ਬਿਰਖਾਂ ਤੀਰਥਾਂ ਤਟਾਂ ਮੇਘਾਂ ਖੇਤਾਂਹ ॥

purkhaa$^{N}$ birkhaa$^{N}$ teerthaa$^{N}$ tataa$^{N}$ mayghaa$^{N}$ khaytaa$^{N}$h.

Ni Mungu peke yake anayejua hesabu na hali ya wanadamu wote, miti, ziara takatifu za hija, ukingo wa mito mitakatifu, mawingu na nyanja.

ਦੀਪਾਂ ਲੋਆਂ ਮੰਡਲਾਂ ਖੰਡਾਂ ਵਰਭੰਡਾਂਹ ॥

deepaa$^{N}$ lo-aa$^{N}$ mandlaa$^{N}$ khandaa$^{N}$ varbhandaa$^{N}$h.

Ni Yeye tu anayejua visiwa, mabara, dunia na mifumo ya jua ambayo ipo ulimwenguni.

ਅੰਡਜ ਜੇਰਜ ਉਤਭੁਜਾਂ ਖਾਣੀ ਸੇਤਜਾਂਹ ॥

andaj jayraj ut-bhujaa$^{N}$ khaanee saytjaa$^{N}$h.

Ni Yeye tu anayejua kuhusu viumbe wanaozaliwa kwa vyanzo vinne vya uumbaji kama vile mayai, chupa cha uzazi, ardhi na jasho.

ਸੋ ਮਿਤਿ ਜਾਣੈ ਨਾਨਕਾ ਸਰਾਂ ਮੇਰਾਂ ਜੰਤਾਹ ॥

so mit jaanai naankaa saraa[N] mayraa[N] jantaah.

Ee Nanak, ni Mungu tu anayejua kuhusu idadi ya bahari, milima na hali ya viumbe wanaoishi ndani mwao.

ਨਾਨਕ ਜੰਤ ਉਪਾਇ ਕੈ ਸੰਮਾਲੇ ਸਭਨਾਹ ॥

naanak jant upaa-ay kai sammaalay sabhnaah.

Ee Nanak, akiwa muumbaji wa viumbe hao, Yeye anawathamini wote.

ਜਿਨਿ ਕਰਤੈ ਕਰਣਾ ਕੀਆ ਚਿੰਤਾ ਭਿ ਕਰਣੀ ਤਾਹ ॥

jin kartai karnaa kee-aa chintaa bhe karnee taah.

Muumba aliyeumba uumbaji, anauchunga vilevile.

ਸੋ ਕਰਤਾ ਚਿੰਤਾ ਕਰੇ ਜਿਨਿ ਉਪਾਇਆ ਜਗੁ ॥

so kartaa chintaa karay jin upaa-i-aa jag.

Ndio, Muumba huyo aliyeumba dunia, anauchunga vilevile.

ਤਿਸੁ ਜੋਹਾਰੀ ਸੁਅਸਤਿ ਤਿਸੁ ਤਿਸੁ ਦੀਬਾਣੁ ਅਭਗੁ ॥

tis johaaree su-asat tis tis deebaan abhag.

Mbele Yake nainamisha kichwa na kutoa heshima yangu, ambaye mfumo wake wa tegemeo ni wa milele.

ਨਾਨਕ ਸਚੇ ਨਾਮ ਬਿਨੁ ਕਿਆ ਟਿਕਾ ਕਿਆ ਤਗੁ ॥੧॥

naanak sachay naam bin ki-aa tikaa ki-aa tag. ||1||

Ee Nanak, bila kutafakari kwa Jina Lake, ishara zote zingine za nje za kidini kama vile Janeu (uzi mtakatifu) na Tikka (nukta kwenye paji) hazina maana.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਲਖ ਨੇਕੀਆ ਚੰਗਿਆਈਆ ਲਖ ਪੁੰਨਾ ਪਰਵਾਣੁ ॥

lakh naykee-aa chang-aa-ee-aa lakh punnaa parvaan.

Mtu anaweza kutenda mamilioni ya vitendo vizuri na vyema na maelfu ya vitendo vya ukarimu ambavyo vinakubalika katika jamii.

ਲਖ ਤਪ ਉਪਰਿ ਤੀਰਥਾਂ ਸਹਜ ਜੋਗ ਬੇਬਾਣ ॥

lakh tap upar teerthaa[N] sahj jog baybaan.

Mtu anaweza kufanya mamilioni ya toba katika ziara takatifu, na kuenda nyikani kufanya yoga katika hali ya utulivu.

ਲਖ ਸੂਰਤਣ ਸੰਗਰਾਮ ਰਣ ਮਹਿ ਛੁਟਹਿ ਪਰਾਣ ॥

lakh soortan sangraam ran meh chhuteh paraan.

Mtu anaweza kuenda kwenye uwanja wa vita na kuonyesha mamilioni ya vitendo vya ujasiri, na hata kupoteza maisha yake hapo.

ਲਖ ਸੁਰਤੀ ਲਖ ਗਿਆਨ ਧਿਆਨ ਪੜੀਅਹਿ ਪਾਠ ਪੁਰਾਣ ॥

lakh surtee lakh gi-aan Dhi-aan parhee-ah paath puraan.

Mtu anaweza kupata uelewa mwingi mtakatifu na hekima takatifu kwa kufanya utafakari na kusoma Vedas na Puranas,

ਜਿਨਿ ਕਰਤੈ ਕਰਣਾ ਕੀਆ ਲਿਖਿਆ ਆਵਣ ਜਾਣੁ ॥

jin kartai karnaa kee-aa likhi-aa aavan jaan.

Muumba, Ambaye ameumba uumbaji huu na ameagizia mapema wakati wa kuzaliwa na kufa kwa mtu.

ਨਾਨਕ ਮਤੀ ਮਿਥਿਆ ਕਰਮੁ ਸਚਾ ਨੀਸਾਣੁ ॥੨॥

naanak matee mithi-aa karam sachaa neesaan. ||2||

Ee Nanak, hila hizi zote za ujanja ni za uongo na ni bure. Neema Yake tu ni muhuri au alama ya kukubalika katika mahakama Yake.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਸਚਾ ਸਾਹਿਬੁ ਏਕੁ ਤੂੰ ਜਿਨਿ ਸਚੋ ਸਚੁ ਵਰਤਾਇਆ ॥

sachaa saahib ayk tooN jin sacho sach vartaa-i-aa.

Ee Mungu, Wewe ndiwe Bwana wa Kweli pekee, ambaye ametoa Ukweli (uadilifu) kila mahali.

ਜਿਸੁ ਤੂੰ ਦੇਹਿ ਤਿਸੁ ਮਿਲੈ ਸਚੁ ਤਾ ਤਿਨ੍ਹੀ ਸਚੁ ਕਮਾਇਆ ॥

jis tooN deh tis milai sach taa tinHee sach kamaa-i-aa.

Yeye peke yake hupokea Ukweli, ambaye Wewe unampa; kisha, yeye anatenda Ukweli.

ਸਤਿਗੁਰਿ ਮਿਲਿਐ ਸਚੁ ਪਾਇਆ ਜਿਨ੍ਹ ਕੈ ਹਿਰਦੈ ਸਚੁ ਵਸਾਇਆ ॥

satgur mili-ai sach paa-i-aa jinH kai hirdai sach vasaa-i-aa.

Ni kwa kukutana na kufuata mafundisho ya Guru wa Kweli ambapo watu wamegundua Ukweli. Guru anathamini Ukweli moyoni mwao.

ਮੂਰਖ ਸਚੁ ਨ ਜਾਣਨ੍ਹੀ ਮਨਮੁਖੀ ਜਨਮੁ ਗਵਾਇਆ ॥

moorakh sach na jaananHee manmukhee janam gavaa-i-aa.

Watu wapumbavu wenye hiari binafsi hawajui, Ukweli ni nini na wanaharibu maisha yao bure.

ਵਿਚਿ ਦੁਨੀਆ ਕਾਹੇ ਆਇਆ ॥੮॥

vich dunee-aa kaahay aa-i-aa. ||8||

Kwa nini wamekuja hata duniani humu?

ਸਲੋਕੁ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਪੜਿ ਪੜਿ ਗਡੀ ਲਦੀਅਹਿ ਪੜਿ ਪੜਿ ਭਰੀਅਹਿ ਸਾਥ ॥

parh parh gadee ladee-ah parh parh bharee-ah saath.

Hata tukisoma na kujifunza vitabu vingi na baada ya kusoma tutengeneza marundo ya vitabu.

ਪੜਿ ਪੜਿ ਬੇੜੀ ਪਾਈਐ ਪੜਿ ਪੜਿ ਗਡੀਅਹਿ ਖਾਤ ॥

parh parh bayrhee paa-ee-ai parh parh gadee-ah khaat.

Tukisoma vitabu vingi mno kwamba mashua au mashimo mengi yanaweza kujazwa navyo.

ਪੜੀਅਹਿ ਜੇਤੇ ਬਰਸ ਬਰਸ ਪੜੀਅਹਿ ਜੇਤੇ ਮਾਸ ॥

parhee-ah jaytay baras baras parhee-ah jaytay maas.

Tunaweza kuvisoma mwaka baada ya mwaka; tunaweza kuvisoma kwa miezi mingi kama ilivyo katika mwaka.

ਪੜੀਐ ਜੇਤੀ ਆਰਜਾ ਪੜੀਅਹਿ ਜੇਤੇ ਸਾਸ ॥

parhee-ai jaytee aarjaa parhee-ah jaytay saas.

Tunaweza kuvisoma maisha yetu yote; tunaweza kuvisoma kwa kila pumzi.

ਨਾਨਕ ਲੇਖੈ ਇਕ ਗਲ ਹੋਰੁ ਹਉਮੈ ਝਖਣਾ ਝਾਖ ॥੧॥

naanak laykhai ik gal hor ha-umai jhakh-naa jhaakh. ||1||

Ee Nanak, kitu kimoja tu, ambacho kinahesabika katika mahakama yake ni kuimba sifa Zake na kutafakari kuhusu Jina Lake. Vyote vingine ni kama kuzurura katika ubinafsi wa mtu.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਲਿਖਿ ਲਿਖਿ ਪੜਿਆ ॥ਤੇਤਾ ਕੜਿਆ ॥

likh likh parhi-aa. taytaa karhi-aa.

Mtu anavyozidi kuandika na kusoma, ndivyo anavyozidi kuwa mwenye ubinafsi na kiburi.

ਬਹੁ ਤੀਰਥ ਭਵਿਆ ॥ਤੇਤੋ ਲਵਿਆ ॥

baho tirath bhavi-aa. tayto lavi-aa.

Mtu anavyozidi kuzurura katika ziara takatifu za hija, ndivyo anavyozidi kuzungumza bure (kama kunguru)

ਬਹੁ ਭੇਖ ਕੀਆ ਦੇਹੀ ਦੁਖੁ ਦੀਆ ॥

baho bhaykh kee-aa dayhee dukh dee-aa.

Mtu anavyozidi kuvaa joho la kidini, ndivyo anavyozidi kujifadhaisha.

ਸਹੁ ਵੇ ਜੀਆ ਅਪਣਾ ਕੀਆ ॥

saho vay jee-aa apnaa kee-aa.

Ee rafiki yangu, unapaswa kustahimili matokeo ya vitendo vyako mwenyewe.

ਅੰਨੁ ਨ ਖਾਇਆ ਸਾਦੁ ਗਵਾਇਆ ॥

ann na khaa-i-aa saad gavaa-i-aa.

Kwa kukosa kula chakula, mtu hajapata sifa zozote za kiroho, yeye amepoteza tu fursa ya kufurahia kiburudisho chake.

ਬਹੁ ਦੁਖੁ ਪਾਇਆ ਦੂਜਾ ਭਾਇਆ ॥

baho dukh paa-i-aa doojaa bhaa-i-aa.

Kwa ajili ya upendo wake wa uwili (matendo balina kumpenda na kumkumbuka Mungu), yeye ameteseka Uchungu mwingi.

ਬਸਤ੍ਰ ਨ ਪਹਿਰੈ ॥ ਅਹਿਨਿਸਿ ਕਹਰੈ ॥

bastar na pahirai. ahinis kahrai.

Yule asiyevaa mavazi yoyote, anateseka usiku na mchana kwa kutiisha mwili

wake kwa makali ya hali ya anga.

ਮੋਨਿ ਵਿਗੂਤਾ ॥ ਕਿਉ ਜਾਗੈ ਗੁਰ ਬਿਨੁ ਸੂਤਾ ॥

mon vigootaa. ki-o jaagai gur bin sootaa.

Akizama katika kimya, mtu amepotoka (kutoka njia ya uadilifu). Anawezaje kuamshwa kutoka kwa usingizi wa ujinga bila mafundisho ya Guru?

ਪਗ ਉਪੇਤਾਣਾ ॥ ਅਪਣਾ ਕੀਆ ਕਮਾਣਾ ॥

pag upaytaanaa. apnaa kee-aa kamaanaa.

Yule anayetembea miguumitupu, anateseka kutokana na vitendo vyake mwenyewe kwa kuumiza miguu yake.

ਅਲੁ ਮਲੁ ਖਾਈ ਸਿਰਿ ਛਾਈ ਪਾਈ ॥

al mal khaa-ee sir chhaa-ee paa-ee.

Yule anayekula mabaki machafu na kurusha majivu kichwani pake,

ਮੂਰਖਿ ਅੰਧੈ ਪਤਿ ਗਵਾਈ ॥

moorakh anDhai pat gavaa-ee.

Mtu huyo kipofu mpumbavu (mjinga) amepoteza staha yake.

ਵਿਣੁ ਨਾਵੈ ਕਿਛੁ ਥਾਇ ਨ ਪਾਈ ॥

vin naavai kichh thaa-ay na paa-ee.

Bila kutafakari kuhusu Jina la Mungu, hakuna kilichoidhinishwa katika mahakama Yake.

ਰਹੈ ਬੇਬਾਣੀ ਮੜੀ ਮਸਾਣੀ ॥

rahai baybaanee marhee masaanee.

Mtu anaweza kuishi nyikani, makaburini au kwenye nyanja za kuchomea maiti,

ਅੰਧੁ ਨ ਜਾਣੈ ਫਿਰਿ ਪਛੁਤਾਣੀ ॥

anDh na jaanai fir pachhutaanee.

Kipofu wa kiroho kama huyo hajui njia ya kweli ya kumgundua Mungu, yeye hujuta na kutubu mwishowe.

**ਸਤਿਗੁਰੁ ਭੇਟੇ ਸੋ ਸੁਖੁ ਪਾਏ ॥**

satgur bhaytay so sukh paa-ay.

Ni Yeye tu, anayekutana na Guru wa Kweli, ambaye hufurahia amani.

**ਹਰਿ ਕਾ ਨਾਮੁ ਮੰਨਿ ਵਸਾਏ ॥**

har kaa naam man vasaa-ay.

Maana yeye analithamini Jina la Mungu akilini mwake.

**ਨਾਨਕ ਨਦਰਿ ਕਰੇ ਸੋ ਪਾਏ ॥**

naanak nadar karay so paa-ay.

Ee Nanak, ni yeye tu ambaye Mungu anatawazia neema Yake, anakutana na Guru.

**ਆਸ ਅੰਦੇਸੇ ਤੇ ਨਿਹਕੇਵਲੁ ਹਉਮੈ ਸਬਦਿ ਜਲਾਏ ॥੨॥**

aas andaysay tay nihkayval ha-umai sabad jalaa-ay. ||2||

Kisha kwa kutoathiriwa na aina yoyote ya matumaini na wasiwasi, na kufuata neno la Guru, yeye anateketeza ubinafsi wake.

**ਪਉੜੀ ॥**

pa-orhee.

Pauree:

**ਭਗਤ ਤੇਰੈ ਮਨਿ ਭਾਵਦੇ ਦਰਿ ਸੋਹਨਿ ਕੀਰਤਿ ਗਾਵਦੇ ॥**

bhagat tayrai man bhaavday dar sohan keerat gaavday.

Ee Mungu, watawa Wako wanapendeza akilini mwako. Wanaonekana wazuri mlangoni Pako, wakiimba Sifa Zako.

ਨਾਨਕ ਕਰਮਾ ਬਾਹਰੇ ਦਰਿ ਢੋਅ ਨ ਲਹਨੑੀ ਧਾਵਦੇ ॥

naanak karmaa baahray dar dho-a na lehn[H]ee Dhaavday.

Ee Nanak, wale ambao wamenyimwa Neema ya Mungu, hawapati kificho katika Mahakama yake na wanaendelea kuzurura bila mwelekeo.

ਇਕਿ ਮੂਲੁ ਨ ਬੁਝਨਿੑ ਆਪਣਾ ਅਣਹੋਦਾ ਆਪੁ ਗਣਾਇਦੇ ॥

ik mool na bujhni[H] aapnaa anhodaa aap ganaa-iday.

Kuna wengine wasioelewa mizizi yao, na pasipo sifa yoyote ya kiroho, wanajiita wakuu.

ਹਉ ਢਾਢੀ ਕਾ ਨੀਚ ਜਾਤਿ ਹੋਰਿ ਉਤਮ ਜਾਤਿ ਸਦਾਇਦੇ ॥

ha-o dhaadhee kaa neech jaat hor utam jaat sadaa-iday.

Ee Mungu, wengine wanapojidai kuwa wa hadhi ya juu ya kijamii, mimi ni kijakazi tu wa hadhi ya chini ya kijamii.

ਤਿਨੑ ਮੰਗਾ ਜਿ ਤੁਝੈ ਧਿਆਇਦੇ ॥੯॥

tin[H] mangaa je tujhai Dhi-aa-iday. ||9||

Natafuta tu kuandamana na wale wanaotafakari kukuhusu Wewe.

ਸਲੋਕੁ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਕੂੜੁ ਰਾਜਾ ਕੂੜੁ ਪਰਜਾ ਕੂੜੁ ਸਭੁ ਸੰਸਾਰੁ ॥

koorh raajaa koorh parjaa koorh sabh sansaar.

Dunia hii yote ni njozi kama tendo la mfanya mazingaombwe. Katika dunia hii isiyo ya kweli, mwongo (asiyedumu) ni mfalme na waongo ni raia watumishi.

ਕੂੜੁ ਮੰਡਪ ਕੂੜੁ ਮਾੜੀ ਕੂੜੁ ਬੈਸਣਹਾਰੁ ॥

koorh mandap koorh maarhee koorh baisanhaar.

Maongo ni makasri na majumba na hawadumu wale wanaoishi ndani yao.

ਕੂੜੁ ਸੁਇਨਾ ਕੂੜੁ ਰੁਪਾ ਕੂੜੁ ਪੈਨ੍ਣਹਾਰੁ ॥

koorh su-inaa koorh rupaa koorh painHanhaar.

Ya uongo ni mapambo ya dhahabu na fedha, na waongo ni wale wanaoyavaa.

ਕੂੜੁ ਕਾਇਆ ਕੂੜੁ ਕਪੜੁ ਕੂੜੁ ਰੂਪੁ ਅਪਾਰੁ ॥

koorh kaa-i-aa koorh kaparh koorh roop apaar.

Wa uongo ni mwili, maongo ni mavazi na uzuri uliokithiri ni kama njozi.

ਕੂੜੁ ਮੀਆ ਕੂੜੁ ਬੀਬੀ ਖਪਿ ਹੋਏ ਖਾਰੁ ॥

koorh mee-aa koorh beebee khap ho-ay khaar.

Uhusiano kati ya mume na mke ni wa muda mfupi mno na wanaangamia katika mizozano ya uongo.

ਕੂੜਿ ਕੂੜੈ ਨੇਹੁ ਲਗਾ ਵਿਸਰਿਆ ਕਰਤਾਰੁ ॥

koorh koorhai nayhu lagaa visri-aa kartaar.

Walio waongo wanapenda udanganyifu, na wanasahau Muumba wao.

ਕਿਸੁ ਨਾਲਿ ਕੀਚੈ ਦੋਸਤੀ ਸਭੁ ਜਗੁ ਚਲਣਹਾਰੁ ॥

kis naal keechai dostee sabh jag chalanhaar.

Tunafaa kuwa na urafiki na nani, wakati dunia nzima ni ya mpito?

ਕੂੜੁ ਮਿਠਾ ਕੂੜੁ ਮਾਖਿਉ ਕੂੜੁ ਡੋਬੇ ਪੂਰੁ ॥

koorh mithaa koorh maakhi-o koorh dobay poor.

Kwa binadamu dunia hii ya kinjozi inaonekana kuwa tamu kama asali na ndiposa njozi hii ya uongo inaangamiza halaiki za watu.

ਨਾਨਕੁ ਵਖਾਣੈ ਬੇਨਤੀ ਤੁਧੁ ਬਾਝੁ ਕੂੜੋ ਕੂੜੁ ॥੧॥

naanak vakhaanai bayntee tuDh baajh koorho koorh. ||1||

Ee Mungu, Nanak anatoa dua hili, kwamba pasipo Wewe, kila kitu ni cha uongo na ni kama njozi

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਸਚੁ ਤਾ ਪਰੁ ਜਾਣੀਐ ਜਾ ਰਿਦੈ ਸਚਾ ਹੋਇ ॥

sach taa par jaanee-ai jaa ridai sachaa ho-ay.

Mtu anajua Ukweli wakati tu Mungu anapoishi moyoni mwake.

ਕੂੜ ਕੀ ਮਲੁ ਉਤਰੈ ਤਨੁ ਕਰੇ ਹਛਾ ਧੋਇ ॥

koorh kee mal utrai tan karay hachhaa Dho-ay.

Uchafu wa udanganyifu unaondolewa na akili na mwili zinakombolewa kutoka maovuni.

ਸਚੁ ਤਾ ਪਰੁ ਜਾਣੀਐ ਜਾ ਸਚਿ ਧਰੇ ਪਿਆਰੁ॥

sach taa par jaanee-ai jaa sach Dharay pi-aar.

Mtu anakuja kujua ukweli kuhusu dunia wakati tu anapobeba upendo kwa Mungu.

ਨਾਉ ਸੁਣਿ ਮਨੁ ਰਹਸੀਐ ਤਾ ਪਾਏ ਮੋਖ ਦੁਆਰੁ ॥

naa-o sun man rehsee-ai taa paa-ay mokh du-aar.

Kwa kusikia Jina la Mungu, akili inapendezwa; kisha, mtu anapata uhuru kutoka kwa misongamano ya kidunia.

ਸਚੁ ਤਾ ਪਰੁ ਜਾਣੀਐ ਜਾ ਜੁਗਤਿ ਜਾਣੈ ਜੀਉ ॥

sach taa par jaanee-ai jaa jugat jaanai jee-o.

Mtu hujua Ukweli wakati tu yeye anajua njia ya kweli ya maisha.

ਧਰਤਿ ਕਾਇਆ ਸਾਧਿ ਕੈ ਵਿਚਿ ਦੇਇ ਕਰਤਾ ਬੀਉ ॥

Dharat kaa-i-aa saaDh kai vich day-ay kartaa bee-o.

Kwa kutayarisha mwili kama shamba, yeye hupanda Mbegu ya Jina la Mungu.

ਸਚੁ ਤਾ ਪਰੁ ਜਾਣੀਐ ਜਾ ਸਿਖ ਸਚੀ ਲੇਇ ॥

sach taa par jaanee-ai jaa sikh sachee lay-ay.

Mtu hufahamu Ukweli tu wakati yeye anapokea mafundisho ya kweli kutoka kwa Guru.

ਦਇਆ ਜਾਣੈ ਜੀਅ ਕੀ ਕਿਛੁ ਪੁੰਨੁ ਦਾਨੁ ਕਰੇਇ ॥

da-i-aa jaanai jee-a kee kichh punn daan karay-i.

Akionyesha huruma kwa viumbe wengine, na kufanya vitendo vya ukarimu na wema.

ਸਚੁ ਤਾਂ ਪਰੁ ਜਾਣੀਐ ਜਾ ਆਤਮ ਤੀਰਥਿ ਕਰੇ ਨਿਵਾਸੁ ॥

sach taa$^{N}$ par jaanee-ai jaa aatam tirath karay nivaas.

Mtu anafahamu ukweli wakati tu anaishi katika ziara takatifu ya nafsi.

ਸਤਿਗੁਰੂ ਨੋ ਪੁਛਿ ਕੈ ਬਹਿ ਰਹੈ ਕਰੇ ਨਿਵਾਸੁ ॥

satguroo no puchh kai bahi rahai karay nivaas.

Kwa kupata mafundisho kutoka kwa Guru wa Kweli, yeye anamakinikia nafsi yake ya ndani.

ਸਚੁ ਸਭਨਾ ਹੋਇ ਦਾਰੂ ਪਾਪ ਕਢੈ ਧੋਇ ॥

sach sabhnaa ho-ay daaroo paap kadhai Dho-ay.

Mungu Mwenyewe anakuwa tiba ya magonjwa yote; na kuondoa dhambi zote.

ਨਾਨਕੁ ਵਖਾਣੈ ਬੇਨਤੀ ਜਿਨ ਸਚੁ ਪਲੈ ਹੋਇ ॥੨॥

naanak vakhaanai bayntee jin sach palai ho-ay. ||2||

Nanak anatafuta kwa unyenyekevu wale ambao wana Ukweli (Mungu) ukiishi moyoni mwao.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਦਾਨੁ ਮਹਿੰਡਾ ਤਲੀ ਖਾਕੁ ਜੇ ਮਿਲੈ ਤ ਮਸਤਕਿ ਲਾਈਐ ॥

daan mahindaa talee khaak jay milai ta mastak laa-ee-ai.

Thawabu ninayoitafuta ni unyenyekevu; ningeipata, ningejifikiria kuwa mwenye bahati mno.

ਕੂੜਾ ਲਾਲਚੁ ਛਡੀਐ ਹੋਇ ਇਕ ਮਨਿ ਅਲਖੁ ਧਿਆਈਐ ॥

koorhaa laalach chhadee-ai ho-ay ik man alakh Dhi-aa-ee-ai.

Kana tamaa ya uongo, na umtafakari Mungu asiyefahamika kwa nia moja.

ਫਲੁ ਤੇਵੇਹੋ ਪਾਈਐ ਜੇਵੇਹੀ ਕਾਰ ਕਮਾਈਐ ॥

fal tayvayho paa-ee-ai jayvayhee kaar kamaa-ee-ai.

Kama vilivyo vitendo tunavyotenda, ndivyo zilivyo tuzo tunazopokea.

ਜੇ ਹੋਵੈ ਪੂਰਬਿ ਲਿਖਿਆ ਤਾ ਧੂੜਿ ਤਿਨ੍ਹਾ ਦੀ ਪਾਈਐ ॥

jay hovai poorab likhi-aa taa Dhoorh tin$^{H}$aa dee paa-ee-ai.

Iwapo imeagizwa hivyo tokea mwanzo, basi mtu anapata kutumikia Watakatifu kwa unyenyekevu.

ਮਤਿ ਥੋੜੀ ਸੇਵ ਗਵਾਈਐ ॥੧੦॥

mat thorhee sayv gavaa-ee-ai. ||10||

Kutokana na upungufu wetu wa hekima, tunakosa sifa za huduma isiyo na ubinafsi.

ਸਲੋਕੁ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਸਚਿ ਕਾਲੁ ਕੂੜੁ ਵਰਤਿਆ ਕਲਿ ਕਾਲਖ ਬੇਤਾਲ ॥

sach kaal koorh varti-aa kal kaalakh baytaal.

Kuishi kwa uadilifu kumekuwa nadra, udanganyifu unapenyeza kote na watu wanatenda kama mapepo kwa ajili ya dhambi na maovu ya Kalyug.

ਬੀਉ ਬੀਜਿ ਪਤਿ ਲੈ ਗਏ ਅਬ ਕਿਉ ਉਗਵੈ ਦਾਲਿ ॥

bee-o beej pat lai ga-ay ab ki-o ugvai daal.

Wale walioishi kwa uadilifu (waliopanda mbegu ya uadilifu akilini mwao) wameondoka kwa staha. Wale ambao akili yao imegawanywa kuwili, mbegu ya uadilifu inawezaje kukua akilini mwao?

ਜੇ ਇਕੁ ਹੋਇ ਤ ਉਗਵੈ ਰੁਤੀ ਹੂ ਰੁਤਿ ਹੋਇ ॥

jay ik ho-ay ta ugvai rutee hoo rut ho-ay.

Mbegu ya upendo kwa Mungu itamea iwapo akili haijagawanywa kuwili na kuna hali mwafaka kama vile hali ya anga baridi na tulivu ya asubuhi mapema.

ਨਾਨਕ ਪਾਹੈ ਬਾਹਰਾ ਕੋਰੈ ਰੰਗੁ ਨ ਸੋਇ ॥

naanak paahai baahraa korai rang na so-ay

Ee Nanak, kama vile bila matayarisho ya awali, nguo mbichi haipakwi rangi vizuri.

ਭੈ ਵਿਚਿ ਖੁੰਬਿ ਚੜਾਈਐ ਸਰਮੁ ਪਾਹੁ ਤਨਿ ਹੋਇ ॥

bhai vich khumb charhaa-ee-ai saram paahu tan ho-ay

Vivyo hivyo, ili kupenyeza akili katika upendo wa Mungu, matayarisho ya awali (ya akili ni) kusitawisha hofu ya Mungu kwa bidii.

ਨਾਨਕ ਭਗਤੀ ਜੇ ਰਪੈ ਕੂੜੈ ਸੋਇ ਨ ਕੋਇ ॥੧॥

naanak bhagtee jay rapai koorhai so-ay na ko-ay. ||1||

Ee Nanak, wakati kwa njia hii akili inapenyezwa na upendo na ujitoaji wa Mungu, basi hakuna wazo la udanganyifu linalotokea ndani mwake.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਲਬੁ ਪਾਪੁ ਦੁਇ ਰਾਜਾ ਮਹਤਾ ਕੂੜੁ ਹੋਆ ਸਿਕਦਾਰੁ ॥

lab paap du-ay raajaa mahtaa koorh ho-aa sikdaar.

(hali duniani ni yenye taabu, inaonekana kwamba) tamaa na dhambi pia imekuwa mfalme na msaidizi wake; na udanganyifu ndio mkurugenzi mkuu.

ਕਾਮੁ ਨੇਬੁ ਸਦਿ ਪੁਛੀਐ ਬਹਿ ਬਹਿ ਕਰੇ ਬੀਚਾਰੁ ॥

kaam nayb sad puchhee-ai bahi bahi karay beechaar.

Ukware ni kama mshauri mkuu, wanaulizia ushauri wake na kisha wakiketi pamoja wanajadiliana kuhusu njia tofauti za kuupumbaza umma.

ਅੰਧੀ ਰਯਤਿ ਗਿਆਨ ਵਿਹੂਣੀ ਭਾਹਿ ਭਰੇ ਮੁਰਦਾਰੁ ॥

anDhee rayat gi-aan vihoonee bhaahi bharay murdaar.

Watumishi wao ni wajinga kutokana na ukosefu wa maarifa, wamejawa na moto wa hamu za kidunia, na wamekufa kiroho.

ਗਿਆਨੀ ਨਚਹਿ ਵਾਜੇ ਵਾਵਹਿ ਰੂਪ ਕਰਹਿ ਸੀਗਾਰੁ ॥

gi-aanee nacheh vaajay vaaveh roop karahi seegaar.

Wanaoitwa wenye busara, wanafanya densi na kucheza tu ala zao za muziki, wakijipamba kwa mapambo mazuri.

**ਊਚੇ ਕੂਕਹਿ ਵਾਦਾ ਗਾਵਹਿ ਜੋਧਾ ਕਾ ਵੀਚਾਰੁ ॥**

oochay kookeh vaadaa gaavahi joDhaa kaa veechaar.

Wanapiga nduru kwa sauti, wakiimba kuhusu vita vya awali na tenzi za mashujaa.

**ਮੂਰਖ ਪੰਡਿਤ ਹਿਕਮਤਿ ਹੁਜਤਿ ਸੰਜੈ ਕਰਹਿ ਪਿਆਰੁ ॥**

moorakh pandit hikmat hujat sanjai karahi pi-aar

Wasomi na wabukuzi wa uongo wanapenda kukusanya utajiri wa kidunia kwa mabishano na hila za ujanja.

**ਧਰਮੀ ਧਰਮੁ ਕਰਹਿ ਗਾਵਾਵਹਿ ਮੰਗਹਿ ਮੋਖ ਦੁਆਰੁ ॥**

Dharmee Dharam karahi gaavaaveh mangeh mokh du-aar.

Watu waadilifu hupoteza ustahili wa uadilifu wao kwa kumuomba Mungu wokovu kama malipo.

**ਜਤੀ ਸਦਾਵਹਿ ਜੁਗਤਿ ਨ ਜਾਣਹਿ ਛਡਿ ਬਹਹਿ ਘਰ ਬਾਰੁ ॥**

jatee sadaaveh jugat na jaaneh chhad baheh ghar baar.

Wanajiita waseja, na kuacha nyumba zao, lakini hawafahamu njia ya kweli ya maisha.

**ਸਭੁ ਕੋ ਪੂਰਾ ਆਪੇ ਹੋਵੈ ਘਟਿ ਨ ਕੋਈ ਆਖੈ ॥**

sabh ko pooraa aapay hovai ghat na ko-ee aakhai.

Kila mtu hujiita kamili; hakuna anayejiita mpungufu.

**ਪਤਿ ਪਰਵਾਣਾ ਪਿਛੈ ਪਾਈਐ ਤਾ ਨਾਨਕ ਤੋਲਿਆ ਜਾਪੈ ॥੨॥**

pat parvaanaa pichhai paa-ee-ai taa naanak toli-aa jaapai. ||2||

Ee Nanak, sifa ya kweli ya mtu itajulikana tu pale ambapo mtu huyo anahukumiwa dhidi ya kipimo cha staha yake iliyopokelewa katika mahakama ya Mungu.

**ਮਃ ੧ ॥**

mehlaa 1.

Salok. Ya Guru wa Kwanza:

ਵਡੀ ਸੁ ਵਜਗਿ ਨਾਨਕਾ ਸਚਾ ਵੇਖੈ ਸੋਇ ॥

vadee so vajag naankaa sachaa vaykhai so-ay.

Ee Nanak, kile ambacho Mungu ameagiza ni sharti kitatendeka kwa sababu Yeye Mwenyewe anahakikisha (kwamba kila kitu kinatendeka kulingana na amri Yake).

ਸਭਨੀ ਛਾਲਾ ਮਾਰੀਆ ਕਰਤਾ ਕਰੇ ਸੁ ਹੋਇ ॥

sabhnee chhaalaa maaree-aa kartaa karay so ho-ay.

Kila mtu hufanya jitihada kuu kutenda kulingana na matakwa yao, lakini kinachotendeka pekee ni ambacho Muumba anatenda.

ਅਗੈ ਜਾਤਿ ਨ ਜੋਰੁ ਹੈ ਅਗੈ ਜੀਉ ਨਵੇ ॥

agai jaat na jor hai agai jee-o navay.

Katika mahakama ya Mungu, hadhi ya kijamii na nguvu haina maana, kwa sababu huko, mtu huhusiana na watu wapya kabisa (ambao hawayumbishwi na hadhi ya mtu yeyote)

ਜਿਨ ਕੀ ਲੇਖੈ ਪਤਿ ਪਵੈ ਚੰਗੇ ਸੇਈ ਕੇਇ ॥੩॥

jin kee laykhai pat pavai changay say-ee kay-ay. ||3||

Hao wachache tu ndio hufikiriwa kuwa wazuri au wema, ambao wametawazwa na staha akaunti yao inapochunguzwa katika mahakama ya Mungu.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਧੁਰਿ ਕਰਮੁ ਜਿਨਾ ਕਉ ਤੁਧੁ ਪਾਇਆ ਤਾ ਤਿਨੀ ਖਸਮੁ ਧਿਆਇਆ ॥

Dhur karam jinaa ka-o tuDh paa-i-aa taa tinee khasam Dhi-aa-i-aa.

Ee Mungu, ni waliotafakari kuhusu Wewe kwa ujitoaji wa upendo, ambao wameagiziwa tamati hiyo.

ਏਨਾ ਜੰਤਾ ਕੈ ਵਸਿ ਕਿਛੁ ਨਾਹੀ ਤੁਧੁ ਵੇਕੀ ਜਗਤੁ ਉਪਾਇਆ ॥

aynaa jantaa kai vas kichh naahee tuDh vaykee jagat upaa-i-aa.

Hakuna kitu kilicho katika nguvu ya viumbe hawa; Wewe umeumba dunia hii na watu wenye uwezo na tabia tofauti.

ਇਕਨਾ ਨੋ ਤੂੰ ਮੇਲਿ ਲੈਹਿ ਇਕਿ ਆਪਹੁ ਤੁਧੁ ਖੁਆਇਆ ॥

iknaa no tooN mayl laihi ik aaphu tuDh khu-aa-i-aa.

Wengine, Wewe unajiunganisha nao Mwenyewe, na wengine, Wewe unawapotosha.

ਗੁਰ ਕਿਰਪਾ ਤੇ ਜਾਣਿਆ ਜਿਥੈ ਤੁਧੁ ਆਪੁ ਬੁਝਾਇਆ ॥

gur kirpaa tay jaani-aa jithai tuDh aap bujhaa-i-aa.

Kwa yule ambaye Wewe umejidhihirisha, amekugundua Wewe kwa neema ya Guru.

ਸਹਜੇ ਹੀ ਸਚਿ ਸਮਾਇਆ ॥੧੧॥

sehjay hee sach samaa-i-aa. ||11||

Yeye ameunganishwa na Wewe kisilika.

ਸਲੋਕੁ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਦੁਖੁ ਦਾਰੂ ਸੁਖੁ ਰੋਗੁ ਭਇਆ ਜਾ ਸੁਖੁ ਤਾਮਿ ਨ ਹੋਈ ॥

dukh daaroo sukh rog bha-i-aa jaa sukh taam na ho-ee.

Ee Mungu, dunia hii Yako ni geni mno, ambapo mateso yanakuwa suluhisho, na raha inakuwa ugonjwa. Pale ambapo kuna raha tele, hakuna huzuni.

ਤੂੰ ਕਰਤਾ ਕਰਣਾ ਮੈ ਨਾਹੀ ਜਾ ਹਉ ਕਰੀ ਨ ਹੋਈ ॥੧॥

tooN kartaa karnaa mai naahee jaa ha-o karee na ho-ee. ||1||

Ee Mungu, Wewe ndiwe muumba na mtendaji wa vyote, mimi ni bure. Hata nikijaribu, hakuna kinachotendeka.

ਬਲਿਹਾਰੀ ਕੁਦਰਤਿ ਵਸਿਆ ॥

balihaaree kudrat vasi-aa.

Ee Muumba unayeenea kote, najiweka wakfu Kwako.

ਤੇਰਾ ਅੰਤੁ ਨ ਜਾਈ ਲਖਿਆ ॥੧॥ ਰਹਾਉ ॥

tayraa ant na jaa-ee lakhi-aa. ||1|| rahaa-o.

Vikomo vyako haviwezi kujulikana.

ਜਾਤਿ ਮਹਿ ਜੋਤਿ ਜੋਤਿ ਮਹਿ ਜਾਤਾ ਅਕਲ ਕਲਾ ਭਰਪੂਰਿ ਰਹਿਆ ॥

jaat meh jot jot meh jaataa akal kalaa bharpoor rahi-aa.

Mwanga Wako unaenea ulimwenguni kote, na Wewe unaonekana kama Mwanga katika viumbe vyote. Nguvu Yako kuu inaenea kote.

ਤੂੰ ਸਚਾ ਸਾਹਿਬੁ ਸਿਫਤਿ ਸੁਆਲਿਉ ਜਿਨਿ ਕੀਤੀ ਸੋ ਪਾਰਿ ਪਇਆ ॥

tooN sachaa saahib sifat su-aaliha-o jin keetee so paar pa-i-aa.

Ee Mungu, Wewe ndiwe Bwana wa Kweli; Sifa Yako ni nzuri sana. Yule anayeimba sifa Zako, hubebwa na kuvukishwa bahari dunia ya dhambi.

ਕਹੁ ਨਾਨਕ ਕਰਤੇ ਕੀਆ ਬਾਤਾ ਜੋ ਕਿਛੁ ਕਰਣਾ ਸੁ ਕਰਿ ਰਹਿਆ ॥੨॥

kaho naanak kartay kee-aa baataa jo kichh karnaa so kar rahi-aa. ||2||

Ee Nanak, imba sifa za Muumba; chochote anachopenda kufanya, Yeye anafanya.

ਮਃ ੨ ॥

mehlaa 2.

Salok, Guru wa Pili:

ਜੋਗ ਸਬਦੰ ਗਿਆਨ ਸਬਦੰ ਬੇਦ ਸਬਦੰ ਬ੍ਰਾਹਮਣਹ ॥

jog sabda$^N$ gi-aan sabda$^N$ bayd sabda$^N$ baraahmaneh.

Jukumu la kweli la Yogi ni kupata hekima takatifu; na jukumu la Brahmin (kuhani wa Kihindu) ni kujifunza na kutafakari Vedas.

ਖਤ੍ਰੀ ਸਬਦੰ ਸੂਰ ਸਬਦੰ ਸੂਦ੍ਰ ਸਬਦੰ ਪਰਾ ਕ੍ਰਿਤਹ ॥

khatree sabda$^N$ soor sabda$^N$ soodar sabda$^N$ paraa kirteh.

Jukumu la Kshatriya ni kupigana kwa ujasiri kwenye uwanja wa vita, na jukumu la Shudras ni kuwatumikia wengine.

ਸਰਬ ਸਬਦੰ ਏਕ ਸਬਦੰ ਜੇ ਕੋ ਜਾਣੈ ਭੇਉ ॥ ਨਾਨਕੁ ਤਾ ਕਾ ਦਾਸੁ ਹੈ ਸੋਈ ਨਿਰੰਜਨ ਦੇਉ ॥੩॥

sarab sabda$^N$ ayk sabda$^N$ jay ko jaanai bhay-o. naanak taa kaa daas hai so-ee niranjan day-o. ||3||

Lakini jukumu la wote ni kutafakari kuhusu Jina la Mungu. Nanak ni mtumishi wa yule ambaye anaijua siri hii kwa sababu yeye ni udhihirisho wa kimwili wa Mungu mtakatifu.

ਮਃ ੨ ॥

mehlaa 2.

Salok, Guru wa Pili:

ਏਕ ਕ੍ਰਿਸਨੰ ਸਰਬ ਦੇਵਾ ਦੇਵ ਦੇਵਾ ਤ ਆਤਮਾ ॥

ayk krisan$^N$ sarab dayvaa dayv dayvaa ta aatmaa.

Mungu huyo mmoja ndiye roho kuu ya miungu wote.

ਆਤਮਾ ਬਾਸੁਦੇਵਸ੍ਹਿ ਜੇ ਕੋ ਜਾਣੈ ਭੇਉ ॥ ਨਾਨਕੁ ਤਾ ਕਾ ਦਾਸੁ ਹੈ ਸੋਈ ਨਿਰੰਜਨ ਦੇਉ ॥੪॥

aatmaa baasdayvsi-y jay ko jaanai bhay-o. naanak taa kaa daas hai so-ee niranjan day-o. ||4||

Yule anayeelewa fumbo hilo, kwamba roho yenyewe ni Mungu, yeye ni udhihirisho wa kimwili wa Mungu safi na Nanak ni mtumishi wake.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਕੁੰਭੇ ਬਧਾ ਜਲੁ ਰਹੈ ਜਲ ਬਿਨੁ ਕੁੰਭੁ ਨ ਹੋਇ ॥

kumbhay baDhaa jal rahai jal bin kumbh na ho-ay.

Kama vile maji yanabaki yamedhibitiwa kwenye mtungi, lakini pasipo maji, mtungi haungeundwa.

ਗਿਆਨ ਕਾ ਬਧਾ ਮਨੁ ਰਹੈ ਗੁਰ ਬਿਨੁ ਗਿਆਨੁ ਨ ਹੋਇ ॥੫॥

gi-aan kaa baDhaa man rahai gur bin gi-aan na ho-ay. ||5||

Vivyo hivyo, akili inazuiliwa kutokana na maovu kwa maarifa matakatifu, lakini maarifa matakatifu hayawezi kupatikana bila mafundisho ya Guru.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਪੜਿਆ ਹੋਵੈ ਗੁਨਹਗਾਰੁ ਤਾ ਓਮੀ ਸਾਧੁ ਨ ਮਾਰੀਐ ॥

parhi-aa hovai gunahgaar taa omee saaDh na maaree-ai.

Iwapo mtu aliyeelimika ni mtenda dhambi, yeye ataadhibiwa, lakini mtu mwema, ijapokuwa hajaelimika, hawezi kuadhibiwa.

ਜੇਹਾ ਘਾਲੇ ਘਾਲਣਾ ਤੇਵੇਹੋ ਨਾਉ ਪਚਾਰੀਐ ॥

jayhaa ghaalay ghaalnaa tayvayho naa-o pachaaree-ai.

Kama vilivyo vitendo vilivyotendwa, ndivyo ilivyo sifa mtu anayopata.

ਐਸੀ ਕਲਾ ਨ ਖੇਡੀਐ ਜਿਤੁ ਦਰਗਹ ਗਇਆ ਹਾਰੀਐ ॥

aisee kalaa na khaydee-ai jit dargeh ga-i-aa haaree-ai.

Hivyo basi, usicheze mchezo kama huo, ambao utakufanya upoteze mchezo wa uzao wa kibinadamu katika mahakama ya Mungu.

ਪੜਿਆ ਅਤੈ ਓਮੀਆ ਵੀਚਾਰੁ ਅਗੈ ਵੀਚਾਰੀਐ ॥

parhi-aa atai omee-aa veechaar agai veechaaree-ai.

Matendo ya walioelimika na ambao hawajaelimika yatahukumiwa katika mahakama ya Mungu.

ਮੁਹਿ ਚਲੈ ਸੁ ਅਗੈ ਮਾਰੀਐ ॥੧੨॥

muhi chalai so agai maaree-ai. ||12||

Mtu ambaye badala ya kufuata mafundisho ya Guru, kwa kiburi anafuata akili yake mwenyewe anaadhibiwa katika mahakama ya Mungu.

ਸਲੋਕੁ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, na Guru wa Kwanza:

ਨਾਨਕ ਮੇਰੁ ਸਰੀਰ ਕਾ ਇਕੁ ਰਥੁ ਇਕੁ ਰਥਵਾਹੁ ॥

naanak mayr sareer kaa ik rath ik rathvaahu.

Ee Nanak, mwili wa binadamu, ambao ndio mkuu kati ya spishi zote, una gari (maadili) na dereva (kanuni).

ਜੁਗੁ ਜੁਗੁ ਫੇਰਿ ਵਟਾਈਅਹਿ ਗਿਆਨੀ ਬੁਝਹਿ ਤਾਹਿ ॥

jug jug fayr vataa-ee-ah gi-aanee bujheh taahi.

Katika kila enzi maadili na kanuni hizi zinazidi kubadilika; ni watu wenye hekima tu wanaoelewa hii.

ਸਤਜੁਗਿ ਰਥੁ ਸੰਤੋਖ ਕਾ ਧਰਮੁ ਅਗੈ ਰਥਵਾਹੁ ॥

satjug rath santokh kaa Dharam agai rathvaahu.

Katika Sat Jug, kuridhika ndiko kulikuwa gari (maadili) na uadilifu ulikuwa dereva (kanuni)

ਤ੍ਰੇਤੈ ਰਥੁ ਜਤੈ ਕਾ ਜੋਰੁ ਅਗੈ ਰਥਵਾਹੁ ॥

taraytai rath jatai kaa jor agai rathvaahu.

Katika enzi ya Treta, useja ndio ulikuwa gari na nguvu ya nia ilikuwa dereva.

ਦੁਆਪੁਰਿ ਰਥੁ ਤਪੈ ਕਾ ਸਤੁ ਅਗੈ ਰਥਵਾਹੁ ॥

du-aapur rath tapai kaa sat agai rathvaahu.

Katika enzi ya Puapar, toba ndiyo ilikuwa gari na silica njema ilikuwa dereva.

ਕਲਜੁਗਿ ਰਥੁ ਅਗਨਿ ਕਾ ਕੂੜੁ ਅਗੈ ਰਥਵਾਹੁ ॥੧॥

kaljug rath agan kaa koorh agai rathvaahu. ||1||

Katika Enzi hii ya Kal Jug, moto wa hamu ya utajiri na nguvu ya kidunia ndio gari na udanganyifu ni dereva.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਸਾਮ ਕਹੈ ਸੇਤੰਬਰੁ ਸੁਆਮੀ ਸਚ ਮਹਿ ਆਛੈ ਸਾਚਿ ਰਹੇ ॥ ਸਭੁ ਕੋ ਸਚਿ ਸਮਾਵੈ ॥

saam kahai saytambar su-aamee sach meh aachhai saach rahay. sabh ko sach samaavai.

Saam Veda anasema kwamba (katika Sat Jug) Bwana wa Dunia (Mungu) alijulikana kama Saytambar. Katika Enzi hiyo kila mtu alitamani ukweli, na kuishi kwa ukweli na uadilifu.

ਰਿਗੁ ਕਹੈ ਰਹਿਆ ਭਰਪੂਰਿ ॥ ਰਾਮ ਨਾਮੁ ਦੇਵਾ ਮਹਿ ਸੂਰੁ ॥

rig kahai rahi-aa bharpoor. raam naam dayvaa meh soor.

Rig Veda anasema kwamba (katika Treta Jug), Mungu anaenea kote na kati ya miungu, jina la Bwana Rama ndilo lililokwezwa kabisa, liking'aa kama jua.

ਨਾਇ ਲਇਐ ਪਰਾਛਤ ਜਾਹਿ ॥ ਨਾਨਕ ਤਉ ਮੋਖੰਤਰੁ ਪਾਹਿ ॥

naa-ay la-i-ai paraachhat jaahi. Naanak ta-o mokhantar paahi.

Ee Nanak, (kulingana na Rig Veda), dhambi zote zinaangamizwa kwa kuimba Jina la Bwana Rama, kisha binadamu anatimiza wokovu.

ਜੁਜ ਮਹਿ ਜੋਰਿ ਛਲੀ ਚੰਦ੍ਰਾਵਲਿ ਕਾਨ੍ਹ ਕ੍ਰਿਸਨੁ ਜਾਦਮੁ ਭਇਆ ॥

juj meh jor chhalee chandraaval kaan$^H$ krisan jaadam bha-i-aa.

Yajur Veda anasema kwamba (katika Dwapar Jug), bwana wa dunia alijulikana kama Bwana Krishna wa tabaka la Yadava, aliyemdanganya binti wa mfalme Chandravali kwa nguvu yake ya kimungu,

ਪਾਰਜਾਤੁ ਗੋਪੀ ਲੈ ਆਇਆ ਬਿੰਦ੍ਰਾਬਨ ਮਹਿ ਰੰਗੁ ਕੀਆ ॥

paarjaat gopee lai aa-i-aa bindraaban meh rang kee-aa.

Yeye aliuleta mti wa kihadithi unaotimiza matakwa ulioitwa Parjaat kwa Gopi wake (mtawa wa kike) na kuburudika katika Vrindavan.

ਕਲਿ ਮਹਿ ਬੇਦੁ ਅਥਰਬਣੁ ਹੂਆ ਨਾਉ ਖੁਦਾਈ ਅਲਹੁ ਭਇਆ ॥

kal meh bayd atharban hoo-aa naa-o khudaa-ee alhu bha-i-aa.

Katika Enzi ya Kali Yuga, Atharva Veda alifanywa mkuu; Allah likaja kuwa Jina la Mungu.

ਨੀਲ ਬਸਤ੍ਰ ਲੇ ਕਪੜੇ ਪਹਿਰੇ ਤੁਰਕ ਪਠਾਣੀ ਅਮਲੁ ਕੀਆ ॥

neel bastar lay kaprhay pahiray turak pathaanee amal kee-aa.

Waturuki na Wapathani walichukua mamlaka na wakaanza kuvaa mavazi ya samawati.

ਚਾਰੇ ਵੇਦ ਹੋਏ ਸਚਿਆਰ ॥

chaaray vayd ho-ay sachiaar.

Kwa njia hii Vedas zote nne zinadai ukweli wao wenyewe kulingana na nyakati zao husika.

ਪੜਹਿ ਗੁਣਹਿ ਤਿਨ੍ ਚਾਰ ਵੀਚਾਰ ॥

parheh guneh tin[H] chaar veechaar.

Kwa kusoma na kutafakari kuhusu vedas hizi, watu husitawisha fikira nzuri akilini mwao.

ਭਾਉ ਭਗਤਿ ਕਰਿ ਨੀਚੁ ਸਦਾਏ ॥ ਤਉ ਨਾਨਕ ਮੋਖੰਤਰੁ ਪਾਏ ॥੨॥

bhaa-o bhagat kar neech sadaa-ay. ta-o naanak mokhantar paa-ay. ||2||

Lakini, Ee Nanak, ni yeye tu anayefanya ibada ya upendo kwa Mungu na kusalia mnyenyekevu anayetimiza ukombozi.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਸਤਿਗੁਰ ਵਿਟਹੁ ਵਾਰਿਆ ਜਿਤੁ ਮਿਲਿਐ ਖਸਮੁ ਸਮਾਲਿਆ ॥

satgur vitahu vaari-aa jit mili-ai khasam samaali-aa.

Ninaweka wakfu maisha yangu kwa Guru wa Kweli; ambaye kwa kukutana naye, nimekuja kumthamini Mungu.

ਜਿਨਿ ਕਰਿ ਉਪਦੇਸੁ ਗਿਆਨ ਅੰਜਨੁ ਦੀਆ ਇਨ੍ਹੀ ਨੇਤ੍ਰੀ ਜਗਤੁ ਨਿਹਾਲਿਆ ॥

jin kar updays gi-aan anjan dee-aa in[H]ee naytree jagat nihaali-aa.

Guru wa kweli ambaye ameangaza akili yangu kwa mafundisho yake kana kwamba yeye ameweka mafuta ya maarifa takatifu machoni mwangu, na kwa hiyo ninatazama ukweli kuhusu dunia.

ਖਸਮੁ ਛੋਡਿ ਦੂਜੈ ਲਗੇ ਡੁਬੇ ਸੇ ਵਣਜਾਰਿਆ ॥

khasam chhod doojai lagay dubay say vanjaari-aa.

Wale wanaomwacha Bwana wao wa kweli na kujiambatisha kwa mwengine, huzamishwa katika bahari ya kidunia ya dhambi.

ਸਤਿਗੁਰੂ ਹੈ ਬੋਹਿਥਾ ਵਿਰਲੈ ਕਿਨੈ ਵੀਚਾਰਿਆ ॥

satguroo hai bohithaa virlai kinai veechaari-aa.

Ni wachache tu wanaogundua kwamba Guru wa Kweli ni kama meli (ya kutuvukisha bahari ya kidunia ya dhambi)

ਕਰਿ ਕਿਰਪਾ ਪਾਰਿ ਉਤਾਰਿਆ ॥੧੩॥

kar kirpaa paar utaari-aa. ||13||

Kwa kunijalia Neema Yake, Yeye amenisaidia kuvuka bahari ya kidunia ya dhambi.

ਸਲੋਕੁ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਸਿੰਮਲ ਰੁਖੁ ਸਰਾਇਰਾ ਅਤਿ ਦੀਰਘ ਅਤਿ ਮੁਚੁ ॥

simmal rukh saraa-iraa at deeragh at much.

Mti wa msimali ni mnyofu kama mshale; ni mrefu mno, na mpana mno.

ਓਇ ਜਿ ਆਵਹਿ ਆਸ ਕਰਿ ਜਾਹਿ ਨਿਰਾਸੇ ਕਿਤੁ ॥

o-ay je aavahi aas kar jaahi niraasay kit.

Lakini ndege wanaokuja na kuukalia kwa tumaini la kula tunda lake, kwa nini huondoka huku wamevunjika moyo?

ਫਲ ਫਿਕੇ ਫੁਲ ਬਕਬਕੇ ਕੰਮਿ ਨ ਆਵਹਿ ਪਤ ॥

fal fikay ful bakbakay kamm na aavahi pat.

Kwa sababu matunda yake hayana ladha, maua yake yanaleta kichefuchefu, na matawi yake ni bure.

ਮਿਠਤੁ ਨੀਵੀ ਨਾਨਕਾ ਗੁਣ ਚੰਗਿਆਈਆ ਤਤੁ ॥

mithat neevee naankaa gun chang-aa-ee-aa tat.

(Vivyo hivyo bila utamu na unyenyekevu, mwonyesho wote wa ukuu hauna maana). Ee Nanak, sifa ya utamu kwa unyenyekevu ndicho kiini cha fadhila zote.

ਸਭੁ ਕੋ ਨਿਵੈ ਆਪ ਕਉ ਪਰ ਕਉ ਨਿਵੈ ਨ ਕੋਇ ॥

sabh ko nivai aap ka-o par ka-o nivai na ko-ay.

Kila mtu huinama kwa ajili yake mwenyewe, na sio kwa ajili ya wengine.

ਧਰਿ ਤਾਰਾਜੂ ਤੋਲੀਐ ਨਿਵੈ ਸੁ ਗਉਰਾ ਹੋਇ ॥

Dhar taaraajoo tolee-ai nivai so ga-uraa ho-ay.

tunafaa kuona kwamba kitu kinapowekwa kwenye mizani, upande ulio chini unafikiriwa kuwa mzito zaidi (vivyo hivyo, yeye anayeonyesha unyenyekevu anafikiriwa kuwa mtu mwema zaidi)

ਅਪਰਾਧੀ ਦੂਣਾ ਨਿਵੈ ਜੋ ਹੰਤਾ ਮਿਰਗਾਹਿ ॥

apraaDhee doonaa nivai jo hantaa miragaahi.

Mtenda dhambi, kama mwindaji wa kulungu, huinama mara mbili zaidi kwa ajili ya nia yake binafsi.

ਸੀਸਿ ਨਿਵਾਇਐ ਕਿਆ ਥੀਐ ਜਾ ਰਿਦੈ ਕੁਸੁਧੇ ਜਾਹਿ ॥੧॥

sees nivaa-i-ai ki-aa thee-ai jaa ridai kusuDhay jaahi. ||1||

Lakini nini kinachoweza kutimizwa kwa kuonyesha unyenyekevu kwa kuinamisha kichwa iwapo moyo unasalia na udanganyifu na ulaghai.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਪੜਿ ਪੁਸਤਕ ਸੰਧਿਆ ਬਾਦੰ ॥

parh pustak sanDhi-aa baada[N].

Mwalimu wa kihindu husoma vitabu vitakatifu na kusali kila siku, na kisha anajishughulisha na mjadala.

ਸਿਲ ਪੂਜਸਿ ਬਗੁਲ ਸਮਾਧੰ ॥

sil poojas bagul samaaDha[N].

Yeye huabudu mawe na kisha kuketi kama kongoti, akijifanya kuwa katika Samadhi.

ਮੁਖਿ ਝੂਠ ਬਿਭੂਖਣ ਸਾਰੰ ॥

mukh jhooth bibhookhan saara[N].

Yeye hutamka udanganyifu, na kupamba uongo wake kama mapambo mazuri,

ਤ੍ਰੈਪਾਲ ਤਿਹਾਲ ਬਿਚਾਰੰ ॥

taraipaal tihaal bichaara[N].

Yeye hukariri sentensi tatu za Gayatri mantra mara tatu kwa siku

ਗਲਿ ਮਾਲਾ ਤਿਲਕੁ ਲਿਲਾਟੰ ॥

gal maalaa tilak lilaata[N].

Shingoni pake kuna rosari, na kwenye paji lake kuna tilak-ishara takatifu;

ਦੁਇ ਧੋਤੀ ਬਸਤ੍ਰ ਕਪਾਟੰ ॥

du-ay Dhotee bastar kapaata[N].

Yeye daima huwa na mavazi mawili ya kiunoni na kuvaa kilemba kichwani pake anaposali.

ਜੇ ਜਾਣਸਿ ਬ੍ਰਹਮੰ ਕਰਮੰ ॥

jay jaanas barahma[N] karma[N].

Lakini iwapo angejua vitendo vya kimungu (sifa za Mungu),

ਸਭਿ ਫੋਕਟ ਨਿਸਚਉ ਕਰਮੰ ॥

sabh fokat nischa-o karma[N].

Basi kwa uhakika yeye angegundua kwamba itikadi na mila hizo zote ni bure.

ਕਹੁ ਨਾਨਕ ਨਿਹਚਉ ਧਿਆਵੈ ॥

kaho naanak nihcha-o Dhi-aavai.

Ee Nanak, tafakari kuhusu Mungu kwa imani kamili.

ਵਿਣੁ ਸਤਿਗੁਰ ਵਾਟ ਨ ਪਾਵੈ ॥੨॥

vin satgur vaat na paavai. ||2||

Pasipo mafundisho ya Guru wa Kweli, hakuna mtu anayepata njia sahihi.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਕਪੜੁ ਰੂਪੁ ਸੁਹਾਵਣਾ ਛਡਿ ਦੁਨੀਆ ਅੰਦਰਿ ਜਾਵਣਾ ॥

kaparh roop suhaavanaa chhad dunee-aa andar jaavnaa.

Mtu ataondoka duniani na kuuacha mwili mzuri hapa.

ਮੰਦਾ ਚੰਗਾ ਆਪਣਾ ਆਪੇ ਹੀ ਕੀਤਾ ਪਾਵਣਾ ॥

mandaa changa aapnaa aapay hee keetaa paavnaa.

Yeye atastahimili matokeo ya vitendo vyake vizuri na vibaya.

ਹੁਕਮ ਕੀਏ ਮਨਿ ਭਾਵਦੇ ਰਾਹਿ ਭੀੜੈ ਅਗੈ ਜਾਵਣਾ ॥

hukam kee-ay man bhaavday raahi bheerhai agai jaavnaa.

Mtu, ambaye ameishi maisha kulingana na mapenzi yake (kutoa amri kulingana na mapenzi yake bila kujali kiwango cha mateso ambacho ameletea wengine), atapaswa kustahimili mateso kama hayo, kana kwamba anafinywa na kubanwa kupitia kwa njia nyebamba baadaye.

ਨੰਗਾ ਦੋਜਕਿ ਚਾਲਿਆ ਤਾ ਦਿਸੈ ਖਰਾ ਡਰਾਵਣਾ ॥

nangaa dojak chaali-aa taa disai kharaa daraavanaa.

vitendo vyake viovu vinapodhihirishwa, yeye huonekana mkirihifu akiteseka.

ਕਰਿ ਅਉਗਣ ਪਛੋਤਾਵਣਾ ॥੧੪॥

kar a-ugan pachhotaavanaa. ||14||

Kisha, yeye hujutia dhambi alizozitenda.

ਸਲੋਕੁ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਦਇਆ ਕਪਾਹ ਸੰਤੋਖੁ ਸੂਤੁ ਜਤੁ ਗੰਢੀ ਸਤੁ ਵਟੁ ॥

da-i-and kapaah santokh soot jat gandhee sat vat.

Ee mbukuzi, janaeou (uzi mtakatifu) ambao umetengenezwa kwa ukarimu badala ya pamba, kwa kutumia nyuzi za kuridhika, mafundo ya useja, na viringa vya silika ya juu,

ਏਹੁ ਜਨੇਊ ਜੀਅ ਕਾ ਹਈ ਤ ਪਾਡੇ ਘਤੁ ॥

ayhu janay-oo jee-a kaa ha-ee ta paaday ghat.

Ni uzi mtakatifu halisi ambao una manufaa kwa roho, iwapo unao, basi uweke shingoni pangu.

ਨਾ ਏਹੁ ਤੁਟੈ ਨ ਮਲੁ ਲਗੈ ਨਾ ਏਹੁ ਜਲੈ ਨ ਜਾਇ ॥

naa ayhu tutai na mal lagai naa ayhu jalai na jaa-ay.

Kwa sababu janaeou (uzi mtakatifu) kama huo hauvunjiki, wala kuchafuka, wala kuchomeka, na kamwe haupotei.

ਧੰਨੁ ਸੁ ਮਾਣਸ ਨਾਨਕਾ ਜੋ ਗਲਿ ਚਲੇ ਪਾਇ ॥

Dhan so maanas naankaa jo gal chalay paa-ay.

Ee Nanak, amebarikiwa mtu huyo anayeondoka duniani akivaa janaeou (uzi mtakatifu) kama hiyo.

ਚਉਕੜਿ ਮੁਲਿ ਅਣਾਇਆ ਬਹਿ ਚਉਕੇ ਪਾਇਆ ॥

cha-ukarh mul anaa-i-aa bahi cha-ukai paa-i-aa.

Ee Mwalimu wa kidini, wewe unanunua uzi huu kwa senti nne na ukikaa jikoni kwa mwenyeji, unauweka shingoni pake.

ਸਿਖਾ ਕੰਨਿ ਚੜਾਈਆ ਗੁਰੁ ਬ੍ਰਾਹਮਣੁ ਥਿਆ ॥

sikhaa kann charhaa-ee-aa gur baraahman thi-aa.

Kisha unanong'ona sikioni pake kwamba tangia sasa yeye, Brahmini, amekuwa Guru wake.

ਓਹੁ ਮੁਆ ਓਹੁ ਝੜਿ ਪਇਆ ਵੇਤਗਾ ਗਇਆ ॥੧॥

oh mu-aa oh jharh pa-i-aa vaytgaa ga-i-aa. ||1||

Lakini mwanaume huyo anapokufa, uzi huo mtakatifu unachomwa, na mtu huyo anakwenda kwa mahakama ya Mungu bila uzi.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਲਖ ਚੋਰੀਆ ਲਖ ਜਾਰੀਆ ਲਖ ਕੂੜੀਆ ਲਖ ਗਾਲਿ ॥

lakh choree-aa lakh jaaree-aa lakh koorhee-aa lakh gaal.

Wanadamu wanatenda maelfu ya wizi, maelfu ya vitendo vya uzinifu, maelfu ya udanganyifu na maelfu ya matusi.

ਲਖ ਠਗੀਆ ਪਹਿਨਾਮੀਆ ਰਾਤਿ ਦਿਨਸੁ ਜੀਅ ਨਾਲਿ ॥

lakh thagee-aa pahinaamee-aa raat dinas jee-a naal.

Usiku na mchana, wanatenda maelfu ya ulaghai na vitendo viovu dhidi ya binadamu wenzao.

ਤਗੁ ਕਪਾਹਹੁ ਕਤੀਐ ਬਾਮ੍ਹਣੁ ਵਟੇ ਆਇ ॥

tag kapaahahu katee-ai baam$^{H}$an vatay aa-ay

ila, wakati Brahmini anakuja nyumbani, yeye hukunja uzi Fulani uliosokotwa kutoka kwa pamba

ਕੁਹਿ ਬਕਰਾ ਰਿੰਨ੍ਹਿ ਖਾਇਆ ਸਭੁ ਕੋ ਆਖੈ ਪਾਇ ॥

kuhi bakraa rinni$^{H}$ khaa-i-aa sabh ko aakhai paa-ay.

Kisha mbuzi anachinjwa, kupikwa na kuliwa na wote; kila mtu husema, ‘uzi mtakatifu umevaliwa’.

ਹੋਇ ਪੁਰਾਣਾ ਸੁਟੀਐ ਭੀ ਫਿਰਿ ਪਾਈਐ ਹੋਰੁ ॥

ho-ay puraanaa sutee-ai bhee fir paa-ee-ai hor.

Uzi huu unapochakaa, hutupwa, na mwingine kuwekwa kwenye nafasi yake.

ਨਾਨਕ ਤਗੁ ਨ ਤੁਟਈ ਜੇ ਤਗਿ ਹੋਵੈ ਜੋਰੁ ॥੨॥

naanak tag na tut-ee jay tag hovai jor. ||2||

Ee Nanak, uzi kamwe haungevunjika iwapo ungekuwa na nguvu ya kiroho (ya ukarimu, kuridhika na silika ya juu).

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਨਾਇ ਮੰਨਿਐ ਪਤਿ ਊਪਜੈ ਸਾਲਾਹੀ ਸਚੁ ਸੂਤੁ ॥

naa-ay mani-ai pat oopjai saalaahee sach soot.

Tunapata staha katika mahakama ya Mungu wakati tu tunapothamini Jina Lake moyoni mwetu, kwa sababu kuimba sifa za Mungu ni uzi mtakatifu wa kweli.

ਦਰਗਹ ਅੰਦਰਿ ਪਾਈਐ ਤਗੁ ਨ ਤੂਟਸਿ ਪੂਤ ॥੩॥

dargeh andar paa-ee-ai tag na tootas poot. ||3||

Kwa kuvaa uzi mtakatifu kama huo, mtu hupokea staha katika mahakama ya Mungu na janaeou (uzi mtakatifu) kama hiyo kamwe haivunjiki.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, ya Guru wa Kwanza:

ਤਗੁ ਨ ਇੰਦ੍ਰੀ ਤਗੁ ਨ ਨਾਰੀ ॥

tag na indree tag na naaree.

Mwalimu wa kidini mwenyewe havai uzi wowote kwa hisi zake ili kuzidhibiti kutokana na maovu, hakuna janaeou (uzi mtakatifu) ya wanawake.

ਭਲਕੇ ਥੁਕ ਪਵੈ ਨਿਤ ਦਾੜੀ ॥

bhalkay thuk pavai nit daarhee.

Kila siku, watu wanatenda dhambi na kuaibishwa.

ਤਗੁ ਨ ਪੈਰੀ ਤਗੁ ਨ ਹਥੀ ॥

tag na pairee tag na hathee.

Hakuna uzi mtakatifu wa miguu ili kuizuia kuenda mahali pabaya, na hakuna uzi mtakatifu wa mikono kuizuia kutoka kutenda maovu.

ਤਗੁ ਨ ਜਿਹਵਾ ਤਗੁ ਨ ਅਖੀ ॥

tag na jihvaa tag na akhee.

Hakuna uzi mtakatifu wa ulimi kuuzuia kuchongeza na hakuna uzi mtakatifu wa macho kuyazuia kutazama kwa nia mbaya.

ਵੇਤਗਾ ਆਪੇ ਵਤੈ ॥ਵਟਿ ਧਾਗੇ ਅਵਰਾ ਘਤੈ ॥

vaytgaa aapay vatai.vat Dhaagay avraa ghatai. vat Dhaagay avraa ghatai.

Ijapokuwa Mwalimu mwenyewe anazurura kote bila uzi wowote wa udhibiti wa kimaadili, yeye hutengeneza na kuweka nyuzi kwa wengine.

ਲੈ ਭਾੜਿ ਕਰੇ ਵੀਆਹੁ ॥

lai bhaarh karay vee-aahu.

Yeye hupokea malipo kwa kutekeleza ndoa;

ਕਢਿ ਕਾਗਲੁ ਦਸੇ ਰਾਹੁ ॥

kadh kaagal dasay raahu.

Kwa kusoma utabiri wao wa nyota, yeye huwaonyesha njia (siku zenye bahati nzuri).

ਸੁਣਿ ਵੇਖਹੁ ਲੋਕਾ ਏਹੁ ਵਿਡਾਣੁ ॥

sun vaykhhu lokaa ayhu vidaan.

Enyi watu, tazameni na msikilize mchezo huu wa ajabu.

ਮਨਿ ਅੰਧਾ ਨਾਉ ਸੁਜਾਣੁ ॥੪॥

man anDhaa naa-o sujaan. ||4||

Ijapokuwa yeye (mwalimu wa kidini) ni kipofu kiakili (mjinga kiroho), ila yeye anajiita mwenye hekima.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਸਾਹਿਬੁ ਹੋਇ ਦਇਆਲੁ ਕਿਰਪਾ ਕਰੇ ਤਾ ਸਾਈ ਕਾਰ ਕਰਾਇਸੀ ॥

saahib ho-ay da-i-aal kirpaa karay taa saa-ee kaar karaa-isee.

Bwana-Mungu anapokuwa mwenye neema na kutawaza huruma kwa mtu, Yeye humfanya kutenda tu kinachomnpendeza Yeye.

ਸੋ ਸੇਵਕੁ ਸੇਵਾ ਕਰੇ ਜਿਸ ਨੋ ਹੁਕਮੁ ਮਨਾਇਸੀ ॥

so sayvak sayvaa karay jis no hukam manaa-isee.

Mtumishi (mtawa) huyo tu anayemtumikia Yeye ndiye tu anayemfanya kutii Amri Yake.

ਹੁਕਮਿ ਮੰਨਿਐ ਹੋਵੈ ਪਰਵਾਣੁ ਤਾ ਖਸਮੈ ਕਾ ਮਹਲੁ ਪਾਇਸੀ ॥

hukam mani-ai hovai parvaan taa khasmai kaa mahal paa-isee.

Kwa kutii Amri Yake, yeye anakubalika katika mahakama ya Mungu na kumgundua Bwana-Mungu.

ਖਸਮੈ ਭਾਵੈ ਸੋ ਕਰੇ ਮਨਹੁ ਚਿੰਦਿਆ ਸੋ ਫਲੁ ਪਾਇਸੀ ॥

khasmai bhaavai so karay manhu chindi-aa so fal paa-isee.

mtawa anapofanya kinachompendeza Bwana Wake, basi yeye hupokea matunda ya hamu za akili yake.

ਤਾ ਦਰਗਹ ਪੈਧਾ ਜਾਇਸੀ ॥੧੫॥

taa dargeh paiDhaa jaa-isee. ||15||

Kisha, yeye huenda kwa Mahakama ya Mungu kwa staha.

ਸਲੋਕ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

**ਗਊ ਬਿਰਾਹਮਣ ਕਉ ਕਰੁ ਲਾਵਹੁ ਗੋਬਰਿ ਤਰਣੁ ਨ ਜਾਈ ॥**

ga-oo biraahman ka-o kar laavhu gobar taran na jaa-ee.

Ee Mwalimu wa kidini, ng'ombe na Brahmin wanafikiriwa kuwa watakatifu nawe, bado unatooza ushuru kwao. Kumbuka kwamba kupaka samadi ya ng'ombe kwenye sakafu jikoni hakutakusaidia kuvuka bahari dunia ya dhambi.

**ਧੋਤੀ ਟਿਕਾ ਤੈ ਜਪਮਾਲੀ ਧਾਨੁ ਮਲੇਛਾਂ ਖਾਈ ॥**

Dhotee tikaa tai japmaalee Dhaan malaychhaa^N khaa-ee.

Wewe unavaa vazi la kiunoni, kupaka alama ya pajini, na kubeba rosari, lakini unapokea riziki yako kutoka kwa Waislamu ambao unawaita Malech (walio najisi).

**ਅੰਤਰਿ ਪੂਜਾ ਪੜਹਿ ਕਤੇਬਾ ਸੰਜਮੁ ਤੁਰਕਾ ਭਾਈ ॥**

antar poojaa parheh kataybaa sanjam turkaa bhaa-ee.

Unaabudu sanamu zilizofichwa ndani, lakini nje unasoma vitabu vya Kiislamu kama Quran ili kupendeza watawala wa Kiislamu nawe unapenda mtindo wa maisha wa Kiislamu.

**ਛੋਡੀਲੇ ਪਾਖੰਡਾ ॥**

chhodeelay paakhandaa.

Kata unafiki wako kabisa,

**ਨਾਮਿ ਲਇਐ ਜਾਹਿ ਤਰੰਦਾ ॥੧॥**

naam la-i-ai jaahi tarandaa. ||1||

Kwa sababu ni kwa kumkumbuka Mungu tu ambapo unaweza kuogelea na kuvuka bahari ya kidunia ya dhambi.

**ਮਃ ੧ ॥**

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਮਾਣਸ ਖਾਣੇ ਕਰਹਿ ਨਿਵਾਜ ॥

maanas khaanay karahi nivaaj.

Watawala fisadi wa Kiislamu wananyanyasa raia wao, lakini wanasali sala zao za kila siku (Nimaz)

ਛੁਰੀ ਵਗਾਇਨਿ ਤਿਨ ਗਲਿ ਤਾਗ ॥

chhuree vagaa-in tin gal taag.

Waajiriwa wao wa Kihindu, wakivaa uzi mtakatifu shingoni pao, wanawatesa maskini.

ਤਿਨ ਘਰਿ ਬ੍ਰਹਮਣ ਪੂਰਹਿ ਨਾਦ ॥

tin ghar barahman pooreh naad.

Nyumbani mwa waajiriwa hao wadhalimu wa Kihindu, Brahmin wanacheza shankh (duvi) ili watuzwe.

ਉਨ੍ਹਾ ਭਿ ਆਵਹਿ ਓਈ ਸਾਦ ॥

un^H^aa bhe aavahi o-ee saad.

Brahmin pia wanafurahia kionjo cha utajiri wao uliokusanywa kwa njia potovu.

ਕੂੜੀ ਰਾਸਿ ਕੂੜਾ ਵਾਪਾਰੁ ॥

koorhee raas koorhaa vaapaar.

uongo ndio rasilimali yao, na biashara yao ni ya uongo (msingi wa shughuli zao zote ni udanganyifu).

ਕੂੜੁ ਬੋਲਿ ਕਰਹਿ ਆਹਾਰੁ ॥

koorh bol karahi aahaar.

Wanachuma riziki yao kwa kusema uongo.

ਸਰਮ ਧਰਮ ਕਾ ਡੇਰਾ ਦੂਰਿ ॥

saram Dharam kaa dayraa door

Hawana hisia za aibu na wanatenda vitendo vyote vya uadilifu.

ਨਾਨਕ ਕੂੜੁ ਰਹਿਆ ਭਰਪੂਰਿ ॥

naanak koorh rahi-aa bharpoor.

Ee Nanak, udanganyifu unadumu kote.

ਮਥੈ ਟਿਕਾ ਤੇੜਿ ਧੋਤੀ ਕਖਾਈ ॥

mathai tikaa tayrh Dhotee kakhaa-ee.

Kwa alama takatifu kwenye paji zao, na mavazi ya kiuno ya zafarani kwenye viuno vyao (hutangaza utakatifu kutoka nje).

ਹਥਿ ਛੁਰੀ ਜਗਤ ਕਾਸਾਈ ॥

hath chhuree jagat kaasaa-ee.

Lakini kwa uhalisia, wao hutesa maskini, kana kwamba wao ni wachinjaji wenye visu mikononi mwao.

ਨੀਲ ਵਸਤ੍ਰ ਪਹਿਰਿ ਹੋਵਹਿ ਪਰਵਾਣੁ ॥

neel vastar pahir hoveh parvaan.

Wakivaa joho za samawati, wanatafuta idhinisho ya watawala wao wa Kiislamu.

ਮਲੇਛ ਧਾਨੁ ਲੇ ਪੂਜਹਿ ਪੁਰਾਣੁ ॥

malaychh Dhaan lay poojeh puraan.

Wao hupokea riziki yao kutoka kwa Waislamu ambao wanaita malech (walio najisi) na wanaabudu Puranas.

ਅਭਾਖਿਆ ਕਾ ਕੁਠਾ ਬਕਰਾ ਖਾਣਾ ॥

abhaakhi-aa kaa kuthaa bakraa khaanaa.

Wao hula nyama ya mbuzi, waliochinjwa baada ya kusoma sala ya Kiislamu (Kalma).

ਚਉਕੇ ਉਪਰਿ ਕਿਸੈ ਨ ਜਾਣਾ ॥

cha-ukay upar kisai na jaanaa.

ilhali wanasema kwamba hakuna mwingine anayestahili kuingia jikoni mwao.

ਦੇ ਕੈ ਚਉਕਾ ਕਢੀ ਕਾਰ ॥

day kai cha-ukaa kadhee kaar.

Baada ya kupaka sakafu ya jiko kwa samadi ya ng'ombe, wao huchora mstari wa mpaka kuizunguka.

ਉਪਰਿ ਆਇ ਬੈਠੇ ਕੂੜਿਆਰ ॥

upar aa-ay baithay koorhi-aar.

Kisha wabukuzi wanafiki huja na kuketi kwenye sakafu ya jikoni.

ਮਤੁ ਭਿਟੈ ਵੇ ਮਤੁ ਭਿਟੈ ॥ ਇਹੁ ਅੰਨੁ ਅਸਾਡਾ ਫਿਟੈ ॥

mat bhitai vay mat bhitai. ih ann asaadaa fitai.

Wao huwaambia wengine, msikuje karibu na jiko letu, isije chakula chetu kikawa najisi (kisichostahili kuliwa).

ਤਨਿ ਫਿਟੈ ਫੇੜ ਕਰੇਨਿ ॥

tan fitai fayrh karayn.

Lakini kwa uhalisia, watu wao hao wanajihusisha katika vitendo fisadi kwa miili yao michafu na kutenda maovu.

ਮਨਿ ਜੂਠੈ ਚੁਲੀ ਭਰੇਨਿ ॥

man joothai chulee bharayn.

Akili zao zimechafuka kwa maovu, lakini kwa nje wanasafisha mdomo wao kwa kusuza kutangaza utakatifu.

ਕਹੁ ਨਾਨਕ ਸਚੁ ਧਿਆਈਐ ॥

kaho naanak sach Dhi-aa-ee-ai.

Nanak anasema, kwa usafi wa kweli, tunafaa kutafakari kuhusu Mungu wa milele (kwa kufanya hivyo mtu anakuwa safi akilini na mwilini),

ਸੁਚਿ ਹੋਵੈ ਤਾ ਸਚੁ ਪਾਈਐ ॥੨॥

such hovai taa sach paa-ee-ai. ||2||

Mungu anagunduliwa wakati tu akili yetu ni safi (sio kwa kupaka samadi ya ng'ombe sakafuni na kuhusika katika vitendo fisadi).

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਚਿਤੈ ਅੰਦਰਿ ਸਭੁ ਕੋ ਵੇਖਿ ਨਦਰੀ ਹੇਠਿ ਚਲਾਇਦਾ ॥

chitai andar sabh ko vaykh nadree hayth chalaa-idaa.

Mungu anaweka kila mmoja katika akili Yake na anafanya wote watende kulingana na neema Yake.

ਆਪੇ ਦੇ ਵਡਿਆਈਆ ਆਪੇ ਹੀ ਕਰਮ ਕਰਾਇਦਾ ॥

aapay day vadi-aa-ee-aa aapay hee karam karaa-idaa.

Yeye Mwenyewe anatawaza staha, na Yeye Mwenyewe anawafanya watende vitendo tofauti.

ਵਡਹੁ ਵਡਾ ਵਡ ਮੇਦਨੀ ਸਿਰੇ ਸਿਰਿ ਧੰਧੈ ਲਾਇਦਾ ॥

vadahu vadaa vad maydnee siray sir DhanDhai laa-idaa.

Yeye ndiye mkuu zaidi kati ya wakuu; mkuu ni uumbaji Wake. Yeye anapatanisha wote kwa kazi zao.

ਨਦਰਿ ਉਪਠੀ ਜੇ ਕਰੇ ਸੁਲਤਾਨਾ ਘਾਹੁ ਕਰਾਇਦਾ ॥

nadar upthee jay karay sultaanaa ghaahu karaa-idaa.

Iwapo Yeye aondoe neema Yake, basi Yeye anaweza kufanya hata wafalme wawe maskini kama wakata nyasi.

ਦਰਿ ਮੰਗਨਿ ਭਿਖ ਨ ਪਾਇਦਾ ॥੧੬॥

dar mangan bhikh na paa-idaa. ||16||

Hakuna mtu anawapa matoleo hata wakati wanaenda kuomba omba kutoka mlango hadi mwingine.

ਸਲੋਕੁ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਜੇ ਮੋਹਾਕਾ ਘਰੁ ਮੁਹੈ ਘਰੁ ਮੁਹਿ ਪਿਤਰੀ ਦੇਇ ॥

jay mohaakaa ghar muhai ghar muhi pitree day-ay.

Iwapo mwizi apore nyumba na kutoa kwa hisani mali aliyoiba akiamini kwamba vitu hivyo vitapelekwa kwa wahenga wake walioaga dunia.

ਅਗੈ ਵਸਤੁ ਸਿਞਾਣੀਐ ਪਿਤਰੀ ਚੋਰ ਕਰੇਇ ॥

agai vasat sinjaanee-ai pitree chor karay-i.

Katika dunia itakayofuata, vitu hivyo vilivyoibwa vinatambuliwa. Kwa njia hii anafanya wahenga wake pia wawe wezi.

ਵਢੀਅਹਿ ਹਥ ਦਲਾਲ ਕੇ ਮੁਸਫੀ ਏਹ ਕਰੇਇ ॥

vadhee-ah hath dalaal kay musfee ayh karay-i.

Mikono ya mlanguzi (Brahmin) inakatwa; hii ndiyo haki ya hakimu wa haki.

ਨਾਨਕ ਅਗੈ ਸੋ ਮਿਲੈ ਜਿ ਖਟੇ ਘਾਲੇ ਦੇਇ ॥੧॥

naanak agai so milai je khatay ghaalay day-ay. ||1||

Ee Nanak, katika dunia itakayofuata, mtu anapokea tu kile ambacho mtu anachuma na kushiriki na maskini.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਜਿਉ ਜੋਰੂ ਸਿਰਨਾਵਣੀ ਆਵੈ ਵਾਰੋ ਵਾਰ ॥

ji-o joroo sirnaavanee aavai vaaro vaar.

Wakati mwanamke anapitia hedhi yake mwezi baada ya mwezi, (watu wanamfikiria kuwa najisi kimakosa),

ਜੂਠੇ ਜੂਠਾ ਮੁਖਿ ਵਸੈ ਨਿਤ ਨਿਤ ਹੋਇ ਖੁਆਰੁ ॥

joothay joothaa mukh vasai nit nit ho-ay khu-aar.

Najisi wa kweli ni wale ambao daima wanazungumza uongo na udanganyifu unazidi kudumu mdomoni mwao; wanazidi kuteseka kwa dhiki kila siku.

ਸੂਚੇ ਏਹਿ ਨ ਆਖੀਅਹਿ ਬਹਨਿ ਜਿ ਪਿੰਡਾ ਧੋਇ ॥

soochay ayhi na aakhee-ahi bahan je pindaa Dho-ay.

Wale wanaodhani wamekuwa safi kwa kusafisha miili yao tu hawaiwi safi.

ਸੂਚੇ ਸੇਈ ਨਾਨਕਾ ਜਿਨ ਮਨਿ ਵਸਿਆ ਸੋਇ ॥੨॥

soochay say-ee naankaa jin man vasi-aa so-ay. ||2||

Ee Nanak, walio safi kwa kweli ni wale ambao Mungu anaishi akilini mwao.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਤੁਰੇ ਪਲਾਣੇ ਪਉਣ ਵੇਗ ਹਰ ਰੰਗੀ ਹਰਮ ਸਵਾਰਿਆ ॥

turay palaanay pa-un vayg har rangee haram savaari-aa.

(wale ambao wana utajiri uliokithiri na) wana farasi wenye saruji, wanaokimbia upesi kama upepo, na wamepamba haremu zao kwa rangi nyingi,

ਕੋਠੇ ਮੰਡਪ ਮਾੜੀਆ ਲਾਇ ਬੈਠੇ ਕਰਿ ਪਾਸਾਰਿਆ ॥

kothay mandap maarhee-aa laa-ay baithay kar paasaari-aa.

Wale wanaoishi kwa fahari katika majumba na makasri yao ya kifahari wakifanya mwonyesho mkuu wa ubinafsi,

ਚੀਜ ਕਰਨਿ ਮਨਿ ਭਾਵਦੇ ਹਰਿ ਬੁਝਨਿ ਨਾਹੀ ਹਾਰਿਆ ॥

cheej karan man bhaavday har bujhan naahee haari-aa.

Wale wanaojihusisha katika kusherehekea hadi watosheleze mioyo yao lakini hawafikirii kuhusu Mungu, wakipoteza lengo la maisha yao.

ਕਰਿ ਫੁਰਮਾਇਸਿ ਖਾਇਆ ਵੇਖਿ ਮਹਲਤਿ ਮਰਣੁ ਵਿਸਾਰਿਆ ॥

kar furmaa-is khaa-i-aa vaykh mahlat maran visaari-aa.

Wale wanaokula vyakula vitamu wanavyotaka vilivyoandaliwa na watu maskini wanyonge; wanasahau kifo kinatazama majumba yao ya kifahari.

ਜਰੁ ਆਈ ਜੋਬਨਿ ਹਾਰਿਆ ॥੧੭॥

jar aa-ee joban haari-aa. ||17||

(Licha ya utajiri huo wote), wakati uzee wao unakuja, wanapoteza uzima wa ujana (na mwishowe wanakufa wakiacha nyuma utajiri wote)

ਸਲੋਕੁ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

**ਜੇ ਕਰਿ ਸੂਤਕੁ ਮੰਨੀਐ ਸਭ ਤੈ ਸੂਤਕੁ ਹੋਇ ॥**

jay kar sootak mannee-ai sabh tai sootak ho-ay.

Iwapo mtu akubali dhana ya unajisi, basi kuna unajisi kila mahali.

**ਗੋਹੇ ਅਤੈ ਲਕੜੀ ਅੰਦਰਿ ਕੀੜਾ ਹੋਇ ॥**

gohay atai lakrhee andar keerhaa ho-ay.

Katika samadi ya ng'ombe na mbao kuna minyoo.

**ਜੇਤੇ ਦਾਣੇ ਅੰਨ ਕੇ ਜੀਆ ਬਾਝੁ ਨ ਕੋਇ ॥**

jaytay daanay ann kay jee-aa baajh na ko-ay.

Kama zilizo nyingi nafaka za chakula, hakuna iliyo bila uhai.

**ਪਹਿਲਾ ਪਾਣੀ ਜੀਉ ਹੈ ਜਿਤੁ ਹਰਿਆ ਸਭੁ ਕੋਇ ॥**

pahilaa paanee jee-o hai jit hari-aa sabh ko-ay.

Kwanza, kuna uhai katika maji, ambayo kwa hiyo kila kitu kinapata uhai na kuwa mbichi.

**ਸੂਤਕੁ ਕਿਉ ਕਰਿ ਰਖੀਐ ਸੂਤਕੁ ਪਵੈ ਰਸੋਇ ॥**

sootak ki-o kar rakhee-ai sootak pavai raso-ay.

Tunawezaje kujilinda kutoka unajisi, kwa sababu unajisi huu daima upo hapo katika jikoni yetu?

**ਨਾਨਕ ਸੂਤਕੁ ਏਵ ਨ ਉਤਰੈ ਗਿਆਨੁ ਉਤਾਰੇ ਧੋਇ ॥੧॥**

naanak sootak ayv na utrai gi-aan utaaray Dho-ay. ||1||

Ee Nanak, unajisi hauwezi kuondolewa kwa itikadi hizi za uongo; unasafishwa tu kwa hekima ya kiroho.

**ਮਃ ੧ ॥**

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਮਨ ਕਾ ਸੂਤਕੁ ਲੋਭੁ ਹੈ ਜਿਹਵਾ ਸੂਤਕੁ ਕੂੜੁ ॥

man kaa sootak lobh hai jihvaa sootak koorh.

Unajisi wa akili ni tama, na unajisi wa ulimi ni udanganyifu.

ਅਖੀ ਸੂਤਕੁ ਵੇਖਣਾ ਪਰ ਤ੍ਰਿਅ ਪਰ ਧਨ ਰੂਪੁ ॥

akhee sootak vaykh-naa par tari-a par Dhan roop.

Unajisi wa macho ni kutazama urembo wa mke wa mwengine, na utajiri wake kwa nia mbaya.

ਕੰਨੀ ਸੂਤਕੁ ਕੰਨਿ ਪੈ ਲਾਇਤਬਾਰੀ ਖਾਹਿ ॥

kannee sootak kann pai laa-itbaaree khaahi.

Unajisi wa masikio ni kusikiliza uchongezi wa wengine.

ਨਾਨਕ ਹੰਸਾ ਆਦਮੀ ਬਧੇ ਜਮ ਪੁਰਿ ਜਾਹਿ ॥੨॥

naanak hansaa aadmee baDhay jam pur jaahi. ||2||

Ee Nanak, ni kwa sababu ya itikadi hizi za unajisi ambapo hata watu wazuri kama bata maji wanafungwa na kupelekwa jehanamu.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਸਭੋ ਸੂਤਕੁ ਭਰਮੁ ਹੈ ਦੂਜੈ ਲਗੈ ਜਾਇ ॥

sabho sootak bharam hai doojai lagai jaa-ay.

Unajisi wote unatoka kwa shaka na kiambatisho kwa uwili.

ਜੰਮਣੁ ਮਰਣਾ ਹੁਕਮੁ ਹੈ ਭਾਣੈ ਆਵੈ ਜਾਇ ॥

jaman marnaa hukam hai bhaanai aavai jaa-ay.

Uzao na mauti yanatii Amri Yake; kwa mapenzi ya Mungu tunakuja duniani humu na kuondoka kutoka humu.

ਖਾਣਾ ਪੀਣਾ ਪਵਿਤ੍ਰੁ ਹੈ ਦਿਤੋਨੁ ਰਿਜਕੁ ਸੰਬਾਹਿ ॥

khaanaa peenaa pavitar hai diton rijak sambaahi.

Kula na kunywa ni safi, kwani Mungu anatoa lishe kwa wote.

ਨਾਨਕ ਜਿਨ੍ੀ ਗੁਰਮੁਖਿ ਬੁਝਿਆ ਤਿਨ੍ਾ ਸੂਤਕੁ ਨਾਹਿ ॥੩॥

naanak jinHee gurmukh bujhi-aa tinHaa sootak naahi. ||3||

Ee Nanak, wale ambao kwa mafundisho ya Guru wameelewa dhana hii ya itikadi za uongo, kwao hakuna unajisi.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਸਤਿਗੁਰੁ ਵਡਾ ਕਰਿ ਸਾਲਾਹੀਐ ਜਿਸੁ ਵਿਚਿ ਵਡੀਆ ਵਡਿਆਈਆ ॥

satgur vadaa kar salaahee-ai jis vich vadee-aa vadi-aa-ee-aa.

Tunafaa kumsifu Guru wa Kweli tukimfikiria kuwa mkuu zaidi; ambaye ndani yake kuna fadhila kuu zaidi.

ਸਹਿ ਮੇਲੇ ਤਾ ਨਦਰੀ ਆਈਆ ॥

seh maylay taa nadree aa-ee-aa.

Mungu anapotufanya tukutane na Guru, basi tunakuja kuona fadhila hizi.

ਜਾ ਤਿਸੁ ਭਾਣਾ ਤਾ ਮਨਿ ਵਸਾਈਆ ॥

jaa tis bhaanaa taa man vasaa-ee-aa.

Inapompendeza Yeye, fadhila hizi huja kuishi katika akili zetu.

ਕਰਿ ਹੁਕਮੁ ਮਸਤਕਿ ਹਥੁ ਧਰਿ ਵਿਚਹੁ ਮਾਰਿ ਕਢੀਆ ਬੁਰਿਆਈਆ ॥

kar hukam mastak hath Dhar vichahu maar kadhee-aa buri-aa-ee-aa.

Akiwa mwenye huruma, Guru huondoa maovu kutoka kwa akili yetu.

ਸਹਿ ਤੁਠੈ ਨਉ ਨਿਧਿ ਪਾਈਆ ॥੧੮॥

seh tuthai na-o niDh paa-ee-aa. ||18||

Mungu anapopendezwa kabisa, hazina zote za maisha zinapatwa.

ਸਲੋਕੁ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਪਹਿਲਾ ਸੁਚਾ ਆਪਿ ਹੋਇ ਸੁਚੈ ਬੈਠਾ ਆਇ ॥

pahilaa suchaa aap ho-ay suchai baithaa aa-ay.

Kwanza kabisa, baada ya kuoga na kuosha mwili wake kwa makini na kuwa "safi", (Brahmin)huja na kuketi katika (jikoni ya mwenyeji wake) "iliyotakaswa".

ਸੁਚੇ ਅਗੈ ਰਖਿਓਨੁ ਕੋਇ ਨ ਭਿਟਿਓ ਜਾਇ ॥

suchay agai rakhi-on ko-ay na bhiti-o jaa-ay.

"chakula safi", ambacho hakuna mtu aliyekigusa mbeleni, kinawekwa mbele yake.

ਸੁਚਾ ਹੋਇ ਕੈ ਜੇਵਿਆ ਲਗਾ ਪੜਣਿ ਸਲੋਕੁ ॥

suchaa ho-ay kai jayvi-aa lagaa parhan salok.

Akiwa "ametakaswa", yeye hula chakula hiki, na kuanza kusoma mantra takatifu.

ਕੁਹਥੀ ਜਾਈ ਸਟਿਆ ਕਿਸੁ ਏਹੁ ਲਗਾ ਦੋਖੁ ॥

kuhthee jaa-ee sati-aa kis ayhu lagaa dokh.

Chakula hiki "safi" hutupwa mahali pachafu (tumbo), basi nani atabeba lawama ya kuchafua lishe safi kama hiyo?

ਅੰਨੁ ਦੇਵਤਾ ਪਾਣੀ ਦੇਵਤਾ ਬੈਸੰਤਰੁ ਦੇਵਤਾ ਲੂਣੁ ਪੰਜਵਾ ਪਾਇਆ ਘਿਰਤੁ ॥ ਤਾ ਹੋਆ ਪਾਕੁ ਪਵਿਤੁ ॥

ann dayvtaa paanee dayvtaa baisantar dayvtaa loon panjvaa paa-i-aa ghirat. taa ho-aa paak pavit.

(kulingana na itikadi ya Brahmin mwenyewe), nafaka ni safi, maji ni safi; moto na chumvi ni safi; wakati kitu cha tano safi, samli (siagi iliyosafishwa), kinapoongezwa, basi chakula "safi na kilichotakaswa" kinafikiriwa kuwa tayari kuliwa.

ਪਾਪੀ ਸਿਉ ਤਨੁ ਗਡਿਆ ਥੁਕਾ ਪਈਆ ਤਿਤੁ ॥

paapee si-o tan gadi-aa thukaa pa-ee-aa tit.

Wakati chakula hiki "safi" kinapoguswa na mwili wa binadamu wenye dhambi, chakula safi kinakuwa najisi mno (kinyesi cha mtu) hivi kwamba kinanuka na kinatemewa mate.

ਜਿਤੁ ਮੁਖਿ ਨਾਮੁ ਨ ਊਚਰਹਿ ਬਿਨੁ ਨਾਵੈ ਰਸ ਖਾਹਿ ॥

jit mukh naam na oochrahi bin naavai ras khaahi.

Vivyo hivyo, mdomo ambao hautamki Jina la Mungu na unakula chakula kitamu bila kumkumbuka Mungu,

ਨਾਨਕ ਏਵੈ ਜਾਣੀਐ ਤਿਤੁ ਮੁਖਿ ਥੁਕਾ ਪਾਹਿ ॥੧॥

naanak ayvai jaanee-ai tit mukh thukaa paahi. ||1||

Ee Nanak, fahamu hili, kwamba mdomo (mtu) kama huo unatemewa mate (kuaibishwa mbele za Mungu).

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa ੧.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਭੰਡਿ ਜੰਮੀਐ ਭੰਡਿ ਨਿੰਮੀਐ ਭੰਡਿ ਮੰਗਣੁ ਵੀਆਹੁ ॥

bhand jammee-ai bhand nimmee-ai bhand mangan vee-aahu.

Mwanaume anatungwa ndani mwa mwanamke na anazaliwa toka kwa mwanamke; kwa mwanamke anapata uchumba na kuolewa.

ਭੰਡਹੁ ਹੋਵੈ ਦੋਸਤੀ ਭੰਡਹੁ ਚਲੈ ਰਾਹੁ ॥

bhandahu hovai dostee bhandahu chalai raahu.

Mwanamke anakuwa rafiki yake; kupitia mwanamke, vizazi vyake huja.

ਭੰਡੁ ਮੁਆ ਭੰਡੁ ਭਾਲੀਐ ਭੰਡਿ ਹੋਵੈ ਬੰਧਾਨੁ ॥

bhand mu-aa bhand bhaalee-ai bhand hovai banDhaan.

Akifa mwanamke wake, yeye hutafuta mwanamke mwingine; ni kupitia kwa mwanamke ambapo tunapatanishwa na dunia.

ਸੋ ਕਿਉ ਮੰਦਾ ਆਖੀਐ ਜਿਤੁ ਜੰਮਹਿ ਰਾਜਾਨ ॥

so ki-o mandaa aakhee-ai jit jameh raajaan.

Tunawezaje kumuita huyo (mwanamke) mwovu, ambaye ametoa uhai kwa wafalme wote (malkia, watakatifu, na watu wengine wakuu).

ਭੰਡਹੁ ਹੀ ਭੰਡੁ ਊਪਜੈ ਭੰਡੈ ਬਾਝੁ ਨ ਕੋਇ ॥

bhandahu hee bhand oopjai bhandai baajh na ko-ay.

(kwa kweli) ni kutoka kwa mwanamke ambapo mwanamke mwengine anazaliwa na hakuna anayezaliwa pasipo mwanamke.

ਨਾਨਕ ਭੰਡੈ ਬਾਹਰਾ ਏਕੋ ਸਚਾ ਸੋਇ ॥

naanak bhandai baahraa ayko sachaa so-ay.

Ee Nanak, ni Mungu mmoja tu wa milele ambaye amekuwepo pasi (kupitia kwa chupa ya uzazi ya) mwanamke.

ਜਿਤੁ ਮੁਖਿ ਸਦਾ ਸਾਲਾਹੀਐ ਭਾਗਾ ਰਤੀ ਚਾਰਿ ॥

jit mukh sadaa salaahee-ai bhaagaa ratee chaar.

Wale ambao daima wanaimba sifa za Mungu, hubarikiwa na kuonekana wazuri mbele ya Mungu.

ਨਾਨਕ ਤੇ ਮੁਖ ਊਜਲੇ ਤਿਤੁ ਸਚੈ ਦਰਬਾਰਿ ॥੨॥

naanak tay mukh oojlay tit sachai darbaar. ||2||

Ee Nanak, nyuso zao zitang'aa katika Mahakama ya Mungu wa milele.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਸਭੁ ਕੋ ਆਖੈ ਆਪਣਾ ਜਿਸੁ ਨਾਹੀ ਸੋ ਚੁਣਿ ਕਢੀਐ ॥

sabh ko aakhai aapnaa jis naahee so chun kadhee-ai.

Kila mtu ana viambatisho vya kihisia duniani humu, tafuta (na unionyeshe) mmoja ambaye hana viambatisho vyovyote.

ਕੀਤਾ ਆਪੋ ਆਪਣਾ ਆਪੇ ਹੀ ਲੇਖਾ ਸੰਢੀਐ ॥

keetaa aapo aapnaa aapay hee laykhaa sandhee-ai.

(Mwishowe), kila mtu hustahimili matekeo ya vitendo vyake.

ਜਾ ਰਹਣਾ ਨਾਹੀ ਐਤੁ ਜਗਿ ਤਾ ਕਾਇਤੁ ਗਾਰਬਿ ਹੰਢੀਐ ॥

jaa rahnaa naahee ait jag taa kaa-it gaarab handhee-ai.

Wakati (tukijua kwamba) hatutabaki duniani humu milele, kwa nini tujiharibu kwa kiburi?

ਮੰਦਾ ਕਿਸੈ ਨ ਆਖੀਐ ਪੜਿ ਅਖਰੁ ਏਹੋ ਬੁਝੀਐ ॥ ਮੂਰਖੈ ਨਾਲਿ ਨ ਲੁਝੀਐ ॥੧੯॥

mandaa kisai na aakhee-ai parh akhar ayho bujhee-ai, moorkhai naal na lujhee-ai. ||19||

Baada ya kusoma maneno haya (mafundisho haya), tunapaswa kujifunza (funzo hili) kwamba hatufai kumuita yeyote mbaya, na hatufai kubishana na wapumbavu.

ਸਲੋਕੁ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਨਾਨਕ ਫਿਕੈ ਬੋਲਿਐ ਤਨੁ ਮਨੁ ਫਿਕਾ ਹੋਇ ॥

naanak fikai boli-ai tan man fikaa ho-ay.

Ee Nanak, yule ambaye daima anazungumza kwa kiburi, huwa mwenye kiburi.

ਫਿਕੋ ਫਿਕਾ ਸਦੀਐ ਫਿਕੇ ਫਿਕੀ ਸੋਇ ॥

fiko fikaa sadee-ai fikay fikee so

Yeye huitwa mwenye na wote na ndivyo huwa sifa yake.

ਫਿਕਾ ਦਰਗਹ ਸਟੀਐ ਮੁਹਿ ਥੁਕਾ ਫਿਕੇ ਪਾਇ ॥

fikaa dargeh satee-ai muhi thukaa fikay paa

Mwenye kiburi anafedheheshwa, naye hakubaliki katika mahakama ya Mungu.

ਫਿਕਾ ਮੂਰਖੁ ਆਖੀਐ ਪਾਣਾ ਲਹੈ ਸਜਾਇ ॥੧॥

fikaa moorakh aakhee-ai paanaa lahai sajaa-ay. ||1||

Mtu kiburi huitwa mpumbavu naye anafedheheshwa kila mahali.

ਮਃ ੧ ॥

mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਅੰਦਰਹੁ ਝੂਠੇ ਪੈਜ ਬਾਹਰਿ ਦੁਨੀਆ ਅੰਦਰਿ ਫੈਲੁ ॥

andrahu jhoothay paij baahar dunee-aa andar fail.

Katika dunia hii kuna watu wengi ambao kindani ni waongo, lakini kinje wameweza kujizolea staha yao.

ਅਠਸਠਿ ਤੀਰਥ ਜੇ ਨਾਵਹਿ ਉਤਰੈ ਨਾਹੀ ਮੈਲੁ ॥

athsath tirath jay naaveh utrai naahee mail.

Hata iwapo wanaweza kuoga katika ziara sitini na nane takatifu za hija, bado uchafu wa maovu kutoka akilini mwao hauondoki.

ਜਿਨ੍ ਪਟੁ ਅੰਦਰਿ ਬਾਹਰਿ ਗੁਦੜੁ ਤੇ ਭਲੇ ਸੰਸਾਰਿ ॥

jin[H] pat andar baahar gudarh tay bhalay sansaar.

Wale ambao wana ukarimu na wema ndani yao lakini wanaweza kuonekana wenye kiburi kinje, ndio watu wema duniani.

ਤਿਨ੍ ਨੇਹੁ ਲਗਾ ਰਬ ਸੇਤੀ ਦੇਖਨ੍ੇ ਵੀਚਾਰਿ ॥

tin[H] nayhu lagaa rab saytee daykhn[H]ay veechaar.

Wao hukumbatia upendo kwa Mungu, na kutafakari kumtazama Yeye.

ਰੰਗਿ ਹਸਹਿ ਰੰਗਿ ਰੋਵਹਿ ਚੁਪ ਭੀ ਕਰਿ ਜਾਹਿ ॥

rang haseh rang roveh chup bhee kar jaahi.

Katika Upendo wa Mungu, wanacheka, na katika Upendo wa Mungu, wanalia, na pia wanakaa kimya.

ਪਰਵਾਹ ਨਾਹੀ ਕਿਸੈ ਕੇਰੀ ਬਾਝੁ ਸਚੇ ਨਾਹ ॥

parvaah naahee kisai kayree baajh sachay naah.

Wao hawamtegemei yeyote mwingine, isipokuwa Bwana wao wa Kweli.

ਦਰਿ ਵਾਟ ਉਪਰਿ ਖਰਚੁ ਮੰਗਾ ਜਬੈ ਦੇਇ ਤ ਖਾਹਿ ॥

dar vaat upar kharach mangaa jabai day-ay ta khaahi.

Wao huulizia Naam kama chakula cha roho yao, na akiwapa wanaishiriki.

ਦੀਬਾਨੁ ਏਕੋ ਕਲਮ ਏਕਾ ਹਮਾ ਤੁਮ੍ਹਾ ਮੇਲੁ ॥

deebaan ayko kalam aykaa hamaa tum$^{H}$aa mayl.

Kuna hakimu mmoja tu na mfumo mmoja wa haki kwa kila mmoja na watu wote wenye vitendo vizuri au vibaya mwishowe hukutana katika mahakama Yake.

ਦਰਿ ਲਏ ਲੇਖਾ ਪੀੜਿ ਛੁਟੈ ਨਾਨਕਾ ਜਿਉ ਤੇਲੁ ॥੨॥

dar la-ay laykhaa peerh chhutai naankaa ji-o tayl. ||2||

Ee Nanak, katika mahakama ya Mungu, akaunti ya kila mmoja inachunguzwa na watenda dhambi huadhibiwa vikali kama mbegu za mafuta zinavyopondwa katika shinikizo la mafuta.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਆਪੇ ਹੀ ਕਰਣਾ ਕੀਓ ਕਲ ਆਪੇ ਹੀ ਤੈ ਧਾਰੀਐ ॥

aapay hee karnaa kee-o kal aapay hee tai Dhaaree-ai.

Ee Mungu, Wewe Mwenyewe umeumba uumbaji, na Wewe Mwenyewe umeweka nguvu Yako ndani yake.

ਦੇਖਹਿ ਕੀਤਾ ਆਪਣਾ ਧਰਿ ਕਚੀ ਪਕੀ ਸਾਰੀਐ ॥

daykheh keetaa aapnaa Dhar kachee pakee saaree-ai.

Wewe unatazama uumbaji Wako kama mchezo wa ubao na kuamua ni vipande (binadamu) vipi ni vya kweli (ambao wametimiza kusudi lao la maisha ya kibinadamu) na vipi ni vya uongo.

ਜੋ ਆਇਆ ਸੋ ਚਲਸੀ ਸਭੁ ਕੋਈ ਆਈ ਵਾਰੀਐ ॥

jo aa-i-aa so chalsee sabh ko-ee aa-ee vaaree-ai.

Yeyote aliyekuja duniani humu, ataondoka; wote watakuwa na wakati wao.

ਜਿਸ ਕੇ ਜੀਅ ਪਰਾਣ ਹਹਿ ਕਿਉ ਸਾਹਿਬੁ ਮਨਹੁ ਵਿਸਾਰੀਐ ॥

jis kay jee-a paraan heh ki-o saahib manhu visaaree-ai

Yeye anayemiliki roho yetu, na pumzi yetu ya uhai – kwa nini tumsahau Bwana Huyo kutoka akilini mwetu?

ਆਪਣ ਹਥੀ ਆਪਣਾ ਆਪੇ ਹੀ ਕਾਜੁ ਸਵਾਰੀਐ ॥੨੦॥

aapan hathee aapnaa aapay hee kaaj savaaree-ai. ||20||

Tunafaa kufanikisha kazi yetu ya kuungana na Mungu wenyewe, kwa kutafakari kuhusu Jina Lake.

ਸਲੋਕੁ ਮਹਲਾ ੨ ॥

salok mehlaa 2.

Salok, na Guru wa Pili:

ਏਹ ਕਿਨੇਹੀ ਆਸਕੀ ਦੂਜੈ ਲਗੈ ਜਾਇ ॥

ayh kinayhee aaskee doojai lagai jaa-ay.

Huu ni upendo wa aina gani, ambao unakwama kwa uwili (kumpenda mwengine ila Mungu)?

ਨਾਨਕ ਆਸਕੁ ਕਾਂਢੀਐ ਸਦ ਹੀ ਰਹੈ ਸਮਾਇ ॥
naanak aasak kaa^N^dhee-ai sad hee rahai samaa-ay.
Ee Nanak, yeye tu anafikiriwa kuwa mpenzi wa kweli, anayesalia kuzama katika upendo wa mpendwa (Mungu) wake milele.

ਚੰਗੈ ਚੰਗਾ ਕਰਿ ਮੰਨੇ ਮੰਦੈ ਮੰਦਾ ਹੋਇ ॥
changai changa kar mannay mandai mandaa ho-ay.
Lakini yule anayefurahia wakati tu vitu vizuri vinatendeka, na kukataa wakati vitu vinatendeka vibaya,

ਆਸਕੁ ਏਹੁ ਨ ਆਖੀਐ ਜਿ ਲੇਖੈ ਵਰਤੈ ਸੋਇ ॥੧॥
aasak ayhu na aakhee-ai je laykhai vartai so-ay. ||1||
Hastahili kuitwa mpendwa wa kweli wa Mungu, kwani yeye anahusiana na Mungu kwa mtindo wa kibishara.

ਮਹਲਾ ੨ ॥
mehlaa 2.
Salok, Guru wa Pili:

ਸਲਾਮੁ ਜਬਾਬੁ ਦੋਵੈ ਕਰੇ ਮੁੰਢਹੁ ਘੁਥਾ ਜਾਇ ॥
salaam jabaab dovai karay mundhhu ghuthaa jaa-ay.
Yule anayetoa salamu za heshima na kumkataa kwa kiburi Bwana wake, anapotoka kimsingi kutoka mwanzo.

ਨਾਨਕ ਦੋਵੈ ਕੂੜੀਆ ਥਾਇ ਨ ਕਾਈ ਪਾਇ ॥੨॥
naanak dovai koorhee-aa thaa-ay na kaa-ee paa-ay. ||2||
Ee Nanak, tabia hizi mbili sio za kweli, na hazikubaliki katika mahakama ya Mungu.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਜਿਤੁ ਸੇਵਿਐ ਸੁਖੁ ਪਾਈਐ ਸੋ ਸਾਹਿਬੁ ਸਦਾ ਸਮ੍ਹਾਲੀਐ ॥

jit sayvi-ai sukh paa-ee-ai so saahib sadaa sam$^{H}$aalee-ai.

Kumtafakari ambaye kwake amani inapatikana; Bwana huyo daima anafaa kukumbukwa.

ਜਿਤੁ ਕੀਤਾ ਪਾਈਐ ਆਪਣਾ ਸਾ ਘਾਲ ਬੁਰੀ ਕਿਉ ਘਾਲੀਐ ॥

jit keetaa paa-ee-ai aapnaa saa ghaal buree ki-o ghaalee-ai.

Tukifahamu kwamba ni sharti tuhimili matokeo ya vitendo vyetu, basi kwa nini tutende vitendo viovu?

ਮੰਦਾ ਮੂਲਿ ਨ ਕੀਚਈ ਦੇ ਲੰਮੀ ਨਦਰਿ ਨਿਹਾਲੀਐ ॥

mandaa mool na keech-ee day lammee nadar nihaalee-ai.

Hatufai kufanya uovu wowote hata kidogo; tunafaa kufikiria matokeo yake kwanza.

ਜਿਉ ਸਾਹਿਬ ਨਾਲਿ ਨ ਹਾਰੀਐ ਤੇਵੇਹਾ ਪਾਸਾ ਢਾਲੀਐ ॥

ji-o saahib naal na haaree-ai tavayhaa paasaa dhaalee-ai.

Tunafaa kuucheza mchezo wa maisha kwa njia ambayo hatutafikirwa kuwa washindwa mbele ya Bwana wetu.

ਕਿਛੁ ਲਾਹੇ ਉਪਰਿ ਘਾਲੀਐ ॥੨੧॥

kichh laahay upar ghaalee-ai. ||21||

(kwa maisha haya ya kibinadamu yenye thamani), tunafaa kufanya vitendo ambavyo vitatuletea staha katika mahakama ya Mungu.

ਸਲੋਕੁ ਮਹਲਾ ੨ ॥

salok mehlaa 2.

Salok, Guru wa Pili:

ਚਾਕਰੁ ਲਗੈ ਚਾਕਰੀ ਨਾਲੇ ਗਾਰਬੁ ਵਾਦੁ ॥

chaakar lagai chaakree naalay gaarab vaad.

Iwapo mtumishi atafanya huduma, kwa ubinafsi na mabishano,

ਗਲਾ ਕਰੇ ਘਣੇਰੀਆ ਖਸਮ ਨ ਪਾਏ ਸਾਦੁ ॥

galaa karay ghanayree-aa khasam na paa-ay saad.

Yeye anaweza kuzungumza kiasi anachotaka, lakini hatakuwa wa kupendeza kwa Bwana wake.

ਆਪੁ ਗਵਾਇ ਸੇਵਾ ਕਰੇ ਤਾ ਕਿਛੁ ਪਾਏ ਮਾਨੁ ॥

aap gavaa-ay sayvaa karay taa kichh paa-ay maan.

Lakini iwapo atatumika bila ya ubinafsi, basi yeye anapata utambuzi.

ਨਾਨਕ ਜਿਸ ਨੋ ਲਗਾ ਤਿਸੁ ਮਿਲੈ ਲਗਾ ਸੋ ਪਰਵਾਨੁ ॥੧॥

naanak jis no lagaa tis milai lagaa so parvaan. ||1||

Ee Nanak, iwapo yeye ataunganishwa na yule ambaye ameambatishwa, kiambatisho chake kinakubalika.

ਮਹਲਾ ੨ ॥

mehlaa 2.

Salok, Guru wa Pili:

ਜੋ ਜੀਇ ਹੋਇ ਸੁ ਉਗਵੈ ਮੁਹ ਕਾ ਕਹਿਆ ਵਾਉ ॥

jo jee-ay ho-ay so ugvai muh kaa kahi-aa vaa-o.

Chochote kilicho akilini kinakuwa dhahiri usoni; maneno yanayozungumzwa tu yanaweza kuwa usemi wa uongo.

**ਬੀਜੇ ਬਿਖੁ ਮੰਗੈ ਅੰਮ੍ਰਿਤੁ ਵੇਖਹੁ ਏਹੁ ਨਿਆਉ ॥੨॥**

beejay bikh mangai amrit vaykhhu ayhu ni-aa-o. ||2||

Tazama aina ya haki mtu anayoitarajia, kwamba anapanda sumu, lakini anaulizia Nekta kama mavuno? (kutenda vitendo vibaya na kutarajia matokeo mazuri).

**ਮਹਲਾ ੨ ॥**

mehlaa 2.

Salok, Guru wa Pili:

**ਨਾਲਿ ਇਆਣੇ ਦੋਸਤੀ ਕਦੇ ਨ ਆਵੈ ਰਾਸਿ ॥**

naal i-aanay dostee kaday na aavai raas.

Urafiki na mtu mwenye akili ambazo hazijakomaa kamwe haufaulu.

**ਜੇਹਾ ਜਾਣੈ ਤੇਹੋ ਵਰਤੈ ਵੇਖਹੁ ਕੋ ਨਿਰਜਾਸਿ ॥**

jayhaa jaanai tayho vartai vaykhhu ko nirjaas.

Kama ajuavyo, yeye hutenda; yeyote anaweza kujijaribia hili mwenyewe.

**ਵਸਤੂ ਅੰਦਰਿ ਵਸਤੁ ਸਮਾਵੈ ਦੂਜੀ ਹੋਵੈ ਪਾਸਿ ॥**

vastoo andar vasat samaavai doojee hovai paas.

Kitu kimoja kinaweza kuzamishwa ndani ya kitu kingine iwapo tu kilicho ndani yake kwanza kiwekwe kando (vivyo hivyo, mtu anaweza tu kuthamini Mungu moyoni iwapo kwanza ataondoa ubinafsi na maovu akilini)

**ਸਾਹਿਬ ਸੇਤੀ ਹੁਕਮੁ ਨ ਚਲੈ ਕਹੀ ਬਣੈ ਅਰਦਾਸਿ ॥**

saahib saytee hukam na chalai kahee banai ardaas.

Sio amri, bali ombi nyenyekevu, ambalo hufanya kazi na Bwana.

**ਕੂੜਿ ਕਮਾਣੈ ਕੂੜੋ ਹੋਵੈ ਨਾਨਕ ਸਿਫਤਿ ਵਿਗਾਸਿ ॥੩॥**

koorh kamaanai koorho hovai naanak sifat vigaas. ||3||

Ee Nanak, tokeo la kutenda udanganyifu ni udanganyifu, sifa ya Mungu pekee,

ndiyo huleta furaha.

ਮਹਲਾ ੨ ॥

mehlaa 2.

Salok, Guru wa Pili:

ਨਾਲਿ ਇਆਣੇ ਦੋਸਤੀ ਵਡਾਰੂ ਸਿਉ ਨੇਹੁ ॥

naal i-aanay dostee vadaaroo si-o nayhu.

Urafiki na mtu ambaye hajakomaa, na upendo na mtu fidhuli

ਪਾਣੀ ਅੰਦਰਿ ਲੀਕ ਜਿਉ ਤਿਸ ਦਾ ਥਾਉ ਨ ਥੇਹੁ ॥੪॥

paanee andar leek ji-o tis daa thaa-o na thayhu. ||4||

Ni kama mistari iliyochorwa majini, isiyoacha alama yoyote.

ਮਹਲਾ ੨ ॥

mehlaa 2.

Salok, Guru wa Pili:

ਹੋਇ ਇਆਣਾ ਕਰੇ ਕੰਮੁ ਆਣਿ ਨ ਸਕੈ ਰਾਸਿ ॥

ho-ay i-aanaa karay kamm aan na sakai raas.

Iwapo mtu ambaye hajakomaa afanye kazi, yeye hawezi kuifanya vizuri.

ਜੇ ਇਕ ਅਧ ਚੰਗੀ ਕਰੇ ਦੂਜੀ ਭੀ ਵੇਰਾਸਿ ॥੫॥

jay ik aDh changee karay doojee bhee vayraas. ||5||

Hata akifanya kitu vizuri, yeye atafanya kitu kitakachofuata vibaya.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਚਾਕਰੁ ਲਗੈ ਚਾਕਰੀ ਜੇ ਚਲੈ ਖਸਮੈ ਭਾਇ ॥

chaakar lagai chaakree jay chalai khasmai bhaa-ay.

Iwapo mtumishi, wakati anatoa huduma, atii Mapenzi ya Bwana wake,

ਹੁਰਮਤਿ ਤਿਸ ਨੋ ਅਗਲੀ ਓਹੁ ਵਜਹੁ ਭਿ ਦੂਣਾ ਖਾਇ ॥

hurmat tis no aglee oh vajahu bhe doonaa khaa-ay.

Staha yake huongezeka, na anapokea thawabu mara dufu.

ਖਸਮੈ ਕਰੇ ਬਰਾਬਰੀ ਫਿਰਿ ਗੈਰਤਿ ਅੰਦਰਿ ਪਾਇ ॥

khasmai karay baraabaree fir gairat andar paa-ay.

Lakini akijifanya kuwa sawa na Bwana wake, yeye anapata ghadhabu ya Bwana wake.

ਵਜਹੁ ਗਵਾਏ ਅਗਲਾ ਮੁਹੇ ਮੁਹਿ ਪਾਣਾ ਖਾਇ ॥

vajahu gavaa-ay aglaa muhay muhi paanaa khaa-ay.

Yeye hupoteza hata mapato aliyochuma (thawabu), na kupata aibu.

ਜਿਸ ਦਾ ਦਿਤਾ ਖਾਵਣਾ ਤਿਸੁ ਕਹੀਐ ਸਾਬਾਸਿ ॥

jis daa ditaa khaavnaa tis kahee-ai saabaas.

Hivyo basi, tumpongeze Mungu, ambaye tunapokea lishe yetu kutoka kwake.

ਨਾਨਕ ਹੁਕਮੁ ਨ ਚਲਈ ਨਾਲਿ ਖਸਮ ਚਲੈ ਅਰਦਾਸਿ ॥੨੨॥

naanak hukam na chal-ee naal khasam chalai ardaas. ||22||

Ee Nanak, siyo amri, bali ombi nyenyekevu linalofanya kazi na Bwana.

ਸਲੋਕੁ ਮਹਲਾ ੨ ॥

salok mehlaa 2.

Salok, Guru wa Pili:

ਏਹ ਕਿਨੇਹੀ ਦਾਤਿ ਆਪਸ ਤੇ ਜੋ ਪਾਈਐ ॥

ayh kinayhee daat aapas tay jo paa-ee-ai.

ni aina gani hiyo ya thawabu iwapo tutadai kwamba tuliipata kwa jitihada yetu wenyewe?

ਨਾਨਕ ਸਾ ਕਰਮਾਤਿ ਸਾਹਿਬ ਤੁਠੈ ਜੋ ਮਿਲੈ ॥੧॥

naanak saa karmaat saahib tuthai jo milai. ||1||

Ee Nanak, hiyo ni thawabu bora zaidi, inayopokelewa kutoka kwa Mungu, wakati Yeye amependezwa kabisa.

ਮਹਲਾ ੨ ॥

mehlaa 2.

Salok, Guru wa Pili:

ਏਹ ਕਿਨੇਹੀ ਚਾਕਰੀ ਜਿਤੁ ਭਉ ਖਸਮ ਨ ਜਾਇ ॥

ayh kinayhee chaakree jit bha-o khasam na jaa-ay.

Hii ni huduma ya aina gani, ambayo kwake hofu ya Bwana haiondoki?

ਨਾਨਕ ਸੇਵਕੁ ਕਾਢੀਐ ਜਿ ਸੇਤੀ ਖਸਮ ਸਮਾਇ ॥੨॥

naanak sayvak kaadhee-ai je saytee khasam samaa-ay. ||2||

Ee Nanak, yeye tu anaitwa mtumishi wa kweli anayeungana na kuwa kitu kimoja na Bwana (Mungu).

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਨਾਨਕ ਅੰਤ ਨ ਜਾਪਨ੍ਹ੍ਹੀ ਹਰਿ ਤਾ ਕੇ ਪਾਰਾਵਾਰ ॥

naanak ant na jaapn[H]ee har taa kay paaraavaar.

Ee Nanak, vikomo vya Mungu haviwezi kujulikana; Yeye hana mwisho wala upungufu.

ਆਪਿ ਕਰਾਏ ਸਾਖਤੀ ਫਿਰਿ ਆਪਿ ਕਰਾਏ ਮਾਰ ॥

aap karaa-ay saakh-tee fir aap karaa-ay maar.

Yeye Mwenyewe huumba, na kisha Yeye Mwenyewe huangamiza.

ਇਕਨ੍ਹਾ ਗਲੀ ਜੰਜੀਰੀਆ ਇਕਿ ਤੁਰੀ ਚੜਹਿ ਬਿਸੀਆਰ ॥

iknHaa galee janjeeree-aa ik turee charheh bisee-aar.

Wengine wanafanya kazi kama watumwa, kana kwamba wana minyororo kwenye shingo zao, wakati wengine ni wakwasi mno, wanaendesha farasi wenye kasi.

ਆਪਿ ਕਰਾਏ ਕਰੇ ਆਪਿ ਹਉ ਕੈ ਸਿਉ ਕਰੀ ਪੁਕਾਰ ॥

aap karaa-ay karay aap ha-o kai si-o karee pukaar.

Yeye Mwenyewe hutenda, na Yeye Mwenyewe anatufanya tutende. Ninafaa kumlalamikia nani?

ਨਾਨਕ ਕਰਣਾ ਜਿਨਿ ਕੀਆ ਫਿਰਿ ਤਿਸ ਹੀ ਕਰਣੀ ਸਾਰ ॥੨੩॥

naanak karnaa jin kee-aa fir tis hee karnee saar. ||23||

Ee Nanak, yule Mmoja aliyefanya uumbaji – Yeye Mwenyewe anauchunga.

ਸਲੋਕੁ ਮਃ ੧ ॥

salok mehlaa 1.

Salok, Guru wa Kwanza:

ਆਪੇ ਭਾਂਡੇ ਸਾਜਿਅਨੁ ਆਪੇ ਪੂਰਣੁ ਦੇਇ ॥

aapay bhaaNday saaji-an aapay pooran day-ay.

Mungu Mwenyewe huumba miili ya binadamu na Yeye Mwenyewe hutawaza amani au mateso kwao.

ਇਕਨੑੀ ਦੁਧੁ ਸਮਾਈਐ ਇਕਿ ਚੁਲੑੈ ਰਹਨਿੑ ਚੜੇ ॥

ikn$^{H}$ee duDh samaa-ee-ai ik chul$^{H}$ai rehni$^{H}$ charhay.

Katika hatima za wengine, Yeye huandika starehe zote, wakati wengine wanahukumiwa kuteseka kwa uchungu.

ਇਕਿ ਨਿਹਾਲੀ ਪੈ ਸਵਨਿੑ ਇਕਿ ਉਪਰਿ ਰਹਨਿ ਖੜੇ ॥

ik nihaalee pai savni$^{H}$ ik upar rahan kharhay.

Wengine wanatulia na kulala kwenye vitanda laini, ilhali wengine husimama kando yao kama walinzi wao.

ਤਿਨੑਾ ਸਵਾਰੇ ਨਾਨਕਾ ਜਿਨੑ ਕਉ ਨਦਰਿ ਕਰੇ ॥੧॥

tin$^{H}$aa savaaray naankaa jin$^{H}$ ka-o nadar karay. ||1||

Ee Nanak, Yeye hupamaba tu maisha ya wale, ambao Yeye huwatupia jicho la Neema.

ਮਹਲਾ ੨ ॥

mehlaa 2.

Salok, Guru wa Pili:

ਆਪੇ ਸਾਜੇ ਕਰੇ ਆਪਿ ਜਾਈ ਭਿ ਰਖੈ ਆਪਿ ॥

aapay saajay karay aap jaa-ee bhe rakhai aap.

Yeye Mwenyewe anaumba na kutengeneza dunia, na Yeye Mwenyewe huipea taratibu.

ਤਿਸੁ ਵਿਚਿ ਜੰਤ ਉਪਾਇ ਕੈ ਦੇਖੈ ਥਾਪਿ ਉਥਾਪਿ ॥

tis vich jant upaa-ay kai daykhai thaap uthaap.

Akiwa ameumba viumbe walio ndani yake, Yeye anasimamia ukuzi na uangamizi wao.

ਕਿਸ ਨੋ ਕਹੀਐ ਨਾਨਕਾ ਸਭੁ ਕਿਛੁ ਆਪੇ ਆਪਿ ॥੨॥

kis no kahee-ai naankaa sabh kichh aapay aap. ||2||

Ee Nanak, tunaweza kumuelezea nani kuhusu hili. Yeye Mwenyewe ndiye msingi na mtendaji wa vyote.

ਪਉੜੀ ॥

pa-orhee.

Pauree:

ਵਡੇ ਕੀਆ ਵਡਿਆਈਆ ਕਿਛੁ ਕਹਣਾ ਕਹਣੁ ਨ ਜਾਇ ॥

vaday kee-aa vadi-aa-ee-aa kichh kahnaa kahan na jaa-ay.

Hakuna kinachoweza kusemwa kuhusu ukuu wa Mkuu (Mungu).

ਸੋ ਕਰਤਾ ਕਾਦਰ ਕਰੀਮੁ ਦੇ ਜੀਆ ਰਿਜਕੁ ਸੰਬਾਹਿ ॥

so kartaa kaadar kareem day jee-aa rijak sambaahi.

Yeye ndiye Muumba, mwenye nguvu zote na mkarimu; Yeye hutoa lishe kwa viumbe vyote.

ਸਾਈ ਕਾਰ ਕਮਾਵਣੀ ਧੁਰਿ ਛੋਡੀ ਤਿੰਨੈ ਪਾਇ ॥

saa-ee kaar kamaavnee Dhur chhodee tinnai paa-ay.

Viumbe hawa hufanya yale yaliyopangwa na Mungu tokea mwanzo.

ਨਾਨਕ ਏਕੀ ਬਾਹਰੀ ਹੋਰ ਦੂਜੀ ਨਾਹੀ ਜਾਇ ॥

naanak aykee baahree hor doojee naahee jaa-ay.

Ee Nanak, isipokuwa msaada wa Mungu, hakuna tegemeo lingine kwa kiumbe.

ਸੋ ਕਰੇ ਜਿ ਤਿਸੈ ਰਜਾਇ ॥੨੪॥੧॥ ਸੁਧੁ

so karay je tisai rajaa-ay. ||24||1|| suDhu

Yeye hutenda chochote anachotaka.

# ਅਰਦਾਸ

Prayer

ੴ ਵਾਹਿਗੁਰੂ ਜੀ ਕੀ ਫ਼ਤਹਿ॥

Mungu ni Mmoja. Ushindi wote ni wa Guru wa Ajabu (Mungu).

ਸ੍ਰੀ ਭਗੌਤੀ ਜੀ ਸਹਾਇ।

Upanga unaoheshimika (Mungu katika sura ya Mwangamizi wa watenda mabaya) utusaidie !

ਵਾਰ ਸ੍ਰੀ ਭਗੌਤੀ ਜੀ ਕੀ ਪਾਤਸ਼ਾਹੀ ||੧੦||

Ushairi wa upanga unaoheshimiwa uliokaririwa na Guru wa Kumi.

ਪ੍ਰਿਥਮ ਭਗੌਤੀ ਸਿਮਰਿ ਕੈ ਗੁਰ ਨਾਨਕ ਲਈਂ ਧਿਆਇ॥

Kwanza kumbuka upanga (Mungu katika sura ya Mwangamizi wa watenda mabaya); basi mkumbuke Nanak (kaa juu ya mchango wake wa kiroho).

ਫਿਰ ਅੰਗਦ ਗੁਰ ਤੇ ਅਮਰਦਾਸੁ ਰਾਮਦਾਸੈ ਹੋਈਂ ਸਹਾਇ॥

Kisha kumbuka na kutafakari kuhusu Guru Angad, Guru Amar Das na Guru Ram Das; Na watusaidie ! (kaa juu ya mchango wao wa kiroho)

ਅਰਜਨ ਹਰਗੋਬਿੰਦ ਨੋ ਸਿਮਰੌਂ ਸ੍ਰੀ ਹਰਿਰਾਇ॥

Kumbuka na kutafakari Guru Arjan, Guru Hargobind na Guru Har Rai Anayeheshimiwa. (kaa juu ya mchango wao wa kiroho)

ਸ੍ਰੀ ਹਰਿਕ੍ਰਿਸ਼ਨ ਧਿਆਈਐ ਜਿਸ ਡਿਠੈ ਸਭਿ ਦੁਖ ਜਾਇ॥

Kumbuka na kutafakari juu ya Guru Har Krishan anayeheshimiwa, ambaye kwa kumwona, maumivu yote hutoweka. (Zingatia mchango wao wa kiroho.

ਤੇਗ ਬਹਾਦਰ ਸਿਮਰਿਐ ਘਰ ਨਉ ਨਿਧਿ ਆਵੈ ਧਾਇ॥

Kumbuka Guru Tegh Bahadur na hapo ndipo vyanzo tisa vya utajiri wa kiroho vitakuja kwa haraka nyumbani kwako.

ਸਭ ਥਾਂਈ ਹੋਇ ਸਹਾਇ॥

Ee Mungu! tusaidie kila mahali kwa kutuonyesha njia.

ਦਸਵਾਂ ਪਾਤਸ਼ਾਹ ਸ੍ਰੀ ਗੁਰੂ ਗੋਬਿੰਦ ਸਿੰਘ ਸਾਹਿਬ ਜੀ! ਸਭ ਥਾਂਈ ਹੋਇ ਸਹਾਇ॥

Kumbuka Guru Gobind Singh wa Kumi anayeheshimiwa (kaa juu ya mchango wake wa kiroho). Ee Mungu! tusaidie kila mahali kwa kutuonyesha njia.

ਦਸਾਂ ਪਾਤਸ਼ਾਹੀਆਂ ਦੀ ਜੋਤ ਸ੍ਰੀ ਗੁਰੂ ਗ੍ਰੰਥ ਸਾਹਿਬ ਜੀ ਦੇ ਪਾਠ ਦੀਦਾਰ ਦਾ ਧਿਆਨ ਧਰ ਕੇ ਬੋਲੋ ਜੀ ਵਾਹਿਗੁਰੂ!

Fikiri na utafakari juu ya nuru ya kimungu ya Wafalme Kumi iliyomo katika Guru Granth Sahib inayoheshimika na ugeuze mawazo yako kwa mafundisho ya kimungu yake na upate radhi kwa kuona Guru Granth Sahib; Tamka Wahe Guru (Mungu wa Ajabu)!

ਪੰਜਾਂ ਪਿਆਰਿਆਂ, ਚੌਹਾਂ ਸਾਹਿਬਜ਼ਾਦਿਆਂ, ਚਾਲ੍ਹੀਆਂ ਮੁਕਤਿਆਂ, ਹਠੀਆਂ ਜਪੀਆਂ, ਤਪੀਆਂ,
ਜਿਨ੍ਹਾਂ ਨਾਮ ਜਪਿਆ, ਵੰਡ ਛਕਿਆ, ਦੇਗ ਚਲਾਈ, ਤੇਗ ਵਾਹੀ, ਦੇਖ ਕੇ ਅਣਡਿੱਠ ਕੀਤਾ,
ਤਿਨ੍ਹਾਂ ਪਿਆਰਿਆਂ, ਸਚਿਆਰਿਆਂ ਦੀ ਕਮਾਈ ਦਾ ਧਿਆਨ ਧਰ ਕੇ, ਖਾਲਸਾ ਜੀ ! ਬੋਲੋ ਜੀ ਵਾਹਿਗੁਰੂ!

Fikiria matendo ya Wapendwa Watano, ya wana wanne (wa Guru Gobind Singh); ya Mashahidi Arobaini; ya Masingasinga jasiri wa azimio lisiloweza kushindwa; ya waja waliozama katika rangi ya Naam; ya wale

walioingizwa katika Naam; ya wale waliomkumbuka Naam na kushiriki chakula chao katika urafiki; ya wale ambao walianza jikoni bure; ya wale walioshika panga zao (kwa ajili ya kuhifadhi haki); ya wale waliopuuza mapungufu ya wengine; Wote waliotajwa hapo juu walikuwa safi na waliojitolea kweli; Tamka Wahe Guru (Mungu wa Ajabu) !

**ਜਿਨ੍ਹਾਂ ਸਿੰਘਾਂ ਸਿੰਘਣੀਆਂ ਨੇ ਧਰਮ ਹੇਤ ਸੀਸ ਦਿੱਤੇ, ਬੰਦ ਬੰਦ ਕਟਾਏ, ਖੋਪਰੀਆਂ ਲੁਹਾਈਆਂ, ਚਰਖੜੀਆਂ ਤੇ ਚੜੇ, ਆਰਿਆਂ ਨਾਲ ਚਿਰਾਏ ਗਏ, ਗੁਰਦੁਆਰਿਆਂ ਦੀ ਸੇਵਾ ਲਈ ਕੁਰਬਾਨੀਆਂ ਕੀਤੀਆਂ, ਧਰਮ ਨਹੀਂ ਹਾਰਿਆ, ਸਿੱਖੀ ਕੇਸਾਂ ਸੁਆਸਾਂ ਨਾਲ ਨਿਬਾਹੀ, ਤਿਨ੍ਹਾਂ ਦੀ ਕਮਾਈ ਦਾ ਧਿਆਨ ਧਰ ਕੇ ਖਾਲਸਾ ਜੀ ! ਬੋਲੋ ਜੀ ਵਾਹਿਗੁਰੂ !**

Fikiria na ukumbuke huduma ya pekee iliyotolewa na wale wanaume mashujaa wa Sikh pamoja na wanawake, ambao walitoa dhabihu vichwa vyao lakini hawakusalimisha Dini yao ya Sikh; ambao walijikata vipande vipande kutoka kwa kila kiungo cha mwili; Ambao waliondolewa vichwa vyao; Ambao walikuwa wamefungwa na kuzungushwa kwenye magurudumu na kuvunjwa vipande vipande; Ambao walikatwa kwa misumeno; Ambao walichunwa wakiwa hai; Waliojitolea mhanga kudumisha heshima ya Wagurdwara; Ambao hawakuiacha imani yao ya Masikh; Ambao walishika Dini yao ya Masikh na wakahifadhi nywele zao ndefu mpaka pumzi yao ya mwisho; Tamka Wahe Guru (Mungu wa Ajabu) !

**ਪੰਜਾਂ ਤਖਤਾਂ, ਸਰਬੱਤ ਗੁਰਦੁਆਰਿਆਂ ਦਾ ਧਿਆਨ ਧਰ ਕੇ ਬੋਲੋ ਜੀ ਵਾਹਿਗੁਰੂ !**

Geuza mawazo yako kwa viti vyote vya Dini ya Sikh na Wagurdwara wote; tamka Wahe Guru (Mungu wa Ajabu) !

**ਪ੍ਰਿਥਮੇ ਸਰਬੱਤ ਖਾਲਸਾ ਜੀ ਕੀ ਅਰਦਾਸ ਹੈ ਜੀ, ਸਰਬੱਤ ਖਾਲਸਾ ਜੀ ਕੋ ਵਾਹਿਗੁਰੂ, ਵਾਹਿਗੁਰੂ, ਵਾਹਿਗੁਰੂ ਚਿਤ ਆਵੇ, ਚਿੱਤ ਆਵਨ ਕਾ ਸਦਕਾ ਸਰਬ ਸੁਖ ਹੋਵੇ।**

Kwanza Khalsa walioheshimiwa wote wanaomba dua hii ili wapate kulitafakari Jina Lako; na raha na starehe zote zije kupitia tafakari hiyo.

**ਜਹਾਂ ਜਹਾਂ ਖਾਲਸਾ ਜੀ ਸਾਹਿਬ, ਤਹਾਂ ਤਹਾਂ ਰਛਿਆ ਰਿਆਇਤ, ਦੇਗ ਤੇਗ ਫ਼ਤਹਿ, ਬਿਰਦ ਕੀ ਪੈਜ, ਪੰਥ ਕੀ ਜੀਤ, ਸ੍ਰੀ ਸਾਹਿਬ ਜੀ ਸਹਾਇ, ਖਾਲਸੇ ਜੀ ਕੇ ਬੋਲ ਬਾਲੇ, ਬੋਲੋ ਜੀ ਵਾਹਿਗੁਰੂ !**

Popote anapokuwa Khalsa, mpe ulinzi na neema Yako; Jikoni huru na upanga kamwe zisije kushindwa; Dumisha heshima ya waja wako; Wape ushindi watu wa Sikh; Upanga unaoheshimiwa uje kutusaidia kila wakati; Na Khalsa wapate heshima daima; Tamka Wahe Guru (Mungu wa Ajabu) !

**ਸਿੱਖਾਂ ਨੂੰ ਸਿੱਖੀ ਦਾਨ, ਕੇਸ ਦਾਨ, ਰਹਿਤ ਦਾਨ, ਬਿਬੇਕ ਦਾਨ, ਵਿਸਾਹ ਦਾਨ, ਭਰੋਸਾ ਦਾਨ, ਦਾਨਾਂ ਸਿਰ ਦਾਨ, ਨਾਮ ਦਾਨ, ਸ੍ਰੀ ਅੰਮ੍ਰਿਤਸਰ ਜੀ ਦੇ ਇਸ਼ਨਾਨ, ਚੌਂਕੀਆਂ, ਝੰਡੇ, ਬੁੰਗੇ, ਜੁਗੋ ਜੁਗ ਅਟੱਲ, ਧਰਮ ਕਾ ਜੈਕਾਰ, ਬੋਲੋ ਜੀ ਵਾਹਿਗੁਰੂ ! ! !**

Tafadhali wape Masingasinga zawadi ya Kalasinga, zawadi ya nywele ndefu, zawadi ya kushika sheria za Sikh, zawadi ya ujuzi wa kimungu, zawadi ya imani thabiti, zawadi ya imani na zawadi kubwa zaidi ya Jina. Ee Mungu ! Waimbaji, kasri na mabango viwepo milele; ukweli na ushinde milele; tamka Wahe Guru (Mungu wa Ajabu) !

**ਸਿੱਖਾਂ ਦਾ ਮਨ ਨੀਵਾਂ, ਮਤ ਉੱਚੀ ਮਤ ਦਾ ਰਾਖਾ ਆਪ ਵਾਹਿਗੁਰੂ।**

Akili za Masingasinga wote zibaki kuwa nyenyekevu na hekima yao imeinuliwa; Ee Mungu ! Wewe ndiye mlinzi wa hekima.

**ਹੇ ਨਿਮਾਣਿਆਂ ਦੇ ਮਾਣ, ਨਿਤਾਣਿਆਂ ਦੇ ਤਾਣ, ਨਿਓਟਿਆਂ ਦੀ ਓਟ, ਸੱਚੇ ਪਿਤਾ, ਵਾਹਿਗੁਰੂ ! ਆਪ ਦੇ ਹਜ਼ੂਰ.....ਦੀ ਅਰਦਾਸ ਹੈ ਜੀ।**

Ee Baba wa Kweli, Wahe Guru ! wewe ndiwe heshima ya wapole, Nguvu ya wanyonge, kimbilio la wasio na makao, tunafanya maombi kwa unyenyekevu mbele zako.....( badilisha tukio au maombi yaliyofanywa hapa).

**ਅੱਖਰ ਵਾਧਾ ਘਾਟਾ ਭੁੱਲ ਚੁੱਕ ਮਾਫ ਕਰਨੀ। ਸਰਬੱਤ ਦੇ ਕਾਰਜ ਰਾਸ ਕਰਨੇ।**

Tafadhali tusamehe makosa na mapungufu yetu katika ukariri wa ombi lililo hapo juu. Tafadhali timiza malengo ya wote.

**ਸੇਈ ਪਿਆਰੇ ਮੇਲ, ਜਿਨ੍ਹਾਂ ਮਿਲਿਆਂ ਤੇਰਾ ਨ ਚਿੱਤਆਵੇ। ਨਾਨਕ ਨਾਮ ਚੜ੍ਹਦੀ ਕਲਾ, ਤੇਰੇ ਭਾਣੇ ਸਰਬੱਤ ਦਾ ਭਲਾ।**

Tafadhali tufanye tukutane na waja wa kweli ambao tukikutana, tunaweza kukumbuka na kutafakari juu ya Jina Lako. Ee Mungu ! kupitia kwa Guru Nanak wa kweli, Jina Lako litukuzwe, na wote wafanikiwe kulingana na mapenzi Yako.

**ਵਾਹਿਗੁਰੂ ਜੀ ਕਾ ਖ਼ਾਲਸਾ, ਵਾਹਿਗੁਰੂ ਜੀ ਕੀ ਫਤਹਿ**

Khalsa ni ya Mungu; ushindi wote ni ushindi wa Mungu.

## Anza Safari ya Nafsi: Tunza Roho Yako

Gundua mazoea ya kuinua safari yako ya kiroho na kupata maana zaidi ya maisha.

Kanuni tatu msingi za Sikhism katika safari:

**Naam Japna:** kumkumbuka Mungu

**Kirat Karni:** fanya kazi kwa uaminifu

**Vand Chhakna:** Kugawana na wengine

Tuongoze na kutuelekeza kwenye ukombozi wa kiroho (mukti) na jamii yenye uadilifu. Kanuni hizi, zilizowekwa katika Guru Granth Sahib, huunda msingi wa maisha ya Sikh.

**Hekima ya 4 ya Guru Ram Das Ji kwa Mazoezi ya Kila Siku:** Katika Guru Granth Sahib (kurasa 305-306), Anatoa umaizi wa kina kuhusu safari ya kiroho ya kila siku ya Sikh:

**Kazi ya Kwanza ya Siku:** Mwanafunzi wa kweli wa Guru huanza kila siku kwa kumkumbuka Mungu kwa upendo.

**Safisha Mwili na Akili:** Amka mapema, oga, kisha jitumbukize katika ukumbusho wa Mungu, ukihisi nafsi yako ikiwa imeoshwa na nekta ya kimungu.

**Kutolewa Kupitia Ukumbusho:** Kufuata mafundisho ya Guru na kukumbuka Jina la Mungu katika ibada huondoa mateso na msukosuko wa ndani unaosababishwa na viambatisho vya kidunia.

**Imba na Tafakari:** Imba sifa za Kimungu bila kusita na kutafakari Jina la Mungu katika shughuli zako za kila siku.

**Kuwa Mwanga wa Amani:** Mfuasi wa Guru ambaye hukumbuka kwa upendo Jina la Mungu kwa kila pumzi hupata nafsi tulivu na yenye kutia moyo.

**Pokea Hekima ya Kimungu:** Guru anatoa hekima hii ya kina juu ya wale ambao wamepata neema Yake.

**Wahimize Wengine:** Guru Nanak anainama kwa mfuasi ambaye hakumbuki Jina la Mungu lakini pia huwahimiza wengine kufanya vivyo hivyo.

**Nafsi Adimu na za Thamani:** Watu waliojitoa kikweli ni wachache sana, hata hivyo kukumbuka kwao manufaa ya Kimungu kunawanufaisha wengine wengi sana kiroho.

**Epuka Ukaidi:** Jitenge na wale wanaopuuza mafundisho ya Guru na kubaki wamenaswa katika mzunguko wa ujinga wa kiroho. Jihadhari na wale wanaozungumza kwa utamu mbele yako lakini wanaeneza mambo hasi nyuma ya mgongo wako.

# Falsafa ya Safari

Falsafa ya Sikhism ina sifa ya mantiki, ufahamu na mbinu yake "bila frills" kwa ulimwengu wa kiroho na wa kimwili. Theolojia yake ina alama ya urahisi. Katika maadili ya Sikh hakuna mtafaruku kati ya wajibu wa mtu binafsi na ule kwa jamii (sangat).

Kalasinga ndiyo dini changa zaidi ulimwenguni iliyoanzishwa na Guru Nanak miaka 500 hivi iliyopita. Inasisitiza imani katika Mtu Mmoja Mkuu na Muumba (Waheguru) wa ulimwengu. Inatoa njia rahisi iliyonyooka inayoelekeza kwenye furaha ya milele na kueneza ujumbe wa upendo na udugu ulimwenguni kote. Kalasinga ni imani ya kumwamini Mungu mmoja na inamtambua Mungu kuwa ndiye pekee asiyewekewa mipaka ya muda au nafasi. Kalasinga inaamini kwamba kuna Mungu mmoja tu, ambaye ni Muumba, Mlinzi, Mwangamizi na hachukui umbo la mwanadamu. Nadharia ya kuzaliwa katika umbo jipya haina nafasi katika Kalasinga. Haiambatanishi thamani yoyote kwa miungu na miungu ya kike na miungu mingine.

Katika Sikhism maadili na dini huenda pamoja. Mtu lazima azingatie sifa za kimaadili na kutenda wema katika maisha ya kila siku ili kupiga hatua kuelekea ukuaji wa kiroho. Sifa kama vile uaminifu, huruma, ukarimu, subira na unyenyekevu zinaweza tu kujengwa na juhudi na ustahimilivu. Maisha ya Guru wetu Wakuu ni chanzo cha msukumo katika mwelekeo huu. Dini ya Sikh inafundisha kwamba lengo la maisha ya mwanadamu ni kuvunja mzunguko wa kuzaliwa na kifo na kuunganishwa na Mungu. Hili linaweza kukamilishwa kwa kufuata mafundisho ya Guru, kutafakari juu ya Jina Takatifu (Naam) na kutenda matendo ya huduma na hisani.

Naam Marg anasisitiza kujitoa kila siku kwa ukumbusho wa Mungu. Mtu anapaswa kudhibiti hisia tano, yaani, Kam (Tamaa), Krodh (hasira), Loabh (choyo), Moh (kushikamana na ulimwengu) na Ahankar (kiburi) ili kufikia wokovu. muungano Taratibu na desturi za kawaida kama vile kufunga na kuhiji, ishara na uthabiti zimekataliwa katika dini ya Sikh. Lengo la maisha ya mwanadamu ni kuungana na

Mungu na hili linatimizwa kwa kufuata mafundisho ya Guru Granth Sahib. Kalasinga inasisitiza Bhagti Marg au njia ya kujitolea. Hata hivyo, inatambua umuhimu wa Gian Marg (Njia ya Maarifa) na Karam Marg (Njia ya Kitendo). Inatilia mkazo mkubwa zaidi juu ya hitaji la kupata Neema ya Mungu ili kufikia lengo la kiroho.

Kalasinga ni dini ya kisasa, yenye mantiki na ya vitendo. Inaamini kwamba maisha ya kawaida ya familia (Grahast) sio kizuizi kwa wokovu. Useja au kuukana ulimwengu sio lazima ili kupata wokovu. Inawezekana kuishi kwa kujitenga katikati ya magonjwa na majaribu ya kidunia. Mshiriki lazima aishi ulimwenguni huku akiweka kichwa chake juu ya mvutano na msukosuko wa kawaida. Lazima awe mwanajeshi msomi, na mtakatifu wa Mungu.

Kalasinga ni ya ulimwengu wote na "dini ya kidunia" na hivyo inakataa tofauti zote katika vigezo vya tabaka, imani, rangi au jinsia. Inaamini kwamba wanadamu wote ni sawa machoni pa Mungu. Gurus walisisitiza juu ya usawa wa wanawake na walikataa mauaji ya watoto wachanga na mazoezi ya Sati (kuwachoma wajane). Pia walieneza kikamilifu kuolewa tena kwa wajane na kukataa mfumo wa purdah (wanawake kujifunika). Ili kuweka akili ikimlenga Yeye ni lazima alitafakari Jina takatifu (Naam) na kufanya matendo ya huduma na mapendo. Inachukuliwa kuwa ni heshima mtu kupata riziki kupitia kazi ya uadilifu (Kirat Karna) na sio kwa njia ya kuomba omba au isiyo ya uaminifu. Vand Chhakna, kugawana na wengine, pia ni wajibu wa kijamii. Mtu huyo anatarajiwa kusaidia wale wanaohitaji, kupitia Daswandh (10% ya mapato yake). Seva, huduma ya jamii pia ni sehemu muhimu ya Kalasinga. Jiko la bure la jumuiya (langar) linalopatikana katika kila gurdwara na lililo wazi kwa watu wa dini zote ni kielelezo kimoja cha huduma hii ya jamii.

Dini ya Sikh inatetea mawazo chanya na matumaini. Haikubali itikadi ya kukata tamaa. Guru waliamini kwamba maisha haya yana kusudi na lengo. Inatoa fursa kwa ubinafsi na utambuzi wa Mungu. Aidha mwanadamu anawajibika katika matendo yake mwenyewe. Hawezi kudai kinga kutokana na matokeo ya matendo yake. Kwa hiyo lazima awe macho sana katika kile anachofanya. Maandiko ya Sikh, Guru Granth Sahib, ni Guru wa Milele. Hii ndiyo dini pekee ambayo imekipa Kitabu Kitakatifu hadhi ya kiongozi wa kidini. Hakuna mahali pa mtu aliye hai Guru (Dehdhari) katika dini ya Sikh.

## Wajibu wa wanawake katika Sikhism

Kanuni za Sikhism zinasema kwamba wanawake wana nafsi sawa na wanaume na wana haki sawa ya kukuza hali yao ya kiroho. Wanaweza kuongoza makutaniko ya kidini, kushiriki katika Njia ya Akhand (ukariri unaoendelea wa Maandiko Matakatifu), kuimba Kirtan (uimbaji wa tenzi katika kusanyiko), kufanya kazi kama Granthis (makuhani). Wanaweza kushiriki katika shughuli zote za kidini, kitamaduni, kijamii, na za kilimwengu. Sikhism ilikuwa dini kuu ya kwanza duniani kutoa usawa kwa wanaume na wanawake. Guru Nanak, alihubiri usawa wa kijinsia, na wakuu waliomfuata waliwatia moyo wanawake kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za ibada na mazoezi ya Sikh.

### Guru Granth Sahib inasema,

"Wanawake na wanaume, wote wameumbwa na Mungu. Haya yote ni mchezo wa Mungu. Anasema Nanak, viumbe vyako vyote ni vyema na vitakatifu" -SGGS uk.304

Historia ya Sikh imeandika jukumu la wanawake kuwaonyesha kama sawa katika huduma, kujitolea, kujitoa mhanga, na ushujaa kwa wanaume. Mifano mingi ya heshima ya maadili ya wanawake, huduma, na kujitolea imeandikwa katika mila ya Sikh.

Kulingana na Sikhism, wanaume na wanawake ni pande mbili za sarafu moja. Katika mfumo wa mahusiano na kutegemeana ambapo mwanamume huzaliwa kutoka kwa mwanamke, na mwanamke huzaliwa kutoka kwa mbegu ya mwanamume. Kulingana na Sikhism, mwanamume hawezi kujisikia salama na kamili katika maisha yake bila mwanamke, na mafanikio ya mwanamume yanahusiana na upendo na msaada wa mwanamke ambaye anashiriki maisha yake pamoja naye, na kinyume chake. Guru Nanak alisema:

"[ni] mwanamke ambaye huendeleza mbio" na kwamba hatupaswi "kumfikiria mwanamke kuwa aliyelaaniwa na kuhukumiwa, [wakati] kutoka kwa mwanamke huzaliwa viongozi na wafalme." SGGS Ukurasa wa 473.

**Wokovu:** Jambo muhimu la kuzungumziwa ni kama dini inawachukulia wanawake kuwa na uwezo wa kupata wokovu, utambuzi wa Mungu hapa au ulimwengu wa juu zaidi wa kiroho. Guru Granth Sahib inasema,

"Katika viumbe vyote ni Bwana aliyeenea, Bwana anazunguka kila aina ya kiume na kike" (Guru Granth Sahib, p.605).

Kutokana na kauli iliyo hapo juu kutoka kwa Guru Granth Sahib, nuru ya Mungu inakaa sawia kwenye jinsia zote mbili. Wanaume na wanawake basi wanaweza kupata wokovu sawa kwa kufuata mafundisho ya Guru. Katika dini nyingi, mwanamke anachukuliwa kuwa kizuizi kwa hali ya kiroho ya mwanamume, lakini si katika Sikhism. Guru anakataa hili. Katika 'Mawazo ya Sasa juu ya Sikhism', Alice Basarke anasema,

"Guru wa kwanza aliweka mwanamke sawa na mwanamume ... mwanamke hakuwa kizuizi kwa mwanamume, lakini mshirika katika kumtumikia Mungu na kutafuta wokovu".

**Ndoa:** Guru Nanak alipendekeza grhastha—maisha ya mwenye nyumba, Badala ya useja na kujinyima, Mume na mke walikuwa washirika sawa na uaminifu uliamrishwa kwa wote wawili. Katika aya takatifu, furaha ya nyumbani inaonyeshwa kama jambo linalotunzwa na ndoa ilitoa sitiari inayoendelea kwa ajili ya maonyesho ya upendo kwa Mungu. Bhai Gurdas, mshairi wa Sikhism ya mapema na mkalimani mwenye mamlaka wa mafundisho ya Sikh, hutoa sifa kuu kwa wanawake. Anasema:

"Mwanamke ndiye kipenzi katika nyumba ya wazazi wake, anapendwa sana na baba na mama yake. Nyumbani kwa wakwe zake, yeye ndiye nguzo ya familia, dhamana ya bahati nzuri ... Kushiriki katika hekima ya kiroho. na nuru na sifa tukufu zilizojaaliwa, mwanamke, nusu nyingine ya mwanamume, humsindikiza hadi kwenye mlango wa ukombozi." (Varan, V.16)

**Hali Sawa:** Ili kuhakikisha hadhi sawa kati ya wanaume na wanawake, Guru hawakutofautisha jinsia katika masuala ya unyago, mafundisho au kushiriki katika

shughuli za sangat (ushirika mtakatifu) na pangat (kula pamoja). Kulingana na Sarup Das Bhalla, Mahima Prakash, Guru Amar Das alipinga matumizi ya hijabu kwa wanawake. Aliwapa wanawake kazi ya kusimamia baadhi ya jumuiya katika wanafunzi na kuhubiri kinyume na desturi ya shibe. Historia ya Sikh inarekodi majina ya wanawake kadhaa, kama vile Mata Gujri Mai Bhago, Mata Sundari, Rani Sahib Kaur, Rani Sada Kaur na Maharani Jind Kaur, walioyachukua majukumu muhimu katika matukio ya wakati wao.

**Elimu:** Elimu inachukuliwa kuwa muhimu sana katika Kalasinga. Ni ufunguo wa mafanikio ya mtu yeyote. Ni mchakato wa maendeleo ya kibinafsi na ndio sababu Guru ya ३ kuanzisha shule nyingi. Guru Granth Sahib inasema,

"Maarifa yote ya kiungu na tafakari hupatikana kupitia Guru" (Guru Granth Sahib, p.831).

Elimu kwa wote ni muhimu na kila mtu lazima afanye kazi ili kuwa bora zaidi. Hamsini na wawili kati ya wamishonari wa Sikh waliotumwa na Guru wa ३ walikuwa wanawake. Katika, 'Wajibu na Hali ya Wanawake wa Sikh', Dk Mohinder Kaur Gill anaandika, "Guru Amar Das alishawishika kuwa hakuna mafundisho yanayoweza kuota mizizi mpaka na yasipokubaliwa na wanawake".

**Vizuizi vya Nguo:** Mbali na kuwataka wanawake wasivae stara, dini ya Kalasinga hutoa taarifa rahisi lakini muhimu sana kuhusu kanuni za mavazi. Hii inatumika kwa Sikhs wote bila kujali jinsia. Guru Granth Sahib inasema,

"Epuka kuvaa nguo ambazo haziuridhishi mwili na akili imejaa mawazo mabaya." SGGS, Ukurasa wa 16

Kwa hivyo, Sikhs watatambua ni aina gani ya nguo zinazojaza akili mawazo mabaya na wanapaswa kuziepuka. Wanawake wa Sikh wanatarajiwa kujitetea kwa Kirpan (upanga) na njia zingine, hili ni jambo la kipekee kwa wanawake kwa

sababu ni mara ya kwanza katika historia ambapo wanawake walitarajiwa kujitetea bila kuwategemea wanaume kwa ulinzi wa kimwili.

**Nukuu za SGGS:** "Katika ardhi na angani, simwoni yeyote wa pili. Miongoni mwa wanawake na wanaume, Nuru Yake inang'aa." Sggs Page 223.

Kutoka kwa mwanamke, mwanamume huzaliwa; ndani ya mwanamke, mwanamume anatungwa mimba; kwa mwanamke anachumbiwa na kuolewa. Mwanamke anakuwa rafiki yake; kupitia mwanamke, vizazi vijavyo huja. Mwanamke wake akifa, anatafuta mwanamke mwingine; kwa mwanamke amefungwa. Basi kwa nini kumwita mbaya? Kutoka kwake, wafalme wanazaliwa. Kutoka kwa mwanamke, mwanamke huzaliwa; bila mwanamke, kusingekuwa na mtu kabisa. Guru Nanak, SGGS Ukurasa 473

**Kuhusiana na mahari:** "Ewe Mola wangu, nipe jina lako kama zawadi yangu ya harusi na mahari." Shri Guru Ram Das ji, Ukurasa wa 78, mstari wa 18 SGGS

**Kuhusu zoezi la Purdah:** "Kaa, kaa, ewe binti-mkwe - usiufunike uso wako kwa pazia. Mwishowe, hili halitakuletea hata nusu ya ganda. Yule aliye kabla yako alikuwa akifunika uso wake kwa pazia. msifuate nyayo zake, sifa pekee ya kufunika uso wako ni kwamba kwa muda wa siku chache watu watasema, "Ni bibi arusi mtukufu gani amekuja." Pazia lako litakuwa kweli ikiwa tu utaruka, kucheza na kuimba sifa kuu za Mungu.-Uk.484, SGGS

Wanawake na kwa hakika nafsi zote zilihimizwa sana kuishi maisha ya kiroho: "Njooni, dada zangu wapendwa na masahaba wa kiroho; nikumbatieni karibu katika busu lenu. Hebu tuungane pamoja, na tusimulie hadithi za Bwana Mume wetu Mwenye Nguvu Zote."- Guru Nanak, ukurasa wa 17, SGGS.

“Rafiki, uvaaji mwingine wote huharibu furaha, uvaaji ambao kwa viungo vya mwili ni mateso, na ambao hujaza mawazo machafu akilini”-SGGS Ukurasa 16

## Umuhimu wa Turban

Turban ni na imekuwa sehemu isiyoweza kutenganishwa ya maisha ya Sikh. Kutoka takriban mwaka wa 1500 A.D na wakati wa Guru Nanak, mwanzilishi wa Sikhism, Sikhs wamepamba kilemba.

kilemba au "pagri" mara nyingi hufupishwa kuwa "pag" au "dastar" ni maneno tofauti katika lahaja mbalimbali zinazoashiria kitu kimoja. Maneno haya yote yanahusu vazi linalovaliwa na wanaume na wanawake kufunika vichwa vyao. Ni vazi la kichwa linalojumuisha kitambaa kirefu kinachofanana na kitambaa kinachofungwa kichwani au wakati mwingine "kofia" ya ndani au patka. Kitamaduni nchini India kilemba kilivaliwa tu na wanaume wa hadhi ya juu katika jamii; wanaume wa hali ya chini au wa tabaka la chini hawakuruhusiwa kuvaa kilemba.

Ingawa kutunza nywele ambazo hazijanyolewa kuliamriwa na Guru Gobind Singh kama mojawapo ya K tano au kanuni za imani, kwa muda mrefu imekuwa ikihusishwa kwa ukaribu na Kalasinga tangu mwanzo wa Sikhi mnamo 1469. Kalasinga ndiyo dini pekee ulimwenguni katika ambayo kuvaa kilemba ni lazima kwa wanaume wote wazima. Idadi kubwa ya watu wanaovaa vilemba katika nchi za Magharibi ni Masingasinga. Sikh pagdi pia huitwa dastaar. Dastaar ni neno la heshima zaidi katika Kipunjabi. Jina hili likitafsiriwa humaanisha "Mkono wa Mungu" kuashiria bbaraka zake.

Masingasinga ni maarufu kwa vilemba vyao vingi na vya kipekee. Kijadi, kilemba kinawakilisha heshima, na kwa muda mrefu kimekuwa kitu ambacho kilihifadhiwa kwa waungwana pekee. Wakati wa utawala wa Mughal wa India, ni Waislamu pekee walioruhusiwa kuvaa kilemba. Wasio Waislamu wote walizuiliwa kabisa kuvaa pagri.

Guru Gobind Singh, katika kupinga ukiukwaji huu wa Mughals aliwataka Masingasinga wake wote kuvaa kilemba. Hili lilipaswa kuvaliwa kwa kutambua viwango vya juu vya maadili ambavyo alikuwa ameviweka kwa wafuasi wake wa Khalsa. Alitaka Khalsa wake awe tofauti na aazimie "kujitofautisha na ulimwengu wote" na kufuata njia ya kipekee ambayo ilikuwa imetolewa na Ma-Sikh Gurus. Hivyo basi, Sikh mwenye kilemba amejitokeza kila mara kutoka kwa umati, kama Guru alivyokusudia; kwani alitaka 'Watakatifu-Askari' wake watambulike kwa urahisi huku wakipatikana kwa urahisi pia.

Wakati mwanaume au mwanamke wa Sikh akivaa kilemba, kilemba hukoma kuwa mkanda wa nguo tu; kwa maana kinakuwa sawa na kichwa cha Sikh. Kilemba, pamoja na nguo nyingine nne za imani huvaliwa na Sikhs, kina umuhimu mkubwa wa kiroho na kimwili. Ingawa ishara zinazohusishwa na kuvaa kilemba ni nyingi - ukuu, kujitolea, kujistahi, ujasiri na uchaji Mungu, lakini!, sababu kuu ambayo Masingasinga huvaa kilemba ni kuonyesha - upendo wao, utiifu na heshima kwa mwanzilishi wa Kanisa. Khalsa Guru Gobind Singh.

"Kilemba ni zawadi ya Guru wetu kwetu. Ni jinsi tunavyojivika taji kama akina Singh na Kaurs ambao huketi kwenye kiti cha kujitolea kwa ufahamu wetu wa hali ya juu. Kwa wanaume na wanawake sawia, utambulisho huu wa kuvutia unaonyesha ufalme, neema, na pekee. . Ni ishara kwa wengine kwamba tunaishi katika hali ya milelena tumejitolea kuwatumikia wote. Kilemba hakiwakilishi chochote isipokuwa kujitolea kamili. Unapochagua kujitokeza kwa kufunga kilemba chako, unasimama bila woga kama mtu binafsi kati ya watu bilioni sita. Ni kitendo cha kipekee."

## Unyenyekevu Muhimu Katika Safari Yako

Unyenyekevu ni kipengele muhimu cha Sikhism. Kulingana na hili, Masingasinga lazima wainame kwa unyenyekevu mbele za Mungu. Unyenyekevu au Nimrata, katika Kipunjabi ni maneno yanayohusiana kwa karibu. Nimrata ni fadhila ambayo inakuzwa kwa nguvu huko Gurbani. Tafsiri ya neno hili la Kipunjabi ni **"Ufadhili"** au **"Unyenyekevu"**. Mtu ambaye akili yake haijakengeushwa na mawazo kwamba yeye ni bora au muhimu zaidi kuliko mtu.

Eneo la tatizo - sio sentensi sahihi hapo juu

Hii ni sifa muhimu ambayo kila mwandamu anafaa kuitunza na ambayo ni sehemu muhimu ya kuweka mawazo ya Sikh na ubora huu lazima uambatane na Sikh wakati wote. Sifa nyingine nne katika hifadhi ya Sikh ni:
Ukweli (Sat), Kuridhika (Santokh), Huruma (Daya) na Upendo(Pyaar).

Sifa hizi tano ni muhimu kwa Sikh na ni wajibu wao kutafakari na kusoma Gurbani ili kuingiza maadili haya na kuwafanya sehemu ya utu wao.

**Anachotwambia Gurbani:**
"Tunda la unyenyekevu ni amani na raha angavu. Kwa unyenyekevu wanaendelea kumtafakari Mungu, Hazina ya ubora. Mtu anayemcha Mungu amezama katika unyenyekevu. Mtu ambaye moyo wake umebarikiwa kwa unyenyekevu wa kudumu. Sikhism inashughulikia Unyenyekevu huchukuliwa kama bakuli ya ombaomba mbele ya mungu"

**Guru Nanak, Guru wa Kwanza wa Kalasinga:**

"Kusikiliza na kuamini kwa upendo na unyenyekevu akilini mwako jitakase kwa Jina, kwenye mahali patakatifu ndani kabisa." - SGGS Ukurasa 4.

"Fanya kuridhika kuwa hereni za masikio yako, unyenyekevu bakuli lako la kuomba, na kutafakari majivu unayopaka mwilini mwako." -SGGS Ukurasa wa 6.

"Katika nyanja ya unyenyekevu, Neno ni Uzuri. Miundo ya uzuri usio na kifani hutengenezwa hapo." SGGS Ukurasa wa 8.

"Kiasi, unyenyekevu na ufahamu angavu ni mama mkwe wangu na baba mkwe" - SGGS Ukurasa 152.

# Safari kuelekea Kiroho

Guru Granth Sahib ni Guru aliye hai wa milele, muundo wa kishairi wa Sikh Gurus, Watakatifu wa Kihindu na Waislamu. Mkusanyiko huo ni zawadi kutoka kwa Mungu kupitia kwao kwa wanadamu wote. Maono yaliyo katika Guru Granth Sahib ni ya jamii yenye msingi wa haki ya Kimungu bila ukandamizaji wa aina yoyote. Ingawa Granth inakubali na kuheshimu maandiko ya Uhindu na Uislamu, haimaanishi upatanisho wa maadili na mojawapo ya dini hizi. Katika Guru Granth Sahib wanawake wanaheshimiwa sana na majukumu sawa kama wanaume. Wanawake wana roho sawa na wanaume na hivyo wana haki sawa ya kukuza hali yao ya kiroho na nafasi sawa ya kupata ukombozi. Wanawake wanaweza kushiriki katika shughuli zote za kidini, kitamaduni, kijamii, na kidunia ikiwa ni pamoja na kuongoza makutano ya kidini.

Sikhism inatetea usawa, haki ya kijamii, huduma kwa ubinadamu, na uvumilivu kwa dini zingine. Ujumbe muhimu wa Kalasinga ni ibada ya kiroho na uchaji wa Mungu wakati wote huku ukitekeleza maadili ya huruma, uaminifu, unyenyekevu na ukarimu katika maisha ya kila siku. Kanuni tatu za msingi za dini ya Sikh ni kutafakari na kumkumbuka Mungu, Kufanya Kazi ili kuishi kwa Uaminifu na kugawana na wengine. Hongera kwa kufanya jitihada za kuendelea na Safari hii ya Kiroho kwa ajili ya nafsi. Tafsiri haiwezi kamwe kuwa karibu na asilia, hasa pale ambapo Guru Granth Sahib kamili iko katika ushairi na matumizi ya sitiari hufanya kazi kuwa ngumu sana. Katika ujumbe wa Kiungu, hadithi za ngano za Kihindu na Kiislamu mara nyingi hutumiwa Pralahad , Harnakash, laxmi, Brahma n.k. Tafadhali usizisome uhalisia wake bali uelewe ujumbe wao wa ndani. Sisitizo kuu ni kwamba Mungu ni mmoja na kuwa na ushirika naye ndilo lengo la maisha ya mwanadamu.

Kazi hii imefanywa kwa miaka mingi na watu kadhaa waliojitolea, ili kukuletea ujumbe wa Kimungu katika lugha yako. Ikiwa una maswali yoyote, tafadhali jisikie huru kutuma barua pepe kwa walnut@gmail.com na tungependa kujiunga nawe katika safari hii.